Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Sita – Tarehe 16 Juni, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 42

**Kazi na Taarifa ya Tume ya Pamoja ya Fedha**

**MHE. ALI AMEIR MOHAMED** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tume ya Pamoja ya Fedha iliyoundwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikamilisha kazi ya kuandaa mapendekezo zaidi ya miaka miwili iliyopita ya namna bora ya kugawana gharama na mapato katika uendeshaji wa Serikali ya Muungano wetu, na kwa kuwa mpaka sasa hakuna chochote kilichotangazwa kuhusu kazi hiyo ya Tume ya Fedha na kufanya utekelezaji wake kutoonekana:-

(a) Je, Serikali inaweza kuliambia Bunge hili kuhusu Kazi na Taarifa ya Tume hiyo?

(b) Je, Serikali inaweza kueleza sababu za msingi za ucheleweshaji au ukimya huo kuhusu mapendekezo ya Tume hiyo hasa ikitiliwa maanani kuwa, Serikali zetu mbili zimekuwa na Mikutano ya pamoja na kuzungumzia masuala ya kuwezesha uendeshaji bora wa Muungano?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali A. Mohamed, Mbunge wa Donge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Tume ya Pamoja ya Fedha imeundwa mwezi Juni, 2003 kwa Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha Sura ya 140 ya mwaka 1996 (*The Joint Finance Commission Act Cap. 140 of 1996*) na kazi zake zimeanishwa katika Ibara za 133 na 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama ifuatavyo:-

- Kuamua kiasi kitakachochangwa na Serikali mbili na kuwekwa kwenye akaunti ya Fedha ya Pamoja kwa madhumuni ya shughuli za Jamhuri ya Muungano kwa mambo ya Muungano.

- Kuchambua mapato na matumizi yatokanayo na, au yanayohusu utekelezaji wa mambo ya Muungano, na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mchango na mgawo wa kila mojawapo ya Serikali hizo.

- Kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za fedha za Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika mambo ya kifedha kati ya Serikali mbili.

- Kutekeleza majukumu mengine ambayo Rais ataipatia Tume au kama Rais atavyoagiza, na kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Pamoja na Fedha imeshawasilisha taarifa yake kwa Mawaziri wanaohusika wa SMT na SMZ.

Kwa upande wa SMZ taarifa hiyo imeshawasilishwa katika ngazi ya Baraza la Mapinduzi na kwa upande wa SMT utaratibu unakamilishwa ili taarifa iwasilishwe katika ngazi ya Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakiri kwamba jambo hili limechukua muda mrefu. Hata hivyo inatupasa tukubali pia kuwa hili si jambo jepesi, bali ni jambo linalopasa kuangaliwa kwa kina na vyombo husika kwani linagusa maslahi ya Taifa na wananchi wa pande zote mbili za Muungano. Jambo hili lilishajadiliwa na Baraza la Mapinduzi kwa upande wa SMZ.

Kwa upande wa SMT liliwasilishwa katika vyombo husika na yalitolewa maelekezo kuwa Wizara ya Fedha na Uchumi (SMT) na Wizara ya Fedha (SMZ) wakutane na kujadili taarifa hiyo kwa pamoja kabla ya kuwasilisha katika Baraza la Mawaziri.

Aidha, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa jambo hili lipo katika agenda zetu kwenye Kamati ya Pamoja na SMT na SMZ ambayo wajumbe wake ni pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi na Mawaziri wa

Serikali zote mbili chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Makamu wa Rais na mara tu likipatiwa ufumbuzi taarifa rasmi itatolewa kwa wananchi kupitia vyombo vya habari nchini kama tunavyofanya siku zote kila baada ya vikao hivyo.

**MHE. ALI AMEIR MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa amekiri kwamba jambo hili ni muhimu sana katika uendeshaji wa Muungano wetu na kwa kuwa katika uendeshaji wa mambo makubwa kama Muungano suala la kuchangia mapato na gharama ni suala muhimu sana. Na kwa kuwa Waziri amekiri kwamba jambo hili limechukua muda mrefu Serikali haioni kwamba kwa kuchelewa chelewa kulikamilisha jambo hili inakaribisha manung'uniko makusudi yanayofanywa kuzusha kero za Muungano katika nchi yetu? (*Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema sisi Serikali tunaona umuhimu kwamba kuna haja ya kuharakisha jambo hili, ili limalizike haraka sana. Ndio maana nikasema katika agenda ya vikao vyetu vya Muungano vya Ushirikiano hii ni agenda ambayo imepewa kipaumbele.

Ningependa kutoa pongezi kwa Mwenyekiti wetu wa Tume hii Mheshimiwa Shellukindo kwa jitihada zote alizofanya kuhakikisha kwamba wao kazi yao wameshamaliza na naahidi kwamba kwa muda mfupi tutajitahidi kulimaliza suala hili ili kero hiyo iondoke.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa suala hili limeshaulizwa Bungeni zaidi ya mara mbili sasa na kwa kuwa Serikali siku zote majibu yao ni hayohayo. Na kwa kuwa kwa upande wa Zanzibar Baraza la Mapinduzi wameshakaa na kuamua na inachoonekana huku ni kikwazo Baraza la Mawaziri. Na kwa vile sio suala hilo tu ambalo linaulizwa na tumeshazoea majibu ya siku zote ya namna hiyo Waziri anaweza akatueleza sasa ni lini litakamilika kama kweli upande wa Jamhuri ya Muungano una nia njema kwa upande wa Zanzibar?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar ni Serikali ya CCM. Ni Serikali ambazo zinajali sana maslahi ya pande zote mbili na napenda kuahidi kwamba tutajitahidi kwa uwezo wote tuharakishe haraka sana jambo hili limalizike.

**MHE.HAMAD RASHID MOHAMED**:Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ni Serikali za CCM. Haoni kwamba anakwenda kinyume cha Katiba ya Serikali ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zanzibar za wananchi wa Tanzania na sio za chama, ila zinaongozwa tu na chama. (*Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani nadhani ilieleweka ni Serikali ya CCM kwa maana kwamba ni Serikali zinazoongozwa na Chama cha Mapinduzi.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa.

Na. 43

**Kuzuia Uchomaji Moto Kwa Mpango**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

Kwa kuwa utafiti wa miaka ya hivi karibuni umeonyeshakuwa, uchomaji moto kwa mpango (*cool/early burning*) hasa katika hifadhi zetu za Taifa kunaharibu na kubadilisha bioanuai hasa za ndege, wadudu na wanyama wadogowadogo:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kurekebisha dhana hiyo ili kuepuka kuvuruga kabisa bioanuai katika hifadhi zetu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba uchomaji moto wa mpango (*Cool/early burning*) hasa katika hifadhi zetu za taifa unaharibu na kubadilisha *bioanuai* hasa za ndege, wadudu na wanyama wadogowadogo.

Pamoja na ukweli huu uchomaji moto wa mpango ni muhimu na umekuwa ukifanyika ili kuweka maeneo ya hifadhi katika hali nzuri kiikolojia ili mradi moto usiwe mwingi uchomwe kwa wakati muafaka na usiwe wa mara kwa mara. Hata hivyo uchomaji moto huu umekuwa ukifanyika katika maeneo yasiyozidi asilimia 33 ya maeneo yaliyo hatarini kutekekezwa na moto haramu kwa malengo yafuatayo:-

- Kuweka makinga moto *(firebreaks*) kuzuia kusambaa kwa moto utokao nje ya hifadhi wakati wa kiangazi.

- Kuhifadhi malisho ya wanyamapori kutokana na mchanganyiko wa maeneo yaliyochomwa na yasiyochomwa; ambapo maeneo yaliyochomwa huwa kama makingamoto (*Fire breaks*).

- Kuinua uzalishaji (*Pasture Productivity*) kwa kuondoa majani ya muda mrefu ili kuruhusu majani laini yanayohitajika kwa ajili ya malisho ya wanyamapori kuweza kumea.

Hata hivyo nia sio kusababisha madhara kwa wanyama wadogo, wadudu na ndege lakini uchomaji moto mpango (*Presicribed early/late burning*) huwawezesha kuhama ili kuupisha moto pale moto unapochomwa kabla nyasi hazijakauka sana. Ingawa ni kweli madhara hayawezi kukosekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zinazochukuliwa na Serikali kurekebisha dhana hiyo ni kama zifuatazo:-

- Kuelimisha jamii zinazozunguka Hifadhi za Taifa kuhusu madhara yanayosababishwa na uchomaji moto ovyo katika maeneo yao wakati wa kusafisha mashamba ambao husambaa hadi kwenye hifadhi na kusababisha uharibifu mkubwa. Shughuli hii hufanywa kupitia mikutano na kuleta viongozi na vikundi vya kijamii hifadhini na kuwapa elimu ya uhifadhi.

- Kuchukua tahadhari dhidi ya kuenea haraka moto katika hifadhi kwa kusafisha (kulima) mipaka ya hifadhi inayopakana na maeneo ambayo moto unaweza kutokea.

- Utekelezaji wa Mkakati wa Kuhifadhi Ardhi na Vyanzo vya Maji wa Machi 2006 kuhusu moto unazingatia hatua zifuatazo: Kutoa zawadi kwa watu au vikundi vya watu watakaotoa taarifa za uchomaji moto misitu na wanaosaidia kuzima moto.

- Kuhakikisha kila hifadhi inakuwa na Mpango wa Matumizi ya Moto *(Fire Management Plan)* ambao utaainisha jinsi moto unavyoweza kutumika au usivyopaswa kutumika ili kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa baadhi ya maeneo kutokana na sababu mbalimbali.
- Kuzuia ujangili ndani ya Hifadhi za Taifa na kusimamia kesi za uhalifu unaoambatana na uchomaji moto kama vile urinaji haramu wa asali na ufukuzaji wa Wanyamapori kwa kutumia moto.

- Mwisho, wataalam kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii na wa *TANAPA* kufanya ziara za mafunzo ili kupata uzoefu wa nchi nyingine na hatua mbadala wanazochukua.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nashukuru kwa majibu ya kina na mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini naomba niulizie zaidi kama ifuatavyo:-

Naamini kwamba kila hifadhi au hifadhi zetu kwa ujumla zina malengo au sera ya uhifadhi ya *bionuwai*. Kwa vile utaratibu huu wa kuchoma bado unateketeza viumbe fulani fulani na kuathiri *bionuwai* ya ujumla (*total bio- diversity*).

Mheshimiwa Waziri atasemaje kuhusu mkanganyiko huu kati ya kuhifadhi (*bio-diversity)* na utaratibu huu unaotumika ambapo tunateketeza viumbe vingine kwa nini usitafutwe namna mbadala ya kuhakikisha kwamba uhifadhi unakuwa ni wa jumla kwa viumbe wote kuliko kuteketeza viumbe vingine na kuwezesha viumbe vichache kuneemeka.

Lakini swali la pili kumetokea utaratibu sasa hivi wa kudharau sana utafiti wa kiikolojia kwenye hifadhi zetu ukilinganisha na miaka ya 1970 na 1980. Matokeo yake ni kwamba vitu vingi hatuvijui vina mwelekeo gani katika hifadhi zetu. Kwa nini Serikali haitengi fedha za kutosha kwa ajili ya utafiti wa ikolojia katika hifadhi zetu za Taifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kuhusu jinsi Serikali itakavyoweza kuwa na uwiano kati ya hifadhi ya *bionuwai* na utaratibu mzima wa kuweza kuweka ikolojia katika hifadhi ili kuweza kupata malisho kwa wanyama wengine.

Mimi ninachosema nchi yetu kama tunavyojua imesaini na imeridhia na ni mwanachama wa Mkataba unaoshughulika na masuala ya *bionuwai* na moja ya majukumu ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na kurudishwa hali ya *bionuwai* haiwezi kupotea.

Kwa hivyo utaratibu unaotumika wa kuchoma moto ni utaratibu ambao unatumika katika maeneo mengi duniani. Nchi ya Canada wanatumia utaratibu huo Mexico, Australia, Marekani na hizi nchi zetu Afrika ya Kusini na wataalamu wa *TANAPA* wiki iliyopita walikuwa katika Mbuga ya Kuga kuweza kuangalia na wenzetu wanafanya nini.

Lakini ni kweli kuna hatua zinazoweza zikachukuliwa ili kupunguza madhara. Hatua ya kama kuwa na *early warning* kuhakikisha kwamba uchomaji unafanywa wa kushtua ili kuwafanya wale wanyama wadogo na nyoka na wengine waweze kuhama ili eneo litakalobaki liweze kuchomwa.

Kwa hivyo utaratibu utafanywa wa kuwa na utaratibu wa kuweza kuhakikisha kwamba madhara yatakuwepo lakini hayatakuwa makubwa ya kuweza kusababisha kuondoka kabisa *bionuwai* ya asili ya maeneo hayo.

Ama kuhusu utafiti ni kweli kabisa suala la utafiti ni suala ambalo lina kipaumbele kidogo kutokana na vipaumbele vingi katika nchi yetu. Lakini tumekubaliana kwamba utafiti sasa hivi na maendeleo ni katika moja ya maeneo ambayo tunaweka uzito, utafiti katika kilimo lakini vile vile katika maeneo hayo ya uhifadhi.

Tunajua wenzetu wa *Frankfurt Zoological Societ* wanatusaidia katika utafiti lakini na sisi tutajaribu kutafuta wengine zaidi na nchi yetu tuweke asilimia katika utafiti kupitia *TANAPA.* Ahsante sana.

Na. 44

**Ujenzi wa Maabara Nchini**

**MHE. ALI KHAMIS SEIF** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika kuhimili tatizo la ufundishaji wa masomo ya Sayansi kwenye shule zetu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, katika Bajeti yake ya 2008/2009 ilikusudia kujenga Maabara kwenye shule mbalimbali nchini:-

(a) Je, ni maabara ngapi mpaka sasa zimejengwa kutokana na ahadi hiyo ya mwaka 2008/2009?

(b) Je, maabara hizo zimepatiwa vifaa vinavyostahili?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI(MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo;-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliahidi kutoa ruzuku ya ujenzi wa vyumba 230 vya Maabara kwa mwaka 2008/2009. Hadi sasa vyumba 182 vya maabara vimejengwa. Ujenzi wa vyumba vilivyobaki unaendelea.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa mpango wa maendeleo ya Elimu ya Sekondari, kila mwaka Serikali inatoa ruzuku ya kununulia vifaa vya kujifunzia na kufundishia, vikiwemo vifaa vya maabara. Katika mwaka 2008/2009, kiasi cha shs.3,965,477,360/= zilitengwa na kugawiwa shuleni kwa ajili ya kununua vifaa vya kujifunzia na kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ruzuku inayotolewa haitoshelezi mahitaji halisi ya kila shule. Wizara, imekuwa ikiwaelekeza wakuu wa shule kununua vifaa hivyo kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa kuwa tatizo la ukosefu wa Maabara ya Sayansi katika shule zetu za Sekondari ni kubwa sana, Serikali imeandaa Mradi mkubwa wa kujenga na kufunga vifaa vya Maabara katika shule zote za Sekondari za Serikali hapa nchini, gharama za mradi wote inakadiriwa kuwa Dola za Kimarekani 592 milioni. Tayari Serikali inajadiliana na washiriki mbalimbali wa maendeleo wakiwemo Benki ya

Dunia (kupitia awamu ya pili ya Mpango wa MES) na Benki ya Maendeleo ya Afrika ili kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza. Je, hizo maabara 44 zilizobakia zitamalizika lini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI(MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, zitamalizika mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mheshimiwa Waziri ningependa kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa maabara inataka walimu ambao ni *laboratory technician* na kwa kuwa shule ambazo zilikuwa zinafundisha *laboratory technician* ziligeuzwa kuwa *University*. Je, hizi Maabara nani anaziendesha iwapo *laboratory technicians* hawapo nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI(MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hii programu niliyoizungumza ambayo itagharamiwa na washiriki wetu wa maendeleo inayo *component* ya *training* ya ku-*train laboratory technicians* ili waweze kwenda katika mashule kusaidia katika ufundishaji na uandaaji wa sayansi kabla ya kufundisha. Lakini kwa sasa hivi tumewaomba wale walimu wa sayansi waanze kufanya hiyo kazi ya *technician* kuandaa na kuanza kufundisha kwa ku-*improvise*.

Na. 45

**Kukifanya Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara cha Moshi kuwa Chuo Kikuu**

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara cha Moshi *(MUCOBS*) kina kila sifa na sababu ya kuwa Chuo Kikuu kamili:-

(a) Je, ni lini Serikali itakifanya *MUCOBS* kuwa Chuo Kikuu kamili?

(b) Je, Kitivo cha Kizumbi, ambacho ni kikubwa kuliko vitivo vyote vya chuo hicho kitakuwa na nafasi gani ya maendeleo ya Chuo Kikuu kipya ikiamuliwa hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI(MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa tarehe 5 Juni, 2009 Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara Moshi kimepata Hati idhini kamili kama ilivyowekwa chini ya Sheria Na. 8 ya mwaka 2005 ya Vyuo Vikuu (*The Universities Act. No.8 of 2005*). Hii ni hatua muhimu ya Chuo hicho Kishiriki kuelekea katika kuwa Chuo Kikuu kamili. Kwa sasa, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara cha Moshi hakijawa tayari kuwa Chuo Kikuu kamili. Chuo kitakuwa na sifa hizo hapo kitakapokamilisha matakwa yote yaliyowekwa na Kamisheni ya Vyuo Vikuu Tanzania *(Tanzania Commission for Universities*) ya Chuo Kishiriki kama *MUCCOBS* kuwa Chuo Kikuu kamili. *(Makofi)*

Baadhi ya matakwa yaliyobaki ni pamoja na ujenzi na upanuzi wa maktaba, kumbi za mihadhara na semina, ujenzi wa maabara pamoja na maabara ya kompyuta na kuongeza idadi ya Wahadhiri ili kutosheleza mahitaji ya Chuo Kikuu kamili. Aidha, Wahadhiri wa *MUCCOBS* wanahitajika kuongeza kasi ya utafiti na kuchapisha matokeo ya utafiti wao katika majarida ya Kimataifa na Utafiti.

(b) Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara cha Moshi kitakapofikia hadhi ya kuwa Chuo Kikuu kamili, Kituo cha Kizumbi kinaweza kuwa Kampasi ya Chuo Kikuu hicho.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru Serikali kwa hatua inazochukua kuelekea kukifanya Chuo Kikuu Kishiriki cha Moshi cha Ushirika kuwa Chuo Kikuu kamili. Hata hivyo nina maswali madogo mawili, lakini ni muhimu kweli kweli kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa *Campus* ya Kizumbi ndio kubwa kuliko *Campus* zote za Chuo Kikuu hiki Kishiriki. Moja kwa nini Serikali katika jibu lake la pili isiseme hivi Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara cha Moshi kitakapofikia hadhi ya Chuo Kikuu kamili kituo cha Kizumbi kitakuwa *Campus* ya Chuo Kikuu sio kinaweza, mashaka ya nini? *(Makofi/Kicheko)*

Je, Waziri au Naibu Waziri watakuwa tayari kuambatana na mimi kutembelea *Campus* hii kubwa ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Kizumbi ili wajionee na hatimaye kutoa fedha za ujenzi wa barabara ya lami kutoka barabara kuu kwenda kwenye *Campus* hiyo na kuona umuhimu wa kutumia kikamilifu hili eneo kubwa la Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, anauliza kwa nini nimetumia neno kuweza badala ya kusema kitakuwa. Inatakiwa kile chuo au Kituo cha Kizumbi kiwe na *facilities* ambazo zitakiwezesha kuwa *Campus*.

Kama itakuwa bado kitakapokuwa Chuo Kikuu *MUCCOBS* kimeshakuwa Chuo Kikuu kamili na kituo cha Kizumbi hakijapata hizo *facilities* haiwezekani kiwe *Campus*. Kwa hiyo, neno "kuweza" bado linaonyesha dhamira halisi ya Wizara kuhakikisha kwamba kituo kile kinaweza kikawa *Campus* kitakapokuwa kimetimiza masharti.

Suala la kwenda Kizumbi mimi ninaliafiki na namshukuru sana Mheshimiwa kwa kutualika lakini masuala mengine anayozungumza kuhusu ujenzi wa barabara ya lami mimi nafikiri haya anaweza kuwasiliana na Halmashauri husika kwa sababu sidhani kama ile barabara ni ya kujengwa na Wizara. Lakini matatizo mengine tutayao palepale tutakapofika kwenye kituo hicho.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri na hasa kukubali mwaliko wa kuelekea huko na ningeshauri uende wewe kwa niaba ya Waziri wako.

Na. 46

**Mikakati ya Kupambana na Ajali za Barabarani**

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR (MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mabara ya Afrika na Asia yanaongoza kwa vifo vinavyotokana na ajali za barabarani zinazoendelea kutokea mara kwa mara.

Kwa mujibu wa *'The Report on Road Traffic Injury Prevention'* inakadiriwa kuwa karibu watu 1,200,000/= hufa kila mwaka kutokana na ajali za barabarani na zaidi ya watu milioni 50 hujeruhiwa ambapo kwa Bara la Afrika na Asia kwa kila watu laki moja watu elfu ishirini na nane hufa kwa ajali za barabarani:-

(a)Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi, kati na mrefu wa kupambana na kupunguza ajali za barabarani?

(b)Je, Tanzania ni nchi ya ngapi katika Afrika Mashariki kwa idadi ya vifo na majeruhi yanayotokana na ajali za barabarani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kudhibiti ajali za barabarani, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za muda mfupi na muda wa kati kama ifuatavyo:-

·Kuendelea kusimamia ipasavyo Sheria na Kanuni za Usalama barabarani. Kurekebisha viwango vya adhabu zinazotolewa kisheria kwa wale wanaokiuka kama vile kutokuwa na leseni, magari hayakusajiliwa na kuendesha gari wakati wamelewa na kadhalika.

·Kuendelea kutoa elimu ya matumizi bora ya barabara kwa watumiaji.

·Serikali itaendelea kuhakikisha magari yanayoingizwa nchini yana ubora unaokubaliwa kulingana na Kanuni za *TBS.*

·Kurekebisha Sheria ili kuwa na ulazima wa kuyakagua magari yote *(Mandatory Vehicle Inspection*).

·Kuwawezesha askari wa kikosi cha usalama barabarani kuwa na vitendea kazi vya kisasa ili kuwadhibiti wanaokiuka sheria na Kanuni za Usalama Barabarani.

·Kila mwaka kuna wiki ya Usalama Barabarani Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya muda mrefu ni pamoja na:-

·Kuboresha miundombinu ya barabara.

·Kuimarisha barabara za pete (*ring roads*) hasa katika maeneo ya miji mikubwa kama Dar es Salaam.

·Kusimamia sheria ya uagizaji wa magari ikiwemo ya abiria ambapo magari yatakayoingizwa nchini na yale yenye umri usiozidi miaka mitano toka kutengenezwa kwake.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna utafiti rasmi uliofanywa na Serikali kubainisha ni nchi ipi inaongoza kwa ajali za barabarani katika Afrika Mashariki.

Hata hivyo kwa mujibu wa takwimu za ajali kwa kipindi cha Aprili, 2009 jumla ya ajali 1,597 zilitokea na watu 219 walifariki na mwezi Aprili, 2008 katika ajali 1,323 jumla ya watu 169 walipoteza maisha. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Siku zote tunasema kwamba kulinda ni bora zaidi kuliko kutibu na Mheshimiwa Naibu Waziri alipokua anajibu swali la msingi ameeleza sana adhabu zinazotolewa.

Lakini Bunge hili limekua likisisitiza siku zote kwamba moja kati ya sababu zinazosababisha ajali ni uchovu wa madereva pamoja na usingizi wakati wakiendesha. Wizara haichukui hatua na haijasema inamikakati gani kuweza kutekeleza ule wito wa Wabunge unaosema mabasi yanayoendeshwa na madereva wetu lazima yawe na madereva wawili ili kuondoa matatizo haya. Hili halikuzungumzwa. Mheshimiwa Naibu Waziri anasemaje kuhusu hatua hii?

Lakini la pili suala la ulevi na amesema anatoa adhabu kwa ulevi. Lakini siku hizi utaona askari wengi wanajificha vichakani wakiwa na tochi za kuangalia mwendo kasi. Lakini askati hao hao hawaoni kwamba sasa hivi umeshafika wakati hata wakati wa mchana kuwa na vipimo vya kupima ulevi pale wanaposimama na tochi zao kuona kama madereva hawalewi hata mchana ili kuzuia ajali?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa suala tulilokua nalo walikuwa wanauliza ni mikakati gani tuliokuwa nayo ya muda mfupi muda wa kati na muda mrefu na nadhani jibu langu la msingi linakamilisha hayo.

Lakini Sheria ipo bayana ya kusema kwamba kila mabasi yanayoakwenda mbali lazima yawe na madareva wawili na hiyo tumekua tunaifuatilia na yale mabasi ambayo yamekua yanakwenda kinyume na hapo hatuna jingine la kufanya isipokua adhabu na yule anayekiuka sheria ambayo imeweka basi kinachofuata ni adhabu na sisi tumekuwa tunafuatilia kuhakikisha kwamba hiyo sheria inafuata. Lakini kumekuwa na ukaidi kwa watu ambao wanamabasi haya wanaweka dereva mmoja na hiyo kwa kweli hatuna jinsi isipokua tunaifuatilia kwa adhabu.

Lakini la pili kuhusu ulevi kama nilivyojibu katika swali la msingi ni kwamba tunajaribu kuboresha vitendea kazi kwa askari wetu wanaosimamia hizi Sheria za barabarani. Ni kweli si nchi nzima kwamba askari watakuwa wana vipimo vya namna hii. Lakini kwa Dar es Salaam tunavyo vipimo na katika miji mingine tumeanza.

Kwa hiyo, jitihada zinafanyika kuona kwamba Jeshi la Polisi linapewa uwezo wa kufanya hivyo lakini hiyo tunaizingatia sana kwa sababu jambo la ulevi ni katika sababu kubwa ambazo zinasababisha ajali barabarani.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nina swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa umezuka mtindo wa baadhi ya askari barabarani kukusanya magari mengi mahali pamoja kwa nia hiyo hiyo ya kucheki. Lakini mtindo huo unaweza ukapelekea ajali.

Je, haoni kama wakati huu sasa ni muafaka wa kuwaasa askari wa barabarani wasifanye vitendo hivyo kwa sababu vinaweza vikapelekea ajali zisizokuwa za msingi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyoyatamka Mheshimiwa Khalifa ni sahihi na hii tumekwisha izungumza

tumewaeleza, lakini taabu inayojitokeza ni ule ufinyu wa barabara zetu. Lakini hilo tutazingatia na tutatizama ni taratibu gani zitafanywa na kwa kweli sehemu nyingine kwa mfano unaposafiri kutoka Dar es Salaam ziko sehemu unakuta magari ambayo yamesimamishwa kwa kweli hilo tutalizingatia.

Na. 47

**Tatizo la Ugonjwa wa Mafua ya Nguruwe**

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni kumetokea ugonjwa wa mafua ya nguruwe ulioanzia nchini Mexico na kuenea katika nchi za Marekani na nchi nyingine za Ulaya; na kwa kuwa Ulimwengu umekuwa kama kijiji kutokana na kukua kwa teknolojia watu wanasafiri kwenda nchini mbalimbali:-

(a) Je, Serikali imeweka mikakati gani ya tahadhari ya kuzuia ugonjwa huo usiingie nchini?

(b) Je, hadi sasa ni watu wangapi wameshafariki na ni kutoka nchi zipi?

(c) Je, ni ishara zipi au dalili gani za ugonjwa huo na wananchi wamepewa maelezo gani ya kuzingatia pindi wanapoziona dalili zimejitokeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** aliuliza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeandaa mkakati wa tahadhari na udhibiti wa ugonjwa huo kwa kushirikisha sekta mbalimbali chini ya Uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Maafa. Tayari maandalizi ya kutayarisha mkakati yameanza ambapo kikao cha awali cha wataalam kutoka Wizara husika kilifanyika tarehe 1 - 2 Juni, 2009. Kwa kuzingatia aina ya maafa mapambano dhidi ya ugonjwa huu yanaongozwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Wizara yangu na taasisi nyingine zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara yangu tumeimarisha udhibiti wa uingizaji wa nguruwe na mazao yake nchini na usafirishaji ndani ya nchi, tunaendelea kutoa elimu na kuzingatia usafi wa mabanda ya kufugia nguruwe pamoja na kufuatilia afya ya nguruwe kupitia Vituo vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo nchini. Aidha, wananchi wameanza kupata taarifa kupitia vyombo vya habari kuhusu ugonjwa huu na hatua za kuchukua ikiwa ni pamoja na usafi wa mabanda kuepuka kuchinja na kula nyama ya nguruwe wagonjwa. Kuzingatia kanuni za usafi wakati wa kutayarisha nyama, kupika nyama ya nguruwe mpaka iive na kufuata kanuni zote za usafi.

Mawasiliano na Mamlaka za Anga, Bandari na Vituo vya Mipakani yanaendelea ikiwa ni pamoja na kufuatilia taarifa za abiria wanaowasili nchini wenye kuonyesha dalili za mafua Makali. Aidha abiria wote wenye mafua wanashauriwa kuahirisha safari hadi watakapopata nafuu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na taarifa za Shirika la Afya Ulimwenguni *(WHO)* hadi kufikia tarehe 12 Juni, 2009 ugonjwa umeenea katika nchi 74 duniani ambapo kuna wagonjwa walioathibitishwa 29,669 na vifo 145.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, dalili za ugonjwa kwa nguruwe ni pamoja na kukohoa, kupiga chafya, pua kutoa makamasi, homa, kupumua kwa shida, kupungua kwa hamu ya kula chakula na wakati mwingine kupoteza mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dalili ni kama ifuatavyo, homa ya ghafla, kuumwa kichwa, maumivu ya viungo, maumivu ya misuli na uchovu, kukohoa, mafua, maumivu ya koo, kichefuchefu, kusikia baridi na mwili kutetemeka na kukosa hamu ya kula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamepewa maelezo yafuatayo ya kuzingaita wanapoona dalili zimejitokeza:-

·Kutoa taarifa kwenye kituo cha afya kilichoko karibu kwa uchunguzi na matibabu.

·Wagonjwa wenye dalili za mafua kutohudumia au kukaa karibu na mabanda ya nguruwe.

·Kuepuka kugusana na nguruwe iwapo wataonyesha dalili za ugonjwa.

·Kufunika pua kwa kitambaa au karatasi laini (*napkin*) wakati mtu anapokohoa au kupiga chafya.

·Kunawa mikono vizuri kwa sabani na maji mara kwa mara.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nina swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kuna baadhi ya Watanzania wanatabia ya kula vibudu yaani wanyama wafu wakiwemo ng’ombe, nguruwe au kitimoto au mbwa na wakati mwingine wanyama hao wanakua na maradhi kama ilivyo kwa homa ya Bonde la Ufa.

Je, Serikali haioni sasa kuwa ipo haja kuchukua hatua za kisheria dhidi ya watu hawa kwa sababu wanahatarisha uhai wao na kutoa maisha ni kosa la jinai?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa watu ambao wanafahamu kabisa si rahisi kula nyama ya mnyama mfu.

Lakini kama hii ikitokea basi ni bahati mbaya lakini Wizara yangu na vyombo vya habari kwa ujumla vimehamasisha watu wasile nyama ya wanyama wafu na sisi tutaendelea kuwashauri hivyo na ni vizuri tukawashauri badala ya kuwachukulia hatua maana wanapofanya hivi ni kwa sababu tunajua kielimu hawafahamu madhara yake. Lakini wananchi wengi wa Tanzania hawali mnyama aliyekufa bali aliyechinjwa.

Na. 48

**Mradi wa Kusambaza Mabomba Mererani**

**MHE. LEKULE M. LAIZER (K.n.y. MHE. DORA H. MUSHI** )aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeazimia kuwapatia wananchi wote maji safi na salama; na kwamba mji mdogo wa Mererani una kisima kilichosajiliwa na chenye uwezo wa kutoa maji kisi cha lita 68,000 kwa saa; na kwa kuwa mradi wa kusambaza mabomba katika mji huo bado haujatekelezwa:-

Je, Serikali haioni haja ya kuwanusuru wananchi hao kwa kutekeleza mradi wa kusambaza mabomba kwenye mji wa Mererani wenye wakazi 48,000.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dora Mushi, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa kuna kisima kirefu cha maji kilichoko Mererani chenye uwezo wa kutoa maji lita 58,000 kwa saa na siyo 68,000 kwa saa ambacho kilichimbwa kwa ufadhili wa *World Vision* Tanzania ambao walijenga pia tanki lenye ujazo wa lita 135,000/- wakanunua pampu ya nchi 6 yenye uwezo wa kusukuma maji lita 54,000 kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro katika mwaka wa fedha 2007/2008 ilitenga kiasi cha shilingi milioni 14 kwa ajili ya usambazi wa maji katika mji mdogo wa Mererani kupitia mpango wa *quickwins* wa Mradi wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira.

Aidha wananchi wa Mererani waliibua mradi wa kusambaza maji kupitia *TASAF* ambapo walipewa Dola za Marekani 30,000 ambazo zilisaidia kukamilisha kazi zilizoanza kufanywa kwa kutumia fedha za *quick wins.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mradi huu kukamilika ambapo ilikuwa ni pamoja na kuchimba kisima, kulaza bomba kuu, tanki la maji na kuweka pampu ya inchi

6 iligundulika kuwa umeme uliopo hautoshelezi kuendesha pampu ya maji. Hivyo basi Halmashauri ya Wilaya na kuwa juhudi kubwa za Mbunge wa Simanjiro Mheshimiwa Christopher Ole- Sendeka walipeleka maombi Wizara ya Nishati na Madini ilitoa hundi shilingi milioni 47 mwanzoni mwa mwezi Mei, 2009 kwa ajili ya kununulia *transfoma* na kuituma *TANESCO* Mkoa wa Arusha. *TANESCO* Arusha wanfanya maandalizi ya kuifunga *transfoma* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza na kuwashukuru Mheshimiwa Dora Mushi, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Sendeka, Mbunge wa Simanjiro kwa juhudi zao kubwa za kusaidiana na Serikali ili kuwapatia wananchi wa Mererani na Simanjiro kwa ujumla maji safi, salama na ya uhakika. Nawahakikishia wao na wananchi wa Mererani na Simanjiro Serikali itaendelea kutimiza wajibu kupitia Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji *(WSDP).*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, napenda kutoa pongezi kwa shirika la *World Vision* kwa kuwasaidia kwa niaba ya watu wa Simanjiro kuwasaidia wananchi wa kule kupata maji.

Kwa kuwa ukame umezidi sana katika maeneo ya wafugaji na kuna baadhi ya maeneo ambayo yanamalisho lakini hayana maji katika Wilaya ya Simanjiro na Wilaya ya Monduli ambayo mifugo imehamia kwa wingi sana. Je, Serikali inaweza kusaidia wananchi hawa kwa dharura kuchimba visima virefu vya kuwasaidia na kuokoa maisha ya mifugo pamoja na wafugaji hawa?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mheshimiwa Lekule Laizer, kwa kuishukuru *World Vision* na vilevile nachukua nafasi hii kuwashukuru *World Vision* kwa msaada wao wa hali na mali katika suala zima la kuwapatia wananchi maji safi na salama.

Kuhusu miradi ya dharura kwa maeneo ya ukame na maeneo ya wafugaji napenda kumhakikishia Mheshimiwa Lekule Laizer kwamba tuko tayari wakati wowote kushirikiana na Halmashauri katika maeneo ya ukame hasa maeneo ya ukame ili tuweze kwa pamoja tukaangalia kwa jinsi gani tunaweza tukawapatia maji wananchi pamoja na mifugo iwe kwa kuchimba visima au kwa kuwaongezea mabwana hasa kwa suala hili la Simanjiro na hasa tatizo kubwa la maji kwa Mji wa Olekesmet kwamba leo hii Maafisa wangu toka Wizara ya Maji wakiongozwa na Mkurugenzi wa Maji mijini wako hapo kuangalia tatizo hilo na kutafuta ufumbuzi wa dharura na Mheshimiwa Ole Sendeka yuko hapo kwa ajili ya shughuli hiyo. Tunategemea kupata mapendekezo yao ili tuweze kuona kwa udharara huo nini tuweze kufanya. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nilimwona Mheshimiwa Samuel Sitta swali la nyongeza. (*Kicheko*)

Naona Mheshimiwa Samuel Sitta ameridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri. Sasa nimwite Mheshimiwa Mgana Msindai.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi niulize swali moja la nyongeza. Nimeridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri lakini anasemaje juu ya ahadi ambayo yeye mwenyewe anakua anatoa kwa ajili ya vijiji vya Mameso, Matimila vilivyoko Peramiho na vijiji vya Matongo, Isene na Senene vilivyoko Iramba ya Mashariki. Ni lini watapata maji?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mgana Msindai naomba kwanza kumshukuru Mheshimiwa Samuel Sitta Mbunge wa Urambo Mashariki siwezi kusahau kwa sababu mimi natoka Rungwe Mashariki. Sasa kwa kuridhika na majibu ninayotoa hapa Bungeni. La pili kuhusu vijiji vilivyotajwa vya Peramiho na Iramba Mashariki napenda kumhakikishia Msindai kwamba iwapo haviko katika vile vijiji kumi basi naomba Halmashauri husika ziviweke katika Mpango wa maendeleo ya maji katika Wilaya hizo. Lakini kama vijiji hivyo vipo basi nina uhakika nitakapotoa taarifa ya maendeleo ya mradi wa vijiji kumi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia basi vijiji hivyo vitaonekana na mahala tulipo itafahamika ili tuweze tukawapatia maji wananchi wa vijiji hivyo.

Na. 49

**Mradi wa Maji wa Tove – Mwiramba**

**MHE. YONO S. KEVELA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mradi wa Tove – Mwiramba Wilaya ya Njombe ni mradi mkubwa wa maji unaofadhiliwa na Serikali ya Italy (Accra), Umoja wa Nchi za Ulaya na Serikali ya Tanzania:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Mradi kwenye vijiji vyenye tatizo kubwa la maji ikiwemo Kata ya Saja – Njombe?

(b) Je, Serikali imechangia nini kwenye Mradi huo mkubwa?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** atajibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Igomba, Saja, Ikulimambo, Uhenge na Itengeleo vilivyo katika Kata ya Saja, Wilaya ya Njombe, vinapata maji kupitia mradi mkubwa wa maji wa Wanging'ombe isipokuwa vijiji vitatu (3) vya Idenyimembe, Igenge na Isimike katika Kata ya Saja. Vimekuwa na matatizo ya maji kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa huduma ya maji kwa kila mwananchi Serikali inatekeleza programu ya Maendeleo ya sekta ya maji katika programu hiyo Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imechagua vijiji kumi vya kipaumbele

ambavyo vitatekeleza programu katika awamu ya kwanza. Vijiji vya Igenge na Isimike vilivyokatika Kata ya Saja viko katika progrmu hiyo.

Rasimu ya Mkataba wa usanifu wa vijiji 10 katika Halmashauri hiyo kati ya Halmashauri na Mtaalam Mshauri iko Benki ya Dunia kwa ajili ya ridhaa hiyo na itapatikana baada ya muda mfupi na kazi ya usanifu wa mradi kuanza. Ujenzi utaanza baada ya usanifu kukamilika na mkandarasi wa ujenzi kupatikana katika mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kijiji cha tatu cha Idenyimembe ambacho kipo katika mradi wa maji wa Wanging'ombe na ambacho kilikuwa hakipati maji toka mwaka 1989, ukarabati umefanyika kuanzia 2008 na kukamilika Machi 2009 kupitia fedha za miradi inayoleta matokeo ya haraka. Sasa kijiji kinapata maji.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ujenzi wa Mradi wa Tove – Mtwango unahusu vijiji 14 na unafadhiliwa na wahisani mbalimbali chini ya uongozi wa Kanisa Katoliki, Jimbo la Njombe inakadiriwa utagharimu shilingi bilioni 5.5 mpaka sasa zimetumika sasa zimetumika shilingi bilioni 4.2. Katika ujenzi wa Mradi wa Tove – Mtwango Serikali imechangia jumla shilingi milioni 406.5 na wananchi wamechangia nguvu kazi sawa na shilingi milioni 180.3.

Vilevile katika Bajeti ya mwaka 2009/2010 Halmashauri ya Njombe imetenga jumla ya milioni 31 kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa mradi. Halmashauri inashauriwa iupe mradi huo kipaumbele kwa kutenga fedha za kutosha kila mwaka hadi mradi utakapokamilika. Serikali ipo tayari kuchangia fedha hizo kupitia programu ya maendeleo ya sekta ya maji kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwashukuru wahusika wafautao katika mradi huu. Kanisa Katoliki Jimbo la Njombe, Shirika la lisilo la Kiserikali la *ACRA*, Umoja wa Ulaya, shirika la Uswiss, Mkoa wa Milano Italia, *Lenato Grand Faundation*, la Uswisi na Mensio Ujerumani , Mikoa ya Monza na Blanza ya Italia, Kikundi cha Mazingira kutoka Italia cha *Ecosystem* pamoja na Mheshimiwa Anne Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini, Mheshimiwa Stanley Kevele Mbunge wa Njombe Magharibi na Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini. Maji ni Uhai, Usafi wa Mazingira ni utu nakushukuru.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijauliza maswali mawili ya nyongeza ninaomba nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo alivyokuja kututembelea na kufungua huu mradi.

Kwa vile miradi mingi ya umwagiliaji ni gharama kubwa na mradi huu mkubwa wa Tove ni kwa ajili ya maji ya kunywa tu; na kwa kuwa umwagiliaji lengo lake kuu ni kuondoa umaskini wa kipato na vijiji husika kama vya Mwiramba, Usalule, Igagala,

Ulembwe, Nyumbanitu, Ulembwe, Mlevela, Igima Mhaji, Lusisi Mlazi na Mngate vimepitiwa huu na huu Mradi.

Je, Serikali ina mikakati gani ikiwa ni pamoja na kujenga mabwawa ya umwagiliaji ili makundi kama ya vijana na wanawake waweze kunufaika?

Swali la pili, kwa vile sasa hivi tuko kwenye kipindi cha Bajeti na madhehebu ya dini yanapiga kelele juu ya kutosamehewa kodi. *(Makofi)*

Je, Serikali inasemaje kuhusu vifaa vya maji na umeme kusamehewa kwa sababu mpaka sasa hivi huyu Father Kamiro na wafadhili wengine kama Mchungaji Paulo wa Korea wanaendelea kutozwa ushuru ambao ni kero kubwa sana. Je Serikali inasemaje kuhusu hilo.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuendeleza mradi wa Tove – Mtwango ili kuhusisha umwagiliaji kwa kuchimba mabwawa au vinginevyo nitashukuru kama Halmashauri ya Wilaya ya Njombe italiweka hilo katika mipango yake ya umwagiliaji na mipango yake ya maji halafu tuweze tukaangalia kitaifa kama itazidi uwezo wa Halmashauri tutakua tayari kusaidia.

Kuhusu vifaa vya maji kusamehewa kodi basi hili ni suala ambalo bila shaka Waziri wa Fedha atalitolea kauli anapomaliza majumuisho ya hoja ambayo inaendelea lakini naamin kwa sababu vifaa hivi vinatumika kwa ajili ya misaada kwa binadamu na kwa ajili ya maendeleo ya jamii, ninauhakika kabisa kwamba litaangaliwa kwa mtizamo huo na Wizara ya Fedha.

Na. 50

**Serikali Kuwasaidia Lishe Bora Waathirika wa UKIMWI**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imejitahidi kuhamasisha wananchi kwenda kupima *VVU* kwa hiari na pindi walioathirika wanapogundulika hupewa ushauri nasaha na kuanza kupewa dawa za kurefusha maisha *(ARVs);* na kwa kuwa dawa hizo ni kali sana na zinahitaji mgonjwa awe anakula chakula chenye virutubisho vya kutosha.

Lakini Watanzania walio wengi hawawezi hata kumudu mlo mmoja kwa siku kwa sababu ya hali duni ya maisha:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwasaidia vyakula vyenye virutubisho muhimu waathirika wasiokuwa na uwezo ili waweze kuishi kwa matumaini zaidi na kuendelea kulijenga Taifa lao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafanya juhudi kuwasaidia watu wanaoishi na *VVU* na wanaotumia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI kwa namna mbali mbali kama ifuatavyo:-

Serikali imekuwa ikianzisha Vituo vya Ushauri Nasaha *(VCT)* na vya matunzo na huduma *(CTC)* ambavyo hutoa ushauri kwa waathirika. Ushauri na elimu inayotolewa ni pamoja nay a chakula na lishe bora katika hali ya maambukizi ya *VVU* na katika matumizi ya dawa za kupunguza makali ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau mbali mbali hapa nchini wamekuwa wakiendesha programu za utoaji wa chakula na lishe kwa watu wanaoishi na *VVU*. Kwa mfano Shirika la Chakula Duniani *(WFP)* linaendesha programu za kugawa chakula kwa ajili ya kuwasaidia watu wanaoishi na *VVU*.

Chakula hiki hugawiwa kwa kaya nzima badala ya mtu mmoja au watu walioathirika pekee. Ugawaji huzingatia vigezo mbali mbali kama vile hali ya afya na lishe ya mwathirika na uwezo wa kaya wa kupata chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Clinton wa *VVU* na UKIMWI *(Clinton HIV and AIDS Initiative)* kwa kushirikiana na Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania, umekuwa ukigawa chakula dawa *(ready to use therapeutic food)* kwa ajili ya watoto wenye utapiamlo na wenye UKIMWI.

Mradi huu ulianzishwa kwenye Mikoa ya na Mtwara, lakini sasa umepanuka na kuhusisha Mikoa ya Dar es salaam, Morogoro, Iringa na Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *USAID* likishirikiana na Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania, sasa hivi liko kwenye mchakato wa kuanzisha programu ya utoaji chakula chenye virutubishi muhimu *(fortified blended food)* na chakula dawa *(ready to use therapeutic food)* kwenye Mikoa ya Dar es salaam, Mwanza, Shinyanga, Iringa na Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma hii itakuwa inapanuliwa kadiri siku zinavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua, matibabu ya *ARV* ni ya maisha, mwathirika akianza kutumia dawa hizi ni lazima aendelee na matibabu bila kukoma. Tunajua vile vile kwamba mgonjwa wa UKIMWI akianza kutumia *ARV* baada ya muda wa wiki chache mwili wake unarejea katika hali nzuri na nguvu zake zinamrudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, haileti maana kumfanya mtumiaji wa *ARV* awe tegemezi kwa chakula cha kupewa. Programu iliyobuniwa ni kuwaandaa walengwa pamoja na kaya zao kujenga uwezo wa kujitegemea kwa kuanzisha miradi midogo midogo ya kujikimu kama vile bustani, ufugaji na kadhalika.

Aidha, Wizara kwa kupitia Shirika lake la Chakula na Lishe imeandaa kijitabu kitakachoelekeza namna mwananchi yeyote anavyoweza kutengeneza chakula chenye virutubisho vya kutosha kwa kutumia vyakula vinavyopatikana hapa hapa nchini. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ni kwamba tukumbuke chakula chenye lishe ni sehemu ya matibabu. Katika majibu yake amesema Wizara inaandaa vijitabu vya kuelimisha watu jinsi ya kutumia chakula chenye lishe bora na chenye virutubisho.

Lakini dawa za *ARV* pamoja na vyakula vyenye lishe bora huwa vinatolewa na wafadhili. Sasa ningependa kujua, Je, Serikali ina mchango gani katika wale wasioweza kupata vyakula hivi maana vyakula hivi haviwafikii watu wote? Ningependa kujua Serikali ina mchango gani katika kusadia kwenye vyakula.

Pili; Je, nchi jirani zinawasaidiaje waathirika wanaotumia dawa za *ARV* pindi wanapohitaji chakula chenye virutubisho?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, ni kweli kabisa kwamba chakula ni sehemu ya matibabu. Mheshimiwa Mwenyekiti, na sasa hivi idadi ya wanaotumia dawa za kurefusha maisha, ni zaidi ya 240,000. Lakini vile vile wako wale wengine ambao hawatumii dawa ambao na wenyewe wana maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kweli kwamba wafadhili ndio wanaotoa, lakini mchango kama Serikali, sisi tunatoa dawa, lakini vile vile tunatoa elimu. Kwa sababu kama nilivyosema, mwathirika yeyote atakapoanza kutumia dawa, afya yake inakuwa ya kawaida. Kwa hiyo, anaweza akafanya kazi yake kama kawaida. *(Makofi)*

Lakini vile vile ninachosema ni kwamba hii elimu tunayoitoa ni kuweza kumsaidia, badala ya kupata zile dawa au vyakula ambavyo ni vya kutengenezwa, anaweza akatumia vyakula vinavyopatikana kwenye maeneo yake kama akachanganya mboga za majani na kadhalika ili aweze kula na kumsaidia.

Kwa hiyo, mimi bado nasema kwamba sisi kama Serikali tukishirikiana na wafadhili tutaendelea kuhakikisha kwamba tunatoa elimu ili wananchi waweze kujitengenezea vyakula kama kawaida, lakini wakati huo huo na dawa tunawapatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili la waathirika wa nchi za jirani, utaratibu wa nchi za jirani zinawasaidiaje walioathirika, ni nchi za jirani zenyewe zina mpango wake.

Lakini sisi kama nchi yetu tutatoa jibu kwamba sisi tutatoa dawa na chakula na bila shaka wale wenzetu katika nchi za jirani na wenyewe ni lazima kama watakuwa wanatoa dawa au wanawapa chakula, basi watakuwa na utaratibu wao wenyewe. Lakini sisi rai yetu ni kutoa dawa na kuwapa elimu na wananchi na kuwafundisha jinsi ya kujipatia dawa na chakula kama inavyopasa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, swali la mwisho, naomba tu mnisamehe, tule muda kidogo wa kuchangia, tumalize swali la mwisho.

Na. 51

**Huduma Zinazotolewa na Hospitali ya Mirembe**

**MHE. OMAR ALI MZEE** aliuliza:-

Kwa kuwa hospitali ya Mirembe hutoa matibabu kwa wagonjwa wa akili ambao idadi imekuwa ikiongezeka maradufu kutokana na hali ngumu ya maisha:-

(a) Je, ni aina gani ya magonjwa sugu yanayoongoza?

(b) Je, aina gani ya tiba zinazotolewa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mbunge wa Kiwani, naomba nitoe maelezo mafupi ya utangulizi kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mirembe ndiyo hospitali maalumu inayotoa huduma za tiba kwa wagonjwa wa akili. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita yaani 2004 - 2008 taarifa zinaonyesha kuwa idadi ya wagonjwa wanaolazwa katika hospitali hiyo ilikuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 6.

Aidha idadi ya wagonjwa wa nje *(Out Patients)* iliongezeka kwa asilimia 25. Hivyo, si kweli kwamba idadi ya wagonjwa imeongezeka maradufu kama inavyosomeka katika swali la Mheshimiwa Mbunge. Zipo sababu nyingi zinazosababisha magonjwa ya akili na baadhi yake ni kama vile:-

Matumizi ya pombe kupita kiasi, matumizi ya dawa za kulevya, kurithi na hali yoyote inayoweza kusababisha msongo wa mawazo ikiwa ni pamoja na ugumu wa maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifutavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, aina za magonjwa sugu ya akili yanayoongoza katika hospitali ya mirembe ni kama ifutavyo:-(i)Magonjwa yanayoshambulia fikra na hisia na kuathiri mwenendo wa tabia ya binadamu. Mara nyingi magonjwa haya ni ya kurithi ambayo ni: *Schizopherenia*, *Bispolar Disorder*, *Mania*, *Sonona (Major Depressive Disorder)* na Kifafa.

(ii)Magonjwa ya akili yanayosabishwa na matumizi ya dawa za kulevya na matumizi ya pombe kupita kiasi kama vile *alcoholism*, *cannabis psychosis* na *heroin dependence.*

(iii) Magonjwa ya akili yanayotokana na magonjwa mengine ya kimwili *(physical diseases)* au kwa jina lingine tunaita *organic psychosis.*

(iv) Magonjwa ya akili yanayosababishwa na mtindio wa ubongo yaani – *Severe Mental Retardatio.*

(b) Mheshimiwa spika, aina za tiba za magonjwa ya akili zinazotolewa katika hospitali ya Mirembe ni kama ifuatavyo:-

(i)Tiba ya aina ya vidonge na sindano *(psychopharmaco therapy).*

(ii) Tiba ya umeme *(Electro-convulsive therapy).*

(iii) Tiba ya unasihi *(psycho therapy).*

(iv) Tiba ya aina ya vitendo inayosaidia kujifunza upya na kupata ujuzi uliopotea baada ya kuugua akili yaani *(occupational therapy).*

(v)Tiba ya vitendo ya mafunzo ya ujuzi mbalimbali ili kuweza kumudu kimaisha baada ya kuathirika na ugonjwa wa akili *(Rehabilitation therapy*.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimwulize.

Je, jamii imeelimishwaje juu ya dhana nzima ya matibabu ya *ECT?*

Je, ni dozi ngapi anaweza kupewa mgonjwa wa *Schizopherenia* mpaka pale anapopona au kupata nafuu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, matibabu ya kutumia *Electro convulsive therapy(ECT)* sijui nitasema nimweleze nini wananchi wapewe elimu gani kwa sababu haya ni magonjwa ambayo mtu, mhusika mwenyewe atakapokwenda hospitalini, akionekana kwamba anahitaji yale matibabu, basi ataweza akaelezwa kuwa tunafanya nini.

Lakini kifupi ni kwamba hii ni tiba ambayo mgonjwa akifika pale hospitalini, anapata dozi ya umeme katika kichwa chake ambayo itamsaidia kama matibabu kwa jinsi ambavyo imetengenezwa. Kwa hiyo, kutoa elimu kwa wananchi kwa ujumla nadhani hii sijui kama itakuwa vipi, lakini nadhani mimi tutakita kwamba yule atakayehusika, basi tutampa yale maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kwamba dozi ni kiasi gani na anapata ngapi. Mimi nafikiri kwamba hili suala ni kwamba dozi itategemea umri, hali ya ugonjwa, mtu mwenyewe yuko namna gani. Lakini kwamba atapewa dozi ngapi, basi hiyo sasa ni utashi wa daktari atakapomwona, kwamba atapata moja, mbili, tatu. Lakini hii itategemea na jinsi mwenyewe yule mgonjwa atakapopata nafuu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita na kwa kweli tumeongeza dakika kadhaa ili tuweze kumaliza maswali yote ambayo yalikuwa kwenye *Order Paper* ya leo. Ninaomba kwa nafasi hii nimshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kushirikiana nasi leo kwenye shughuli zetu asubuhi akikalia kiti chake kama Mbunge. Mheshimiwa Spika, tunakushukuru sana na tunapata faraja unapojumuika na sisi kwenye kiti chako hapa ndani.

Ninayo matangazo machache hapa mbele yangu. Lakini Waheshimiwa Wabunge, nimepokea hapa viji-*note* kama sita wakinihoji kwa nini sijataka kutekeleza ile *speed* na *standard* ya Mheshimiwa Spika ya kuvaa joho aliyoitangaza.

Waheshimiwa Wabunge, sasa, ninaomba niseme kasi ile bado iko kwenye maandalizi na bahati mbaya leo nilipofika nilikuta joho lililoko tayari ni la Mheshimiwa Job Ndugai, nilipojaribu, kwa kweli ilikuwa ni shughuli nzito. Nafikiri mmeelewa vizuri hilo.

Kwa hiyo, ninaomba muwe wavumilivu na nadhani baada ya muda mfupi basi ile kasi *speed* na *standard* ya Mheshimiwa Spika itaonekana na tutakuwa kwenye mavazi rasmi. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, ninao wageni wacheche ambao wako hapa mbele. Ninaomba kwanza nitambue uwepo wa Mheshimiwa Balozi wa Sweden Nchini, Mheshimiwa Stephan Halstrom. Ameambatana na *Counselor for Political Affairs and Trade*, Mr. Andreas. *We are very much happy for your presence and we appreciate the way you visit our Parliament. Thank you very much. We wish good stay and we wish you a safe journey back to* Dar es salaam, *and let me say* Karibuni tena! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli leo kuna wageni wengine wa Mheshimiwa Felister Bura na hao ni wanafunzi 50 wa Chuo Kikuu cha Dodoma, wanachama wa Tawi la CCM Chuo Kikuu cha Dodoma.

Ninaomba wote wasimame. Ahsante sana. Na labda tu kwa faida, Mwenyekiti wa Tawi tungeomba pia usimame ili Waheshimiwa Wabunge waweze kukutambua. Karibuni sana. Naona imesimama Sekretarieti nzima ya Tawi la Chuo Kikuu la Chama cha Mapinduzi. Tunawakaribisheni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo pia tangazo la mgeni mwingine mmoja ambaye nimeambiwa hapa, ni Ndugu Faudhia Jabir Katundu – Mjasiriamali na Mwanamitindo ambaye ni mgeni wa Mheshimiwa Alshymaa John Kwegyr. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo ya kazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kwamba leo tarehe 16 kutakuwa na Kikao cha Kamati saa 7.00 mchana, Chumba Namba 231, ghorofa ya pili, jengo la utawala. Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hiyo, mnaombwa mhudhurie bila kukosa.

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, naye ameniomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo, saa 7.00 mchana katika Ukumbi Namba 219 jengo la utawala, kutakuwa na kikao cha Kamati. Ajenda ya kikao hicho ni kupitia na kuthibitisha maoni ya Kamati kuhusiana na masuala ya Bajeti. Wajumbe wote mnaombwa mhudhurie bila kukosa.

Ninalo tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, naye anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo tarehe 16 mwezi huu wa sita kutakua na kikao cha Kamati yake saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Tafadhali sana Wajumbe wa Kamati hiyo nao wanaombwa kuhudhuria kikao hicho.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani tumemaliza ajenda ya asubuhi, sasa nitamwita Katibu anipe mwongozo tuendelee na ajenda inayofuata. Katibu tuendelee na *Order Paper!*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010 na Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2008 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2009/2010

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaendelea na majadiliano na kwa faida ya wananchi wa Tanzania, tunaendelea na mjadala wa Bajeti na Hoja iliyo mbele yetu kwa sasa bado tunaendelea na Hoja ya Waziri wa Fedha na Uchumi na Waheshimiwa Wabunge wataendelea kujadili hotuba hiyo ya bajeti ya Waziri wa Fedha na Uchumi. Msemaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Fred Tungu na Mheshimiwa William Kusila ajiandae.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipatia nafasi niweze kuchangia Bajeti ya Serikali ambayo iko mbele yetu. Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake na watendaji wake wote kwa kuweza kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipongeze hotuba ya Kamati ya Fedha na Uchumi, ilikuwa nzuri sana. Mwisho nipongeze hotuba ya Kambi ya Upinzani Bungeni iliyowasilishwa na Kiongozi wa Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid, ambayo imeainisha vyanzo vingi sana vya mapato, ikiwa Serikali itazingatia, itaongeza pato la Taifa kwa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda moja kwa moja kwenye mchango wangu, ningependa kupata ufafanuzi wa suala dogo lifuatalo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu, Bunge ndio chombo au taasisi ambayo inaidhinisha Matumizi ya fedha zote za Serikali kwa Matumizi ya Kawada na za Matumizi ya Maendeleo. Lakini, nimekuwa najiuliza maswali kitu ambacho sijapata majibu bado. Mwaka 2007 baada ya Bunge kupitisha Bajeti hapa, Mheshimiwa Rais alitangaza kutoa shilingi bilioni moja kwa kila Mkoa kwa ajili ya kukopesha wajasiriamali, fedha ambazo ziliishia kwenye mifuko ya wachache na hazikufika kwa walengwa fedha hizi hazikuwepo kwenye Bajeti. Mwaka huu 2009 kwenye hotuba ya Rais, amesema kwamba Serikali itatoa bilioni 20 kwa ajili ya mikopo ya riba nafuu kwa kilimo kwa kununua zana za Kilimo kama matrekta. Hili halijaonyeshwa kwenye hotuba.

Pia Rais kasema kwamba, Serikali itatoa shilingi bilioni 20 kwa ajili ya Hifadhi ya Chakula cha Taifa, nayo haijaonyeshwa kwenye hotuba.

Sasa nashindwa kuelewa kwamba, Serikali ina mifuko miwili! Fedha tunayopitisha hapa Bungeni, halafu kuna mfuko mwingine ambao Bunge halifahamu mahali ulipo! Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningependa tupate ufafanuzi baadaye.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda moja kwa moja kwenye hotuba yangu; kwanza kabisa, naomba nizungumzie fedha za ruzuku zinazokwenda kwenye Halmashauri zetu. Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zetu zina Idara nyingi sana na kila Idara ina umuhimu wake na ina kazi zake. Lakini hizi fedha za *OC* zinapelekwa kwenye Idara tano tu ambazo ni Idara ya Kilimo, Elimu, Afya, Ujenzi na Maji. Idara

nyingine ziliobaki zikiwepo Maliasili, Mipango, Fedha, Maendeleo ya Jamii zinaambiwa zipate mapato kutokana na makusanyo ya Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara hizi ambazo ni muhimu kama Idara ya Maliasili ambayo yenyewe tu ina Sekta sita na Ardhi ikiwepo ndani, zinafanya kazi kwa mazingira magumu sana. Halmashauri kama hakuna hela, ina mana Idara hizi zinakaa mwaka mzima hazijafanya kazi yoyote. Matokeo yake, mwaka uliopita 2008 Serikali ilishauri kwamba zitengwe shilingi 200,000 kwa mwezi kwa hizi Idara ambazo hazipati *OC* kwa ajili ya kujiendesha.

Lakini fedha hizo kwa mwaka mzima hazikutolewa. Mwaka huu tena 2009, Serikali imeshauri zitoke shilingi 300,000 kwa ajili ya kuwezesha Idara hizi zifanye kazi. Nazo fedha hizi hazijatolewa. Sasa nashindwa kuelewa, Serikali inategmea sana Halmashauri kwa ufanisi wa kazi, Idara kama ya Maliasili ambayo ina Ardhi ndani yake, ina Misitu, Mazingira, Uvuvi, Nyuki, itajiendesha kwa namna gani? Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili Idara hizi ziweze kujiendesha kwa ufanisi, naomba sana Serikali ihakikishe inaziangalia Idara hizi. Na bahati mbaya kabisa basi, fedha za Halmashauri, inategemea na Mkurugenzi, kama Mkurugenzi ataamua aipe Idara anayotaka au asiipe. Basi, kama Mkuu wa Idara fulani hana maelewano mazuri na Mkurugenzi, anaweza ikakaa miaka miwili haijapata hata senti. Tunategemea nini kwenye Halmashauri zetu? Kwa hiyo, matokeo yake ndio matatizo kwamba viwanja kwenye Halmashauri haviwezi kupimwa kutokana na kwamba fedha hazitengwi, Serikali haitengi fedha na Halmashauri haitengi fedha. Kwa hiyo, hakuna ufanisi. Ninajua kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kuthamini kila Idara. Kwa hiyo, Serikali ihakikishe inatenga fedha na hasa kwa Idara muhimu kama Maliasili ambayo ina Sekta nyingi sana. Niende kwenye hoja nyingine. Bajeti ya mwaka huu imekuja na kauli mbiu ya Kilimo Kwanza. Mimi niliposikia kauli mbiu ni Kilimo Kwanza kuanzia kwenye uzinduzi kule Dar es salaam, nikajua sasa Serikali imeamua, imejizatiti kikamilifu. Kweli tutaanza sasa kuboresha kilimo chetu. Lakini nimekuja kuangalia kwenye Bajeti, nilitegemea angalau asilimie kumi ya Bajeti iende kwenye kilimo. Lakini bado tumeendelea kuiminya. Tunazungumza, maneno na matendo ni tofauti. Ndio maana sekta hii haipigi hatua. Tunachozungumza ni maneno kwamba tunaiboresha, lakini kimatendo tunaiwezesha kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Kilimo, tunapozungumza kilimo, tunazungumza kuanzia uzalishaji, usindikaji, usafirishaji na masoko ambayo ni uuzaji. Kwa hiyo, mambo haya yote manne ni muhimu kama hatutawekeza kikamilifu kwenye maeneo yote haya manne, hatuwezi kuboresha kilimo. Mimi naona kwamba Serikali inasema kweli tunaboresha kilimo, lakini ninavyoangalia kwamba Bajeti ni ndogo na bado tuna matatizo sana. Kwenye uzalishaji tuna matatizo, usafirishaji miundombinu ni mibovu, kwenye usindikaji viwanda hatuna, kwenye masoko nayo ni matatizo. Bado tutachukua muda mrefu sana kuboresha kilimo Tanzania. Serikali pamoja na kusema kwamba inaboresha kilimo, lakini yenyewe haiko tayari kuwekeza kwenye kilimo, inategemea wawekezaji, yenyewe inasema kwamba tutaweka mazingira mazuri, wawekezaji waje wawekeze kwenye kilimo.

Lakini tuangalie wawekezaji wengi hawataki kuwekeza kwenye kilimo kwa sababu kuna risk zake kwenye kilimo. Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, sasa hivi hatuwezi kutegemea mvua kwa kilimo Tanzania. Tukiangalia benki, hazitoi mikopo kwa kilimo, tukiangalia miundombinu ya umwagiliaji, bado ni dhaifu sana na hata midogo iliyopo haikidhi mahitaji. Atatakaye kuja kuwekeza kwenye kilimo tukiwa tunamsubiri itachukua karne nyingine kuboresha kilimo. Mimi ningefikiri kwamba kama Serikali imeamua kweli kuboresha kilimo, yenyewe iingine kuboresha kilimo, iwekeze kikamilifu kwenye kilimo, kwa namna hiyo tutakwenda. Lakini kwa kutegemea mwekezaji aje aweze kwenye kilimo, tuboreshe kilimo, itatuchukua karne moja nyingine kuhakikisha kwamba tunaleta mabadiliko kwenye kilimo. Suala lingine ni suala la kuhusiana na mipango inayoanzishwa na Serikali kwa ajili ya kuboresha kilimo ambayo siyo endelevu. Kwa mfano, kuna mpango wa *ASDP*, hii ni program ya miaka saba ambayo ilianzishwa mwaka 2006 mpaka 2013. Hadi sasa ni takriban miaka mitatu imepita, tulitakiwa tuwe tumetumia angalau bilioni 578.6 ambayo ni sawa na asilimia 21.4, lakini tumetumia shilingi bilioni 198 sawa na asilimia 7.3.

Sasa mimi nashindwa kuelewa, kabla hatujafanya tathmini, tujue mwendendo mzima wa programu hii kama imeleta manufaa kiasi gani, imeleta tija kwa wakulima, tumeachana nayo, tumeiweka pembeni, tunaanza programu nyingine. Kwa nini hatuna utaratibu wa kutathmini tuhakikishe kwamba mradi umeanza, umekamilika tumepata faida gani, kama umeleta manufaa tujue, kama haujaleta manufaa tujue ndio tuingine kwenye programu nyingine. Lakini kushika hiki, tunaancha, tunashika hiki tunaacha, hatuwezi kufika kwa mwendo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijidhatiti kwamba kama imeanzisha programu, ihakikishe kweli inapima kila baada ya muda fulani, tumetumia kiasi kadhaa, tumezalisha kiasi kadhaa, imeleta manufaa kiasi kadhaa. Kama haifai ndio tunaingia kwenye programu nyingine. Lakini mwendo tunaoenda nao, inatuchukua muda mrefu sana kuleta mabadiliko. Bajeti ya mwaka huu haijaonyesha popote unafuu wa nishati kwa matumizi ya nyumbani. Ili kunusuru mazingira yetu ambayo yanaendelea kuharibika. Asilimia 80 ya Watanzania sasa hivi wanatumia bado mkaa na kuni kwa maeneo ya mijini na vijijini. Umeme haushikiki na umeendelea kutokushikika kabisa, hakuna mwenye uwezo wa kupika kwa kutumia umeme. Tukiangalia vitu vingine kama mafuta ya taa hayashikiki, sasa hivi lita ni shilingi 800 mpaka shilingi 1000. Nishati nyingine bado ziko juu. *(Makofi)*

Bajeti ya Mwaka jana imetoa punguzo la ushuru kwenye mafuta ya Majiko Poa pamoja na kwenye gesi. Lakini ningetegemea angalau mwaka huu ituambie sasa kutokana na ushuru tuliopunguza kwenye Moto Poa, kiasi kadhaa wameacha mkaa, wameenda kutumia Moto Poa. Hakuna! Hakuna anayetumia MotoPoa mpaka sasa hivi. Kwa hiyo, ushuru uliotolewa kwenye Moto Poa haujatoa tija kwa Taifa, haujatoa tija kwa wananchi. Ni wachache wanaotumia. Wengi bado wameendelea kutumia mkaa. Kwa hiyo, Serikali lazima ibuni mikakati mingine madhubuti. Matumizi ya Mkaa yanaendelea kila siku. Hapa Bungeni nimewahi kuuliza swali, Serikali haijui kiasi cha mkaa kinachotumika, ni mwingi kweli, mkaa unaongezeka kila siku. Mwendo tunaoenda nao, tutakuwa tunaongeza jangwa. Serikali ibuni mbinu ya kuweza kuja na unafuu

kwenye nishati ya kutumia jikoni, vinginevyo, misitu yetu inateketea huku Watanzania tumetulia. Mwaka huu Serikali imeendelea kuongeza kodi kwenye bidhaa za sigara, tena imeongeza kweli kweli kipindi hiki. Na ninatambua kwamba kila mwaka Serikakali inanufaika kutokana na kuongeza kodi kwenye bidhaa kama pombe na sigara. Lakini kinachonishangaza, kwa nini kodi inaongezwa kwenye sigara, lakini bei ya zao la sigara ambayo ni tumbaku haipandi? Kila mwaka inabaki pale pale kwa nini? Kwa nini isiende sambamba na kupanda kwa bei ya zao la tumbaku. Mkulima wa tumbaku yeye anaendelea kuilimia Serikali ipandishe ushuru, tuendelee kupata fedha ambazo ni pato la Taifa, tunashukuru, lakini mkulima huyu ameendelea kuwa mtumwa wa kilimo hiki. *(Makofi)*

Nina wasi wasi sana kama hatutakuwa makini, ushuru tunaoongeza kwenye sigara utahamia kwenda kuwa mzigo kwa wananchi kwa sbabu makampuni ya tumbaku wanatumia kila shilingi kuinyonya kutoka kwa wananchi. Nina wasi wasi sana kwamba makampuni haya yataendelea kuongeza kodi ilioyoongezwa inaenda kwa mwananchi. Kwa hiyo anayepata machungu ni mwananchi na siyo huyu mfanyabiashara ambaye anatengeneza sigara. Kwa hiyo, ninaomba sana, sambamba na kuongeza ushuru kwenye sigara, Serikali ihakikishe pato la tumbaku linakuwa kubwa, ihakikishe kwamba bei ya tumbaku inapanda. Mpaka sasa hivi kilo ya tumbaku ni 2300/2500, lakini ona sigara hapa, ona sigara ilivyopanda. Naomba sana Serikali ilichukulie hili kwa makini kuhakikisha kwamba wakulima wa tumbaku nao wananufaika na zao lao kwa sababu wameendelea kuwa maskini, wameendelea kuwa ni watumwa wa makampuni huku Serikali imeendelea kuyalea na kuendelea kupandisha kodi bila kuwajali wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kilimo cha mkataba. Tumeendelea kweli kuanza kusisitiza kuwepo kwa kilimo cha mkataba. Lakini kilimo cha mkataba miaka yote hakijawahi kuwa na tija. Sijui Serikali imefanya tathmini gani? Wananchi wanawalimia wawekezaji, wanaendelea kuwa watumwa wa wawekezaji.

Ninaomba sana Serikali kabla ya kujidhatiti na kuingiza miguu yote kwenye kilimo cha mkataba, ifanye tathmini kuona kwamba mkulima ndiye anayenufaika au mwekezaji ndiye anayenufaika. Vinginevyo wakulima wetu wanaendelea kuwa maskini. Mfano halisi ni wa zao la tumbaku ambalo wakulima wameendelea kulima miaka nenda rudi, hawanufaiki huku wawekezaji wakiendelea kunufaika na Serikali bado inaendelea kuliangalia suala hili bila kuchukua hatua. Naomba sana liangaliwe kwa umakini ya wa hali ya juu ili wakulima waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumeongezwa kodi ya asilimia 10 kwenye mafuta ya kula. Hili mimi nalipinga kabisa. Ninalipinga kabisa kwa sababu maisha ya Mtanzania ni magumu. Tunavyoongeza kodi kwenye mafuta, ina maana hata yule aliyekuwa anaweza kutumia kijiko cha mafuta atashindwa kutumia kwa sababu mafuta ya kula yatapanda bei maradufu kutokana na ongezeko hili la ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi hapa nchini wakulima wetu wamekuwa wanajitahidi sana kulima alizeti. Kwa mfano Mkoa wa Singida sasa hivi yanazalishwa

mafuta mengi, maeneo mbali mbali, Dodoma inazalishwa alizeti, Tabora inazalishwa alizeti na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyopandisha kodi tujue kwamba soko la ndani linapata na matatizo. Kwa hiyo, tunaomba sana mzigo huu usiende kwa wakulima wetu, mzigo huu usiende kwa wananchi wetu, tuhakikishe kwamba tunawajali kwa kuwapunguzia makali ya maisha kwa kutokuongeza kodi kwenye mafuta ya kula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuongezewa Bajeti, nashukuru, huduma ya elimu imeongezewa Bajeti tunashukuru pamoja na maji. Lakini, inapoongezwa Bajeti hapa, tuione *impact* vijijini, tuone *impact* kwenye shule zetu ambako hakuna walimu wa kutosha, hakuna huduma, hakuna vifaa. Tuone kwamba kweli Bajeti imeongezeka kwenye elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti sasa hivi wanafunzi wanakaa chini kabisa. Serikali imejenga jengo bila kujali kwamba shule sio jengo, shule ni jengo na vifaa vyake. Kwa hiyo, wahakikishe kwamba shule ambazo hazina madawati zinapata madawati, hazina vifaa vya kusomea vinapata vifaa vya kusomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine kule Tabora Urambo. zipo shule ambapo wanafunzi wana walipa walimu. Wazazi wamekaa wamechoka shule haina walimu wakaamua kuajiri walimu wanne wao wenyewe, kwa hiyo wanafunzi wanachangishwa fedha kila mwezi wawalipe wale walimu hebu fikiria kwa miaka arobaini na nane ya uhuru. Mwanafunzi anamlipa mwalimu kweli hii ni haki! Sasa leo hapa tumeongeza bajeti tunaomba shule zote zipate walimu wa kutosha, zipate vifaa wanafunzi wanasoma katika hali ngumu ,wanafunzi kukaa chini hawawezi kusoma kwa ufanisi. Lazima tuboreshe mazingira ya wanafunzi wetu sambamba na kuboresha majengo ya shule ya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la Afya. Mkoa wa Tabora ni wa mwisho kwa kuwa na Madaktari wachache, na ni wa mwisho kuwa na wauguzi wachache. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali iangalie. Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Muda ahsante Mheshimiwa Magdalena Sakaya naona ulishika kasi kweli hapa. Sasa nawaomba Waheshimiwa Wabunge nimwite Mheshimiwa Fred Tungu Mpendazoe, halafu Mheshimiwa Wiliam Kusila, ajiandaye.

**MHE. FRED TUNGU MPENDAZOE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba hii. Kwanza kabisa niseme kwa dhati. Naipongeza Serikali kwa hatua ambayo imechukua, kuweza kunusuru wananchi kutokana na mtikisiko wa Uchumi Duniani. Hili kwa dhati kabisa naomba niipongeze Serikali. Na kwa dhati kabisa nimpongeze Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa kuweza kufikiria jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hatua zilizochukuliwa na Serikali naomba nitoe maoni yafuatayo. Na hasa kwa wakulima wa pamba. Kwanza nilikuwa nadhani Serikali inatakiwa kuchukua hatua kuwanusuru pia wakulima wa pamba ambao kwa mwaka jana walilima pamba kwa gharama ya shilingi laki tatu na kumi. *(Makofi)*

Lakini kwa bei ambayo itapatikana kutokana na Serikali kuwafidia wafanyabiashara au wanunuzi wa pamba bei inaweza ikawa shilingi mia tatu hamsini, kwa bei hiyo mkulima wa pamba hawezi kufidia gharama alizozitumia.

Kwa hiyo, ipo haja ya Serikali vilevile kuwafidia wakulima kutokana na mtikisiko wa kiuchumi Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti , la pili ipo haja ya Serikali kuchukua hatua ya kuongeza ruzuku za pembejeo. Na hasa madawa ya kilimo cha pamba kwa sababu kwa mwaka jana pamoja na kwamba mtikisiko haukuwepo, wakulima hawakuweza kununua madawa ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti katika madawa yaliyosambazwa mwaka jana asilimia arobaini na nane yalinunuliwa. Asilimia hamsini na mbili hayakuweza kununuliwa, pamoja na kutokuwepo mtikisiko wa uchumi Duniani. Sasa mtikisiko upo na bei ya mia tatu hamsini haiwezi kulipia gharama ya kulimia pamba kwa wakulima wa pamba, hawawezi kulima pamba vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo umuhimu wa Serikali kuongeza ruzuku kwa madawa ya kilimo ili wakulima wa pamba waweze kulima pamba mwaka kesho la sivyo dhana ya "KILIMO KWANZA" haina maana yoyote. Kwa sababu wakulima hawawezi kulima sasa "KILIMO KWANZA" maana yake ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili naomba nizungumzie pato la Taifa. Katika taarifa iliyotolewa, pato la Taifa ni Trilioni ishirini na nne *point* nane. Ni sawa na laki sita na ishirini na nane elfu na mia mbili hamsini na sita kwa mwaka kwa mtu. Ni sawa na shilingi elfu moja mia saba ishirini na moja kwa mtu kwa siku, ni sawa na dola moja *point* mbili kwa siku kwa mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maisha ya dola moja *point* mbili au shilingi elfu moja mia saba ishirini na moja kwa siku si maisha yaliyo bora kwa Mtanzania.

Lakini wakati wananchi wengi wanaishi maisha ya umaskini ya shilingi elfu moja mia saba ishirini na moja kwa siku kuna wananchi wachache, kuna Watanzania wachache wanao miliki Uchumi wa nchi hii na kusababisha umaskini mkubwa kwa Watanzania walio wengi waishio kwa shilingi elfu moja mia saba ishirini na moja kwa siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya Tanzania ni tajiri yenye watu maskini. Lakini umaskini huo wa Watanzania unatokana na maamuzi mengine mabovu ya Serikali au ya Viongozi wetu ambao tumewapa dhamana. *(makofi).*

Inatakiwa Serikali iwe makini zaidi katika maamuzi inayoyafanya ili pato la Tanzania liweze kuongezeka. Serikali ilitakiwa kuwa makini katika kubinafsisha reli yetu, ambapo katika Bajeti inaanza kutengewa fedha. Serikali ilitakiwa kuwa makini katika uuzaji wa nyumba za Serikali, Serikali ilitakiwa kuwa makini katika ununuzi wa rada, ndege ya Rais, *helcopter* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ashakhum* siyo matusi nirudie kusema mawe yaliyo chini ya bahari kamwe hayawezi kusikia kilio cha kiu ya mtende ulioko jangwani. Nimeomba *ashakhum* siyo matusi. Wakati wananchi wengine wanapiga vita ufisadi kuna watu wanao kejeli wakisema ufisadi ni agenda moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna wananchi wanaoishi kwa shilingi elfu moja mia saba ishirini na moja kwa siku. Wananchi wanataka majibu kwa maswali yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini wanaohusika na mikataba ya kwenye sekta ya madini na inajulikana imeingizia hasara Serikali yetu hawajachuliwa hatua? Kwa nini watendaji wa Serikali waliohusika na sakata la *RICHMOND* wanaendelea na kazi zao na tunatenga Bajeti kwa ajili yao! Serikali inachukua hatua gani kuhusu waliohusika na ubinafsishaji wa reli yetu na mgodi wa Kiwira wakati kuna Watanzania wanaishi kwa shilingi elfu moja mia saba ishirini na moja kwa siku. Wananchi wanataka majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutochukua hatua dhidi ya uovu ni kubariki uovu. Na ninakubaliana na msemo wa kisambaa unaosema “ukitaka kuepuka inzi tupa kibudu au tupa mzoga” Serikali inapokuwa haichukui hatua dhidi ya ufisadi na mafisadi ina bariki uovu. Na haitaweza kuepuka kulaumiwa na Watanzania. Itaendelea kuwa na harufu ya ufisadi na yenyewe. Ipo haja ya kuchukua hatua mapema iwezekanavyo, Dhidi ya ufisadi na mafisadi ili pato la Mtanzania liweze kuongezeka. Nizungumzie uhuru wa kutoa maoni na demokrasia. Ibara ya tisa kifungu cha kinasema kwamba, nchi itatawaliwa kwa kufuata misingi ya kidemokrasia na Ujamaa. Na ibara ya kumi na nane kifungu cha kwanza kinazungumzia uhuru wa kutoa maoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti penye uhuru ni pale watu wanaweza kutoa maoni yao. Lakini penye demokrasia ni pale Serikali ina sikiliza maoni ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanasikitika kwa Serikali kutaka kuwazuia Wananchi kujadiliana masuala yanayowakera kutoka kwenye Serikali yao walioichagua. Ibara ya nane kifungu cha kwanza A mpaka C cha Katiba kinasema Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na Serikali inapata madaraka na mamlaka toka kwa wananchi hivyo Serikali ina wajibu wa kuwasikiliza wananchi maoni yao juu ya Serikali yao walioichagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itakosolewa na wananchi walioichagua. Wananchi wanao wajibu wa kuikemea Serikali kama inakwenda vinginevyo, kwa sababu wameichagua wao. Serikali haikuchaguliwa na malaika toka mbinguni, haikuchaguliwa

na Miungu. Kwa hiyo, wanaoweza kuisema Serikali kwamba iende vizuri ni Wananchi walioichagua Serikali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie *issue* ya *DECI.* Mimi naomba kusema kwa dhati Serikali imefanya vizuri sana kwa hatua ambayo imechukua kuhusu mambo ya *DECI, absolutely* naunga mkono. Lakini kwa upande mwingine naomba kusema wananchi kwa kukata tamaa uwezeshaji haujawa mzuri, fedha zilizotolewa za JK hazikuwafikia wananchi wa kawaida. Mikopo wananchi wa kawaida hawawezi kukopa kwenye mabenki unategemea wafanye nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watachukua mbadala wowote ule. Kwa hiyo, pamoja na hatua ambazo zinachukuliwa na Serikali ni nzuri. Lakini inatakiwa kuwawezesha zaidi wananchi kuweka unafuu wa Wananchi waweze kukopa, kwenye *SACCOS* wananchi hawawezi kuingia kwa sababu hawana mtaji. Mbadala wao ni *DECI!* Si kizuri lakini wananchi ndicho walicho nacho mbele yao. Serikali ina wajibu wa kuwawezesha zaidi wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine naomba kuzungumza kuikumbusha Serikali kuhusu ahadi ilizo waahidi Wananchi wa jimbo la Kishapu. Kwa nyakati tofauti mwaka jana, Serikali iliahidi kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara kutoka Kolandoto mpaka Meatu kupitia Mhunze kwa kiwango cha lami.

Iliahidi kujenga barabara ya Mwigumbi mpaka Maswa kwa kiwango cha lami, kwa nyakati tofauti iliahidi kutoa fedha kwa ajili ya umeme katika Makao Mkuu ya Kishapu, Kwa nyakati tofauti iliahidi kuongezea fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ambayo imekamlika kilometa ishirini na nne tu, kutoka Bunambiu mpaka Mhunze kupitia Ngundangali.

Mheshimiwa Mwenyekiti,wananchi wanashauku kuona utekelezaji wa ahadi hizo mwaka huu. Kwa sababu mwaka jana Serikali ilituambia tuvute subira, tumevuta vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kama nitapata nafasi kumalizia nizungumzie suala la ajira. Katika taarifa ya hotuba imeeleza asilimia kumi na moja ya Watanzania hawana ajira, asilimia saba vijijini hawana ajira, asilimia thethini na nne Jijini Dar es salaam hawana ajira. Lakini cha kusikitisha ukiwa Dar es salaam utakuta Wachina wanafanya biashara ambazo zingefanywa na Watanzania, utakuta Wakorea wanafanya vitu ambavyo vingefanywa na Watanzania .

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusitisha kwenye mahoteli mengi sasa hivi utakuta ni Wananchi kutoka Kenya , Uganda na nchi zingine ndiyo wanaofanya kazi, lakini Watanzania hawana ajira. Ninaiomba Serikali kwa makusudi iweke utaratibu, utakaowalinda Watanzania hawa ambao ajira zao sasa zinaenda mikononi mwa wageni. Tufanye kwa makusudi Serikali inaweza kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili Wachina, Wakorea wanaofanya biashara za ajabu ajabu katika Jiji laDar es salaam wanaingiaje kwenye nchi yetu! Hivi wenzetu hamuwaoni ambao mna wajibu wa kufuatilia na kujua kweli hawa watu wa Korea, Wachina wanafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ambazo zingetakiwa kufanywa na Watanzania wenzetu zinafanywa na wageni. Hilo nilikuwa naomba Serikali ilizingatie na ichukue hatua za makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina muda kidogo labda nizungumzie usimamizi wa fedha za Serikali. Katika *report* ya Mkaguzi wa fedha mwaka jana imeonyesha bilioni tatu nukta tano zilitolewa bila hati za malipo. Bilioni moja nukta nne zilitolewa kwa utaratibu ambao si mzuri ina maana *almost* bilioni tano zimetumika katika mazingira ya ufisadi. Aidha Serikali ina peleka fedha nyingi sana kwenye Halmashauri kwa sasa. Kama hatutadhibiti ufisadi katika ngazi ya Wilaya naamini mipango yote ya Serikali inayokwenda kwenye Wilaya zetu haitatekelezwa. Lakini kibaya zaidi kuna bilioni mia moja na saba zilizopelekwa na Serikali Kuu na wahisani hazijatumika Wilayani. Kwa sababu ya uhamasishaji hafifu. Lakini Mwalimu Nyerere alisema kifuatacho ambacho ni muhimu kuhusu uhamasishaji, alisema hivi; “Viongozi wetu katika ngazi ya Wilaya wana uwezo mkubwa sana wa kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye maandamano ya kuwapokea viongozi wa kitaifa, wanauwezo mkubwa sana wa kuhamasisha wananchi kuhudhuria mikutano ya wageni wa kitaifa lakini wamepungukiwa sana na sifa na uwezo wa kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye miradi yao ya maendeleo”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu akienda ziara anapokelewa na umati mkubwa sana, Rais akienda anapokelewa na umati mkubwa sana.Waambie watu waende kwenye mikutano ya kuibua miradi hawapo. Lakini tatizo ni uwezo wa viongozi ngazi ya Wilaya kuhamasisha watu washiriki mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hayati Nyerere aliliona hilo akaona viongozi ngazi ya Wilaya wana uwezo sana wa kuhamaisha maandamano. Kushiriki mikutano ya wageni wa kitaifa wapeleke katika sifa ya kuhamasisha wananchi waweze kuibua miradi, na waweze kusimamia miradi yao. Viongozi hawa hawana alisema Mwalimu Nyerere na tatizo hilo bado lipo na ni kubwa sana kwa sasa ndio maana bilioni mia moja na saba, zilizotolewa na Serikali Kuu na zilizotolewa na wafadhili, hazikutumika wakati wananchi wana kero za maji, huduma mbovu za afya, barabara mbovu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya Serikali kuangalia watendaji wetu wa ngazi ya Wilaya wana uwezo wa kuhamasisha wananchi kushiriki Mipango ya Maendeleo yao. Nitaunga mkono Hoja hii baada ya Serikali kujibu Hoja zangu. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukurusana Mheshimiwa Fred Tungu Mpendazoe. Waheshimiwa Wabunge naomba sasa nimwite Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Elisa Mollel, ajiandaye na kwa mujibu wa kuendesha shughuli za Bunge

kwa kuzingatia jinsia nitampa nafasi Mheshimiwa Florence Kyendesya baada ya Mheshimiwa Elisa Mollel. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2009/2010.

Mhemishiwa Mwenyekiti, nitaanza mchango wangu kwanza kabisa kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hotuba yake aliyoitoa kupitia Wazee wa Mkoa wa Dodoma na Wabunge wa Bunge hili Tukufu kuhusiana na mtikisiko wa Uchumi au wa kifedha Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika hotuba hiyo ambayo ilikuwa na maelezo ya kina sana. Ilitusaidia kupata uelewa mzuri, kuhusiana na tatizo hili kubwa la dunia na vilevile ilitujengea ujasiri wote kwa pamoja, ili tuweze kukabiliana na tatizo hili kiume kama alivyosema yeye mwenyewe, namshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa fedha na Uchumi Manaibu wake, na watendaji na wataalamu wote katika Wizara ya Fedha na Uchumi kwa Hotuba hii nzuri ya Bajeti, ambayo kwa kiwango kikubwa sana imejielekeza katika kukabiliana na tatizo tulilonalo hivi sasa la mtikisiko wa kifedha na uchumi duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza mchango wangu kwanza kwa kujielekeza kwa masuala ya nyumbani. Na la kwanza kabisa nataka kuchangia kuhusiana na suala la kilimo cha zabibu katika Mkoa wa Dodoma. Na niharakishe tu kutamka kwamba mimi mwenyewe ni mkulima wa zabibu kama kanuni zetu zinavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze sana Serikali kwa uamuzi wa kupandisha ushuru wa bidhaa za mvinyo. Ambao unatengenezwa kwa zabibu kutoka nchi za nje kwa kiwango kinachozidi asilimia ishirini na tano, kutoka shilingi elfu moja na hamsini na tatu kwenda elfu moja mia moja thelathini na moja .

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi huu ni uamuzi mzuri sana na wenye manufaa kwa wakulima wa zabibu katika Mkoa wetu wa Dodoma.

Lengo lake ni kulinda viwanda vyetu vya mvinyo lakini, wakati huo huo kulinda bei ambayo mkulima wa zabibu ataipata kutoka kwenye viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mtikisiko wa kifedha duniani nchi zinazolima zabibu kwa wingi duniani kama vile Italia, Afrika ya Kusini na Ufaransa zimejikuta zina mvinyo mwingi ambao hauna soko. Bei ya mvinyo katika nchi hizo umeteremka sana. Taarifa niliyo nayo karibu nchi zote hizo mvinyo sasa unauzwa kwa bei ya chini sana. Italia unauza kwa chini ya senti arobaini ya *Euro* kwa *glass* ya *wine* mtu anapoitaka kutoka kwenye *counter* ambayo ni kiwango kinachofanana na shilingi mia saba za kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukilinganisha na bei ya sasa ambayo ni kati ya shilingi elfu moja mia tano mpaka elfu mbili katika soko, na katika nchi yetu hivi kwa sasa. Afrika ya Kusini hivyohivyo mvinyo unauzwa kwa chini ya dola moja katika soko. Kwa hiyo maana yake ni kwamba kama tusipokuwa waangalifu mvinyo huu wote utatafuta soko katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo taarifa ya kuaminika .Kwamba kampuni moja ya Afrika ya Kusini ilikusudia kununua moja ya kiwanda chetu kikubwa cha mvinyo hivi sasa katika Mkoa wa Dodoma na kinachotengeneza mvinyo wa kimataifa sio kwa lengo la kukiendeleza, lakini kwa lengo la kukiua. Ilikuwa kikishanunuliwa kifungwe na kisiweze kuzalisha tena mvinyo ili waweze kupata nafasi kuuza mvinyo kutoka katika nchi yao ya Afrika Kusini lakini walikataliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa kutouziwa ulikuwa ni mzuri sana. Mkoa wa Dodoma tegemeo letu kubwa kwa mazao ya biashara ya kudumu na ya manufaa ya kutuondolea umaskini ni pamoja na zao hili la zabibu. Kwa hiyo, Serikali tunaiomba iendelee kulilinda zao hili ili lisife tena. Huko nyuma zao hili lilikufa kwasababu tulikosa soko. Naomba tusiliachie tena likafa kwa sababu ya soko kutawaliwa na mvinyo kutoka nchi zingine. Kwa hiyo, uamuzi huu ni mzuri lakini naomba tuangalie kama kweli hiki kiwango ambacho kimepandishwa kinatosheleza kuufanya mvinyo unaotengenezwa na viwanda vyetu humu nchini uweze kushindana na huu mvinyo kutoka nchi za nje ambao bei yake imeshuka sana kutokana na mtikisiko wa kifedha duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti ,jambo jingine ambalo nilitaka nichangie kwa kifupi ni suala la umwagiliaji. Sote tunakubaliana kwamba ili kilimo chetu kiweze kushamiri na hasa katika hali hii ya ukame ambao unaongezeka siku hadi siku kutokana na kupanda kwa joto duniani na uharibifu wa mazingira, suala la umwagiliaji lazima lipewe umuhimu ambao linastahili hasahasa katika sehemu zile zenye ukame kama Mkoa wa huu wa Dodoma. Sasa hivi tumekuwa tunazungumza muda mrefu. Lakini mimi bado napata wasiwasi kama kweli katika kupanga vipaumbele vyetu tunaelekeza rasilimali kule ambako zinastahili. Tunazungumzia mara nyingi sana kiwango kinachotengwa katika kilimo lakini mara nyingi hatuendi na kuangalia kama hizo rasilimali hata kama ni kidogo ni kiasi gani zinaelekezwa katika maeneo yanayo stahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri tukubaliane kwamba katika maeneo ya ukame kama Mkoa huu wa Dodoma, suala la kilimo cha umwagiliaji lazima lipewe kipaumbele namba moja kwa suala la kilimo. Mikoa mingine yenye ukame kama Shinyanga suala hili liwe na umuhimu wa kipekee halafu Mikoa mingine nayo tutazame masuala mengine ambayo yatafanya kilimo kiweze kushamiri kama kinavyotakiwa kama vile masuala ya mbolea na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwetu hapa suala la mbolea siyo la muhimu kama vile Mikoa mingine. Kwasababu bahati nzuri sana sisi Mkoa wetu, udongo wetu una madini mengi yanayotakiwa kwa mimea na suala la matumizi ya mbolea si muhimu sana

kwetu. Sasa sisi tuchimbiwe mabwawa, tuchimbiwe malambo ili tuweze kufanikiwa katika suala la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana *Tanzania Menonite* kwa kuonyesha njia nyingine mbadala ambayo kwa kweli inaweza kuwa ni ya manufaa sana katika suala hili la kilimo cha umwagiliaji. Nalo ni suala la makinga maji, katika Mkoa wa Dodoma na sehemu nyingi zenye ukame tuna hayo makorongo, mito hii ya muda ambayo tunaita makorongo ambayo huwa inapitisha maji mengi sana wakati wa masika na kiangazi inakauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mito hii mingi ina maeneo mengi mazuri kwa ajili ya kujenga makinga maji. Na ni mradi rahisi sana unakinga tu yale maji, unauziba ule mto ili maji yale yanapotiririka katika mto huo yanazuiwa mahali. Yanazuiwa kwa kiasi fulani na si ajabu kufikia *level* ile mengine yanaruhusiwa kuendelea, kwa hiyo, kwa mto mmoja unaweza kufanya makinga maji hata matano, sita, saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama yake sio kubwa sana. Wameshatujengea makinga maji mawili katika mto mmoja wapo karibu sana na mji huu wa Dodoma inagharimu kama tu milioni thelathini na tatu kwa kinga maji moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kiasi amabcho Serikali yetu inaweza kumudu na ikajenga makinga maji mengi , katika maeneo mengi ya Mkoa huu wa Dodoma, kwasababu ya mito ambayo inafaa kwa miradi kama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, manufaa ya makinga maji haya kwanza kabisa ni kutunza maji, kwa matumizi ya binadamu na mifugo. Lakini vilevile yanajenga ukanda fulani mkubwa tu ambao unakuwa na unyevu wa kudumu kutokana na yale maji kuendelea kunyonywa kwenye ardhi. Kwa hiyo unakuta yanajenga eneo labda la umbali wa mita kama mia tatu, mia nne ambayo inakuwa na unyevu wa kudumu. Hivyo kuruhusu kilimo cha mwaka mzima katika eneo lile iwe ni ya mboga au mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile inasaidia sana kurekebisha mazingira. Inasaidia kujenga uoto wa asili katika eneo hilo ambalo linakuwa ni la unyevu wa kudumu na kurekebisha sana mazingira. Sasa nasema hii ni miradi mizuri. Gharama yake siyo kubwa sana na tungeweza kunufaika sana kwa kujenga makinga maji katika maeneo mengi, katika Mkoa huu wa Dodoma, na katika Mikoa mingine ya ukame ambayo nayo ina makorongo kama haya ya Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali iangalie uwezekano wa kuchukua mradi huu ambao wenzetu wa *Menonite.* Kanisa la *menonite* wameanzisha ili tuweze kuendeleza katika maeneo mengi ya Mkoa huu wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kwanza! na mimi nakubaliana sana na suala hili mradi tunakubaliana kwamba kilimo kwanza. Na katika mazingira haya tuliyonayo ya hivi sasa ya msukosuko wa uchumi duniani tunakubaliana wote kitakachotuokoa katika

hali hii ni pamoja na kilimo. Kuzalisha kwa wingi mazao ya chakula na mazao ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tujielekeze katika kinazingatiwa na kuhakikisha kwamba tunafungua kilimo cha mashamba makubwa. Watusaidie wale wanaoweza kuanzisha mashamba makubwa na kuzalisha mazao kwa wingi. Watu binafsi lakini hasa hasa mimi ningependa sana kuishawishi Serikali kwamba tutumie majeshi yetu ya Magereza na JKT vizuri katika suala hili. Tuwape nyenzo, fedha, ili wafungue mashamba makubwa na kuzalisha mazao kwa mahitaji ya nchi na hata kuuza nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao uzoefu wa Magereza kwa kazi nzuri ambayo wameweza kuifanya katika eneo hili. Tunajua mashamba mengi ambayo yanamilikiwa na Magereza jinsi yalivyofanikiwa. Katika hali hii, hili ni eneo moja, hawa ni watu ambao tunaweza kuwatumia wakaweza kuzalisha chakula kingi na mazao mengi kwa ajili ya biashara. Tunayo nguvu kazi ya bure pale, badala ya kila mara kufanya bajeti ya kulisha wafungwa tukiwapa fedha wanaweza kuzalisha chakula cha kutosheleza mahitaji ya wafungwa pamoja na kuisaidia nchi katika suala la chakula na hata kuuza nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, JKT hivyo hivyo, tunaweza kulitumia ili kutusaidia katika kuzalisha chakula hapa nchini na hata kuuza mazao mengine nchi za nje. Kwa hiyo, tunapozungumzia kilimo kwanza, pamoja na kuhakikisha kwamba, tunawasaidia wakulima wetu wadogo wadogo, lakini tuelekeze fedha na nyenzo kwa watu ambao wanaweza kufungua mashamba makubwa na kuzalisha chakula kingi ambacho kinaweza kutusaidia katika hali hii na kuondoka na tatizo hili haraka inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika haya yote, suala la miundombinu ni muhimu na umuhimu wake wote tunauelewa, ni lazima nchi yetu tuifungue kila kona iweze kufikika kiurahisi. Kwa hiyo, suala la *trunk roads* na barabara zingine za mikoa katika maeneo yote ya nchi yetu, ni muhimu sana. Kwa misingi hiyo, naomba sana suala la kuangalia barabara kati ya Arusha na Iringa, ambayo imebakia sasa ndiyo tatizo kubwa kati ya Kusini na Kaskazini mwa nchi yetu, lipewe umuhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni barabara kuu na ni barabara kubwa Afrika ambayo inaunganisha Afrika Kaskazini na Kusinina mahali peke yake ambapo pamebakia tatizo ni hapa kwetu, tukiunganisha Arusha na Iringa tutaiunganisha Afrika yote Kusini na Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri inayoifanya ya kuunganisha Kaskazini mwa nchi yetu na Magharibi mwa nchi yetu. Naomba suala hili la barabara ya kutoka Babati, Iringa kujengwa kwa kiwango cha lami litiliwe maanani ili tuweze kuiunganisha nchi yetu na usafiri wa kutoka kusini hadi kaskazini, uweze kurahisika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hii ya misukosuko mikubwa ya fedha Duniani, suala la kuzalisha bidhaa zetu wenyewe kwa mahitaji yetu nchini na hata kuuza

nchi za nje,  lina umuhimu wa kipekee. Kwa hiyo, jukumu la wajasiriamali katika nchi yetu ni kubwa na ni zito, linastahili kupewa umuhimu. Wajasiriamali wa Tanzania wanajitahidi sana kuzalisha bidhaa mbalimbali za kilimo na nyingine za viwandani, lakini kuna tatizo ambalo ninaliona, ni la shirika la viwango ambalo ni lazima lipewe umuhimu

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Nakushukuru sana Mheshimiwa William Kusila, kwa mchango wako. Tunaendelea na mchangiaji anayefuata, ni Mheshimiwa Elisa Mollel, atafuatia Mheshimiwa Kyendesya na Mheshimiwa Khadija  ajiandae.

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii uliyonipa asubuhi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake aliyotupa juzi kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Dodoma kuhusu mtikisiko wa uchumi wa dunia na vyombo vya fedha duniani. Hotuba hiyo imetupa mwelekeo wa bajeti hii ya mwaka 2009/2010. Aidha, niipongeze Serikali kwa maandalizi mazuri ya bajeti hii ya mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa idhini yako, naomba nianze na kero za Serikali ambazo hazitekelezeki hususani kwenye Jimbo langu la Arumeru Magharibi. Kero hizi zimekuwa za muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwanza kabisa, nianze na kero ya huduma za afya. Katika mwaka wa 2008, Serikali imeingia ubia na kukubali Hospitali ya Seleiani ambayo ni ya KKKT, Dayosisi Mkoani Arusha kuwa Hospitali Teule ya Arumeru Magharibi. Mkataba huo umesainiwa kati ya Serikali na Dayosisi Disemba, tarehe tano 2008. Hospitali hii inahudumia watu 350,000 wa Jimbo la Arumeru Magharibi, ina uwezo wa kupokea mpaka wagonjwa mia moja kwa siku na ina uwezo wa kulaza wangonjwa mpaka 140 kwa siku, ina wafanyakazi 206, mishahara ya wafanyakazi ni shilingi milioni 82 kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kusema, licha ya mkataba uliopo kati ya Serikali na Dayosisi Mkoani Arusha, wafanyakazi hawa wameendelea kufanya kazi ya kuhudumia katika hospitali hii kwa miezi saba sasa bila ruzuku ya mshahara kutoka Serikalini ambayo ni kiasi cha shilingi milioni 560.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inasikitisha sana kwa sababu Serikali licha ya ahadi yake ya kuhusisha sekta binafsi katika huduma za jamii kama ilivyofanya hapa na licha ya kuwepo mkataba wa kuonesha majukumu ya Serikali na majukumu ya Dayosisi kwa upande mwingine, bado Serikali haijaweza kuheshimu mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti nina barua ambayo hospitali imeandikiwa na Serikali kutoka Hazina hawasemi chochote juu ya mkataba ambayo ina malimbikizo ya milioni

560 mpaka leo wala hawasemi juu ya jinsi gani watalipa, wamesema nashauri utekelezaji wa maamuzi haya yaanze mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa lakini hii ni ahadi tu, je, malimbikizo ya miezi saba yatapatikana katika mwaka huu wa fedha na je, Serikali itaanza kuheshimu mkataba huu kati yake na Dayosisi Mkoani Arusha? Nitaomba wakati Waziri wa Fedha aki-*wind up* anieleze hili tatizo litatatuliwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi na viongozi wa Dayosisi na viongozi wa Hospitali hii ya Saleiani, tumezunguka kwenye Wizara ya Manejimenti ya Utumishi wa Umma na Wizara ya Afya, Hazina mara nyingi sana na hakuna jibu ambalo tumepewa, kila mmoja anapiga mpira. Sasa kama Serikali imeshaingia kwenye mkataba, kwa nini hizi ofisi za Serikali zinazohusika zinatupiana mpira? Hii ni kero nzito sana na ninaomba nipewe uamuzi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero nyingine inatokana na huduma ya maji. Serikali imeahidi kwamba itasaidia kupunguza tatizo la maji katika Jimbo langu la Arumeru Magharibi. Hii ni ahadi ya Serikali tangu wakati ule wa uchaguzi na kila wakati Serikali imekuwa inaahidi. Hivi karibuni kumechimbwa visima karibu vitatu vya kupeleka maji Monduli, vimechimbwa katika Jimbo langu la Arumeru Magharibi kwenye Mji wa Ngaramtoni. Visima hivi vimemalizika, vina maji, visima viwili vimewekewa miundombinu ya bomba ya kupeleka maji Monduli na mabomba haya yanapita kwenye Jimbo langu la Arumeru Magharibi, linapita kwenye vijiji vinne ndiyo ifikie Monduli. Kilichofanyika hapa, mabomba yametandikwa kwenye vile visima kwenda Monduli vijiji vinne ambavyo ni Vijiji vya Olmoturumeti, Likamba, Leitushula na Nengumu mpaka Monduli. Kile kisima cha Jimbo la Arumeru Magharibi kimeachwa pale hakina miundombinu ya bomba. Ubaguzi huu kwa wananchi wa nchi mmoja wa Mkoa mmoja unatokeaje? Naomba Serikali ijibu. Mimi sina ugomvi na watu wa Monduli kupata maji, ugomvi wangu ni kwamba kwa nini ubaguzi huu unakuwepo katika kugawa huduma za jamii katika Majimbo yanayopakana? Serikali itupe bomba tusambaze maji katika vijiji hivi vinne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero nyingine inatokana na maji ambayo wananchi wa Arumeru walikuwa wanapata kutoka mlima wa Monduli kwenda kwenye Kijiji kinachoitwa Oljorovusi. Mgogoro huu una miaka zaidi ya kumi na tano sasa kila wakati Serikali inasema tutaangalia na mara ya mwisho mwaka 2006 Wizara iliamua kwamba itatoa fedha za kujenga vyanzo na vidaka maji na kusaidia maji yaende kwenye kijiji cha Oljorovusi, mpaka leo haya hayajafanyika. Nikienda Wizarani, wanasema tumewaambia Mkoa lakini Wizara iliahidi kwamba itatoa fedha. Kwa kero hii ya maji, naomba Serikali iwape majibu wananchi wa Arumeru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero ya tatu ambayo ni nzito pia kwa sababu inahusu huduma za jamii na maendeleo ya kiuchumi katika Jimbo langu, ni mzozo uliopo kati ya wananchi wa kata tatu za Mlangarini, Moshono na Nduruma na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Kumekuwa na mgogoro wa ardhi ambapo Jeshi wanasema ardhi ni yao na wanavijiji wanasema ardhi ni yao kwa miaka mia tumekuwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda Wizara ya Ulinzi, wanasema tunalishughulikia, nikienda pengine wanasema tunalishughulikia, ni vizuri Serikali iwe wazi, wananchi ni wa Serikali hii na Jeshi ni la nchi hii na ni la wananchi sasa kwa nini tupigwe mpira hivi. Sasa hivi JWTZ, wameweka mabango ya simenti yanayosomeka "usifike hapa, usiendeleze ardhi kwa shughuli yoyote" ujenzi wa shule umekwama, ujenzi wa zahanati umekwama na kadhalika. Tunaomba Serikali itoe uamuzi lakini hatutaki kusikia tena tunaambiwa usipite hapa na Serikali haisemi chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia ahadi ya Serikali kuhusu nishati ya umeme katika jimbo langu la uchaguzi. Tangu mwaka wa 1996 na nimeiandikia Serikali na ninayo barua hapa, tuliahidiwa Arumeru kupata umeme na kila mwaka na kila wakati naikumbusha Serikali juu ya ahadi hii, hakuna la maana lililofanyika. Naomba sasa umeme katika vijiji vya Likamba, Oljoro, Mirongo, Sambasha na Oldonyosambu sasa kwenye bajeti hii niambiwe inakuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba sasa niingie kwenye bajeti hii hasa kuhusu msamaha wa kodi kwenye mashirika ya dini. Mimi sikubaliani kabisa na kuondoa msamaha wa kodi kwenye madhehebu ya dini hasa katika huduma za afya, elimu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapa, kazi nzuri inayofanywa na KKKT Dayosisi ya Mkoa wa Arusha katika Hospitali Teule, sikubaliani kabisa na Serikali,i nashauri misamaha hii iendelee hasa katika huduma za elimu, afya, maji, kilimo na mifugo kwa yale madhehebu yote ambayo yanatoa huduma hii. Kama kuna upungufu, Serikali uutazame, kama kuna uhalifu huo uhalifu Serikali uutazame na tusahihishe yale matangazo yetu ambayo yanatoa msamaha kwa mashirika haya ya dini. Zaidi kama ni vigumu kwa Serikali kuita hii ni misamaha, basi iite ruzuku, tuondokane na neno la msamaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Serikali kuondoa msamaha katika ushuru wa mafuta ya *petrol*, lakini *petrol* wanayotumia hawa wanaochimba madini, ni kidogo sana tuweke na *diesel* na tuweke na kampuni zote zilipe kodi tusiondoe ushuru huo na kampuni ziwe zile za zamani na za sasa ambazo zinaingia mkataba na Serikali zilipe kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie juu ya Ushuru wa Forodha ulioondolewa kwenye mitumba. Serikali imeteremsha kodi ya mitumba kutoka asilimia 45 mpaka asilimia 35. Nafikiri punguzo hili ni dogo sana. Nguo za mitumba ndiyo nguo zinategemewa na watu wengi huko vijijini na hata mijini na nguo hizi zinawasaidia watu wasio na ajira na pia wale wasio na uwezo. Kodi ya Forodha ielekezwe kwenye haya maduka na wafanyabiashara wanaoleta nguo mpya ambao watu wenye uwezo wanaweza kununua. Tuwasaidie wakulima, vijana na akina mama ambao hawana uwezo. Ninashauri ushuru huu kwa nguo hizi za mitumba ungeteremshwa mpaka asilimia ishirini ili

kuwasaidia wale wananchi ambao hawana uwezo katika kupambana na mtikisiko huu wa kiuchumi katika dunia nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 38, Mheshimiwa Waziri ametaja mashirika ambayo yanatakiwa kuimarishwa ili kuongeza ufanisi, mashirika hayo ni *TTCL, TRL*, TAZARA na *ATCL*. Ninapenda kuuliza Tanzania *Ports Authority*, tunafanya nini, *TANESCO* tunafanya nini, *DAWASCO* tunafana nini, Tanzania *Postal Bank* ambayo jana Mheshimiwa Lupembe ameizungumzia vizuri, tunafanya nini, Tanzania *Fertilizer Company* na *STAMICO*, tunafanya nini, mashirika haya yote yapo hoi yanatakiwa yaimarishwe na Serikali ili tija kwa Serikali kutokana na haya mashirika iongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naomba nikushukuru na ninaomba niseme kwamba nitaunga mkono hoja hii ya bajeti endapo Serikali itanipa majibu ya kutosha. *(Makofi)*

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Waziri wa Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kuipongeza bajeti hii nzuri ambayo inaleta matumaini kwa Watanzania endapo itatekelezwa kama ilivyopangwa. Vilevile nampongeza Waziri wa Fedha na Uchumi pamoja na watendaji wake wote kwa kutuletea bajeti iliyo wazi na nzuri, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo machache tu ya kuweza kuongelea hapa, kwanza napenda kuongelea kuhusu kuondolewa kwa misamaha ya kodi kwa madhehebu ya dini. Kwanza kabisa, nayapongeza sana haya mashirika ya dini kwa kazi nzuri wanayoifanya hususani ujenzi wa vyuo vikuu na shule za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa sekondari na vyuo vikuu vinavyoendeshwa na mashirika ya dini, kwa kweli wameipunguzia sana mzigo Serikali, mathalani pale ambapo Serikali ingehitaji kujenga vyuo vikuu saba inaweza ikajenga vyuo vitatu, fedha zingine zikatumika kwenye maendeleo mengine au kwenye miradi mingine kama vile miundombinu na afya, kwa kweli nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina kigugumizi kidogo kwamba kwa sasa haya mashirika ya dini yanapata misamaha ya kodi, lakini mbona misamaha hii haimsaidii mwanafunzi au mzazi kutokana na gharama kubwa ya ada inayotozwa kwenye vyuo hivyo na sekondari kuliko zile za Serikali kwa nini? Hapa ndipo sielewi kidogo ndiyo maana nasema napata kigugumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuone mifano halisi michache, Chuo Kikuu Tumaini Iringa kwa mwaka mmoja kinatoza ada shilingi milioni mbili na laki nane kwa masomo ya Sheria, Chuo Kikuu cha St. Johns hapa Dodoma kwa mwaka ni milioni moja na laki

nane na sitini na kwa mwaka huu 2009 wanaongeza tena mimi sielewi ni kiasi gani. Chuo Kikuu cha St. Agustine cha Mwanza kwa mwaka mmoja ni milioni mmoja na laki nane hado milioni mbili kwa mwaka. Nichukue shule za sekondari chache tu, St. Marian ya Bagamoyo, O-*Level* ni milioni moja na laki mbili kwa mwaka na milioni moja na laki nne kwa *A-Level.* Sasa ukiangalia Vyuo vya Serikali, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Dodoma ni laki saba hadi milioni mmoja na laki nne kwa mwaka, shule za sekondari za Serikali haifiki hata laki mmoja sote hapa tunajua na tuna watoto wetu wanasoma huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimesema mimi napata kidogo kigugumizi, lakini kazi wanayoifanya ni nzuri lakini hiyo misamaha kwa mwanafunzi na mzazi ananufaika nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mashirika ya dini yanafanya kazi nzuri sana, mimi kwa kweli nayapongeza sana tena kwa maendeleo ya Watanzania na tunayaona kwa macho, Mashirika ya Dini yana vitega uchumi vizuri sana, tuchukue hapa Dodoma St. Gaspar, nani hajaona St. Gaspar hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli ile hoteli ya St. Gaspar kweli isitozwe kodi! Inashindana na Dodoma Hotel, ukiacha Dodoma Hotel kwa hapa Dodoma mimi naiona St. Gaspar, kwa kweli ni hoteli nzuri sana, ina *bar*, ina *restaurant*, ina kumbi za mikutano, naomba tuangalie pande mbili za shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tuangalie kwa makini sana, kwa sasa hivi kumekuwepo na mifumuko mingi sana ya uanzishwaji wa makanisa, kuna Mikoa mingine utakuta kuna makanisa zaidi ya mia tatu.

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, wananiambia ungetoa mfano kama Mkoa gani, ama Mbeya ama wapi? (*Makofi*)

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano baadaye kwa kuwa bado naendelea kuchangia, viongozi wa makanisa hayo wamekuwa wakihama kutoka kanisa moja kwenda kanisa lingine, wakati neno la Mungu halihitaji kuhamahama, Wakristo tunasema ng’ang’ania msalaba hata kama kuna matatizo, lakini kuna kuhamahama kwa viongozi wa makanisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa baadhi yao ndiyo hao wanaojinufaisha binafsi, wapo viongozi wengi wa Makanisa, ni wazuri sana na ni safi sana tunawafahamu, taifa linawafahamu na sisi wote tunawafahamu, wale wachache wanaojinufaisha binafsi ndiyo wanaponza wenzao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa inabidi Serikali iwadhibiti wale ambao wanaanzisha mambo yao kwa kujinufaisha, wanapewa misamaha ya kodi lakini wanaitumia vibaya na hao ndiyo wadhibitiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo mifano lakini hapa siyo mahali muafaka kutaja hawa ambao wananufaika binafsi na tunafahamu mambo mengine yako wazi lakini kwa kuwa hapa si mahali muafaka, nisingependa nianze kuyataja hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie kwenye sekta ya kilimo, mipango mizuri tumeelezwa hapa na tumesoma kwenye vitabu, mimi naipongeza sana Serikali kwa kuweka sekta ya kilimo kuwa kipaumbele, ningeomba kuwepo na ufuatiliaji ili kwamba ile mpango iliyowekwa itekelezwe. Ufuatiliaji uwe kwa watendaji Wizara na taasisi zake, vinginevyo mipango mizuri iliyowekwa na Serikali tutakuja kuona kwamba hakuna kitu ambacho kimetekelezwa kwa sababu nia nzuri ya Serikali ni kumnufaisha mwananchi wa kawaida au mlengwa. Kwa hiyo, ninaomba sana kuwepo na ufuatiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kuipongeza Serikali kuhusu kuwaona na kuwatambua wastaafu kwa kuongeza *pension* kwa wastaafu, naomba kuonyesha *interest* zangu kwamba na mimi ni mstaafu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili mimi naipongeza sana Serikali lakini katika bajeti hii haijaoneshwa kwamba ni kiwango gani labda tusubiri kwenye Idara inayohusika ya Utumishi. Kwa hiyo, kuipongeza sana hapa nashindwa kwa sababu sijui ni kiwango gani kimeongezwa kwa kima cha chini cha pensheni. Kima cha chini sasa hivi ni shilingi 20,000, sijui ni kiwango gani kimeongezwa isije ikawa imeongezwa shilingi elfu moja halafu hapa tukaambiwa kwamba pensheni imeongezwa, isije ikaongezwa shilingi elfu tano halafu tukaambiwa kiwango cha chini cha cha pensheni kimeongezwa, mimi sitaunga mkono hoja kwenye Wizara inayohusika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wazee wetu hawa wastaafu ndiyo wameifikisha nchi hii hapa tulipo, wale ambao wanapata shilingi 20,000 kwa mwezi ndiyo wameifikisha nchi hii hapa tulipo, bila wale sijui tungekuwa wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waziri anayehusika ama Serikali iliangalie sana kama waliongeza kidogo mimi sitaunga mkono bajeti hiyo, ninaomba waangalie kabla ya kutuletea hapa, angalau kima cha chini kiwe elfu hamsini kwa mwezi. Hawa wazee wetu ukiwaona leo, wengi wao walikuwa wanalelewa na watoto wao baada ya kustaafu, hawa watoto Mungu amewachukua na wameachiwa vijukuu, badala ya kuwapeleka kwenye vituo vya yatima wanawalea wao hao wazee, wanawalipia ada za Sekondari na wengine wapo Vyuo Vikuu. Kwa hiyo, shilingi elfu ishirini wale wa zamani, angalau hawa waliostaafu baada ya mwaka 1996, hao nafasi zao kidogo ni nzuri lakini waliostaafu kabla ya 1996, kwa kweli hali zao ni duni sana. Ninaiomba Serikali iangalie kwa makini wanapotuletea hapa bajeti ya Wizara hiyo tujue ni kiasi gani na wasitufumbe kwamba kwa mwezi wanapata kiasi hiki isije ikawa wameongeza shilingi elfu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kyendesya hasa wakati unamalizia hoja hii ya wazee, umekuwa ukiongea kama Mchungaji kabisa, kwa hiyo, nakupongeza sana, umeonyesha uzalendo na Mzee wa Kanisa, Mheshimiwa Lubeleje, amesikia, nimemwona alikuwa akitikisa kichwa kukubali.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na msemaji anayefuata ni Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy atafuatiwa na Mheshimiwa Shibuda.

**MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia nikaweza kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu na kuweza kuchangia hoja hii ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, naomba ku-*declare interest*, mimi ni mfanyabiashara. Kwanza, naomba kuchangia hoja ya *TICTS* ikiambatana na Bandari pamoja na *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni masikitiko yangu makubwa sana kwamba Waziri Mkuu anapozungumzia kitu, anakuwa tayari ameshakiona na ndani ya Bunge hili, alisema *TICTS* ni mtendaji mbovu na hafai lakini nashangaa mpaka leo bado hatujalitolea ufafanuzi suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakaa Zanzibar na mara nyingi natumia vyombo vya bahari; ukifika karibu na Bandari ya Dar es Salaam, unakuta kila siku hazipungui meli 10 au 12 ziko katika Bandari na zaidi sisi tunahusika, tunaleta mizigo. Mizigo inatoka nje, inachukua wiki tatu katika Bandari ya Dar es Salaam kwa sababu siku hizi kuna mtandao unaona mzigo wako mpaka unapofikia. Kwa hiyo, unakaa pale Bandarini si chini ya siku 21 mpaka mwezi mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipo katika Kamati ya Miundombinu na tunajua *TICTS* hawana vifaa vya kutosha. Kwa sababu kama wana vifaa vya kutosha, kwa mujibu wa maelezo yao, basi wasingekodi vifaa vya Bandari! Vilevile walitoa ahadi kama wataongeza kina katika Bandari, lakini mpaka leo wanakaribia kumaliza ile miaka kumi ya mwanzo, hakuna jambo lolote lililofanyika. Pia walipewa habari kwamba, kama mizigo inakusanyika, basi waende katika *yard* ya Ubungo lakini bado msongamano unabakia kuwa mkubwa kwa sababu utendaji wao hauridhishi, kutokana na kutokuwa na vifaa vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, iangalie nchi yoyote inaendelea kwa kukusanya mapato ya kodi. Wenzetu hawana Bandari, sisi tuna Bandari nyingi sana hapa Tanzania, ikiwemo ya Mtwara, Zanzibar, Tanga na kwingine ambapo kuna Bandari lakini hazitumiki, haswa ukiangalia Bandari ya Mtwara, ambayo ilikuwa na vipingamizi vingi sana kutoka kwa *TRA*, lakini nashukuru nimesikia sasa hivi imeruhusiwa ifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, iwe na maneno mafupi, vitendo viwe virefu kwa sababu wanasema sana maneno ambayo utekelezaji wake unakuwa si mzuri

na baadaye kizuri au kibaya, wenzetu wa jirani, huchukua mipango yetu na wakaitekeleza wao. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie sana jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TRA*. *TRA*, ina kitengo kinaitwa *Long Room* na ni *Long Room* kweli maana yake bora warekebishe sasa hivi maana kutokana na utandawazi uliokuwepo, waiite *Short Room*. *Long Room* hiyo, kila siku inaundiwa mitandao mipya. Mara utasikia kuna *TISCAN*, mara kuna *ASYCUDA++*, mara kuna *SISCAN* lakini ufanisi wake hatuuoni. Kwa hiyo, naomba, kwa sababu kwanza hatuna umeme wa uhakika, unapokuwepo umeme katika *Long Room*, basi bandarini hakuna, ukiwepo umeme Bandarini, katika maofisi mengine hakuna; kwa hiyo, kazi zetu ambazo zinafanyika pale zinazorota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna mtandao ambao unaitwa *SISCAN*, ambao una *load documents* zako lakini bado unapokwenda pale, kitu kimo katika mtandao, lakini unaambiwa hakionekani, hayo ni maajabu sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie kwa kina watendji wake kwa sababu hao ndio wanazorotesha nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia wafanyabiashara wa Zanzibar, wanaoleta magari yao hapa, wanakuwa tayari wamekwishalipa na huu mtandao umekwishaunganishwa mpaka Zanzibar, lakini cha kusikitisha ni kwamba lazima wahakikishe kwamba wanalipa *storage* na wanalipa *difference* ambayo kule wanakuwa wameshalipa kikamilifu wakati *TRA* ni moja na mtandao tayari tumeshafunga. Haya ni mambo ya kusikitisha sana, nchi ni moja lakini manyanyaso ndio kama hayo wanayofanyiwa wafanyabiashara wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninapenda kuuliza *TRA* wao wana ujuzi, wamefanya kazi siku nyingi, wanajua Watanzania wanaleta nguo, wanaleta magari, wanaleta viatu na mambo mengine, sasa tunachokiuliza inakuwaje wakawa hawajui bei, kila siku lazima waulize? Kwanza unaambiwa *document* zako zipo *TISCAN*, zinapelekwa huko nje sijui Singapore kwenda kuhakikishwa bei. Kwa nini sisi tunafanya kazi kwa kutokujiamini wakati vitu ndio hivyo hivyo, hakuna kipya kinachobadilika. Kwa hiyo, naiomba Serikali, iondoshe urasimu kwa sababu mapato ya kwanza yanapatikana kutokana na Bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda naweza kusema kwamba wanawakandamiza watu ili wahakikishe wanakusanya mapato ambayo yanapita kikomo, kwa sababu wao wanalipwa *5%*, ikiwa wamepitisha yale mapato. Kwa hiyo, hii 5% naona ndio inasababisha watu wanalipa bei kali ambayo haipo katika dunia hii lakini hapa Tanzania ipo. Naomba jambo hili Serikali iliangalie kwa kina kabisa, vinginevyo nchi hii kila siku tutakuw tunarudi nyuma, tunasema nchi ni maskini wakati nchi hii sio maskini, ni tajiri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Hong Kong, ni kisiwa kidogo tu, lakini kinaendeshwa na Bandari. Nashangaa Tanzania, ina Bandari nane, ambazo ni kubwa, nzuri, kama Mtwara ina kina kirefu cha maji, naomba tena meli zikashuke kule, lakini

bado ni mlolongo wa maneno kila siku, hakuna vitendo. Kwa hiyo, naiomba Serikali iache maneno mengi ifanye vitendo ili kuinusuru nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye *ATCL. ATCL* inabeba nembo ya Taifa. Nchi hii, wenzetu waliokuwa hawana imani wameiingiza katika hasara kubwa wameingia mikataba utafikiri wao hawaishi katika nchi hii. Imefika mpaka sasa hivi *ATCL* imefilisika kabisa, japo Mheshimiwa Rais ana nia njema kabisa ya kulinusuru shirika hili, lakini bado ni mzigo wa Serikali na Serikali, haijawa *serious* katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ATCL* ina ndege mbili tu, ina wafanyakazi 364, hiki ni kichekesho jamani, 364 kwa ndege mbili, kwa kweli tutaweza kufika mahali sisi, kila siku tunasema kwamba nchi hii tunataka iendelee, nchi ambayo, shirika linalobeba nembo yetu ya Taifa, kulitangaza Taifa letu, leo tumefika hapa tulipofika. Haina *route* ya kutoka Dar es Salaam - Zanzibar, haina *route* ambayo ingeweza kwenda Muscat *direct*, haina *route* ya aina yoyote ambayo inaweza ikafanya biashara. Kwa hiyo, naiomba Serikali ihakikishe inaitoa nchi hii katika umaskini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni mkataba wa *TRL*. *TRL* ina mkataba mbovu sana, Serikali ina asilimia 49 na wenzetu upande wa pili wana asilimia 51. Huyu mtu aliyeiingiza Serikali katika mkataba huu mbovu, kwa kuhakikisha kwamba Serikali haina *management* kuanzia mtu wa kwanza mpaka wa kumi na nane ni mhindi tu, hivyo kweli Serikali tunaitakia mema? Kweli watu ambao sio Watanzania, watawaonea huruma Watanzania? Naomba suala hili, hiyo *management*, pamoja na mtaji, basi tuhakikishe Serikali inatoa, ili tuhakikishe nchi hii inapata mapato. Ukitembea kuanzia Dar es Salaam mpaka Kigoma, unakuta miundombinu ya reli sio mizuri, majengo mabaya, yanaweza yakahatarisha hata maisha ya watu. Jengo lenyewe ukiingia unaweza ukaogopa jinsi lilivyo na ufa, sasa kweli kama ingekuwa mtu ambaye yuko pale ni Mtanzania, kweli asingeweza kuwaonea huruma watu wa Kigoma akawafikiria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa ni kuhusu simu za mikononi. Nimeona kama imeongezwa ushuru katika kadi za simu. Simu mlaji wa mwisho ni mwananchi, kwa hiyo unavyoongeza kitu chochote kinachohusiana na simu, hakimpati yule muuzaji, mfanyabiashara yeye anahakikisha tu kwamba pesa zake zinarudi. Kwa hiyo, ninachoomba Serikali ikokotoe vizuri mapato, sio kupoteza mapato, maana inaonekana mashirika ya simu yanapata faida kubwa, lakini Serikali haiwafikii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sina la zaidi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Khadija, mara zote umekuwa ukisema wakati ambao unaona ni muafaka kwako na kwa kweli unachokisema, unakuwa umejianda vya kutosha. Hongera sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mheshimiwa Shibuda, halafu Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid ajiandae, atafatiwa na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu na muda ukitosha, tutamalizia na Dr. Mzeru Nibuka, Mbunge wa Morogoro Mjini.

**MHE MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata fursa hii ili nami nichangie hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Maswa, viongozi wa Serikali na watumishi wa Serikali, Madiwani na watumishi wote wa Halmashauri Kuu, wanachama wa CCM na viongozi wa CCM wa ngazi zote pamoja na Mabalozi wa Nyumba Kumi Kumi, mke wangu na watoto wangu, naomba nitoe shukrani za dhati sana kwamba nimepata fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kutukia fursa hii, kumshukuru Mheshimiwa Rais na kumpongeza kwa juhudi zake katika huduma zote na vilevile kuhakikisha nidhamu ya watumishi wa Serikali inaimarika, walikuwa wanakokotoa kwa uhondo wa madaraka, rasilimali za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, naomba kutumia fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa juhudi zake zote pamoja na wadau wote waliofanikisha ujenzi wa bajeti hii iliyo mbele yetu. Nampongeza Mheshimiwa Dr. Kigoda pamoja na Kamati yake, pamoja na watu wote waliohangaika na kuhusika katika kuhakikisha kwamba wanaboresha bajeti yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nachukua fursa hii pia kumpongeza Spika kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kusimamia Bunge la Tanzania, ili lisiwe Baraza la kutunga sheria bali liwe pia na jukumu na kuhakikisha tunatekeleza wajibu muhimu kwa Watanzania na wananchi wote kupitia Bunge hili. Amesimamia mageuzi, amesimamia shughuli zote na mabadiliko ya tabia na desturi na vilevile najua katika kutekeleza majukumu haya, ameweza kuunda watu wenye hila na chuki dhidi yake lakini naamini Mwenyezi Mungu yuko pamoja naye na sisi tutaendelea kuungana naye na wakati ukifika basi tutamuombea dua na kuwahamasisha wananchi wahakikishe wanamrejesha katika ushindi wa kishindo mwaka 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile misukosuko hujenga uimara wa binaadamu, basi naamini kwamba yeye ni madhubuti na Wabunge wote wa Tanzania ni madhubuti dhidi ya vishindo vyote vitakavyojitokeza hasa kwa wale ambao wana jaribujaribu kumendeamendea Majimbo na naomba niwaambie kwamba Majimbo yote sio tunda mwitu yana wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba bajeti kazi yake kubwa ni kusadikisha utekelezaji wa ilani na uchaguzi. Kwa Tanzania, naomba kubainisha kwamba wapiga kura, si wale tu wanaotoka katika Majimbo ya Mawaziri, Manaibu Mawaziri na Makatibu Wakuu, kwamba ndio wale wenye fursa ya kuweza kukipa ushindi Chama chetu cha Mapinduzi. Napenda kusema kwamba viongozi wetu ambao wapo katika dhamana mbalimbali, Mawaziri, Makatibu Wakuu, ni vyema wakahakikishe keki hii tunaigawana sawiya katika Majimbo ili tuamshe msisimko wa wananchi kuelewa kuwa bajeti ya Taifa ni kwa maslahi ya Taifa. Hivyo tusiangalie kwamba mtu ambaye hayupo kwenye Kamati fulani basi mgao wake unakuwa mdogo. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mawaziri wote, nawaomba hili mlitazame ili tusifikie pahala tukaanza kusema humu

kwamba kwa nini kuna kiwango hiki kimezidi, kwa nini kuna bilioni 15 wakati sisi katika barabara za vijiji Maswa pesa ni kidogo, maeneo yanayozalisha pamba, pesa ni kidogo. Kwa hiyo, naomba hili niliseme ili tuweze kuwa na msisitizo wa kwenda pamoja katika kugawana rasilimali za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeomba fidia kwa ajili ya migogoro ya vijijini ambayo tumetoa kujenga shule na vituo vya afya. Pesa ni kidogo sana ninayoomba, milioni 106 tu, barabara vijijini, tunaomba milioni 820 ili tuweze kufidia, ili tuweze kuibua uzalishaji wa pamba, lakini tunazungushana, tunazungushana, lakini je, maeneo ambayo wanatoka viongozi, migao yao ipo namna gani? Nimezungumzia kila wakati juu ya Idara ya Afya, tunalaumiwa Watanzania wa Kisukuma tuna imani potofu, tunalaumiwa kwamba tunaenda kwa waganga wa jadi, je, kwa nini wananchi wasiende kwa waganga wa jadi ikiwa hakuna *ambulance* ya kumtoa alipo na kumpeleka hospitali! Mtu anakaa kijijini umbali wa kilomita 100 kufika hospitali ya Wilaya. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aje katika Hospitali yetu ya Wilaya. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha kaeni mtafakari; Watanzania wa Kisukuma wamechoka kushtakiwa ni wachawi, wanauwa vikongwe, wakati ninyi hamfanyi juhudi zozote za kuondoa kero hiyo kwa kuweka utaratibu maalum wa kuwakomboa. Nawaomba watani zangu tuungane tuhakikishe ndugu zenu Wasukuma wa Kitanzania, wanaokolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia sasa suala la Katiba yetu ya Tanzania na naomba kunukuu Ibara ya 9 ambayo inasema kwamba lengo la Katiba hii ni kuwezesha ujenzi wa Tanzania yenye undugu na amani na kufuata siasa ya ujamaa na kujitegemea, kwa kuzingatia mazingira yaliyomo hapa Tanzania na kwa hiyo shughuli za Serikali yetu inapaswa kuhakikisha kwamba utajiri na utamaduni wa Tanzania unaendelezwa, unahifadhiwa na unatumika kwa manufaa ya Watanzania wake wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ndio mtaji mkuu wa kutekeleza mikakati mbalimbali ya kustawisha uchumi na ustawi wa maendeleo ya jamii. Sasa mwenendo wa bajeti yetu, mimi nashindwa kuelewa, makusanyo yake na utegemezi wa kupata misaada kutoka nchi mbalimbali. Je, bado tunaendelea kujenga siasa ya ujamaa na kujitegemea? Je, tunajenga Serikali yetu kwa muujibu ya matakwa ya Katiba kwamba ni ya ujamaa na kujitegemea au tumepoteza mwelekeo? Naiomba Serikali itusaidie kuelewa, kwa sababu, mdai chake huambiwa mbaya; sasa hivi tunajiuliza, wafadhili au wahisani ambao wanatoa michango mbalimbali, wawekezaji wanakuja na itikadi zao ambazo ni za ubepari, tulisema ubepari ni unyama, tukasema ni unyampala, tukaupiga vita, lakini je, leo tuna dira gani? Serikali yetu inatekeleza kweli ujamaa na kujitegemea? Naomba tusaidiwe. Je, tutagaramia vipi, maendeleo ya nchi yetu kama sisi wenyewe hatuna uwezo wa kukusanya mapato yetu ndani ya nchi? Kwa mfano, Wakenya sasa hivi wanaweza kukusanya mapato ndani ya nchi na wameweza kuhimili mahitaji ya Serikali. Je, tunajenga ujamaa na kujitegemea baada ya miaka mingapi? Wakati sasa hivi tunazungumzia mgogoro uliosababishwa na mtikisiko wa uchumi, je, kweli mgogoro wa kuinua uchumi wetu umekuwa unakuwa kwa kiasi gani? Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atusaidie kutuelimisha na kutuhabarisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iwe na ujasiri wa kusema kama kweli tunaendelea na ujamaa au tumeondoka nao. Serikali yetu, haitaki kuuza mtaji wake; pamba mwaka jana tu imeingiza bilioni 196. Bodi ya Pamba inahitaji bilioni 2 ili kuongeza uzalishaji wa pamba, lakini Serikali haitaki kutoa. Je, Serikali hii, kama inataka kujenga Serikali ya ujamaa na kujitegemea, inasaidia pesa kiasi gapi kwenda katika bodi zote ili kuendeleza zao la pamba? Je, ziliomba shilingi ngapi na wamewapa nini? Je, ni mikakati gani Serikali mnajiandaa nayo ili kuhakikisha kwamba uzalishaji wa pamba unakua wakati usimamizi haupo! Naomba hilo Serikali ijiandae kunijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na mashirika ya umma, Shirika la Reli lilikuwa na uongozi mzuri sana, lakini kwa sababu ya ufinyu wa mitaji, limekufa. Tukaagiza Menejimenti kutoka nje, hivi kila mahali Watanzania tutashika lini hatamu za nchi yetu ikiwa kila jambo tunataka wageni waje kutusimamia na kutuendelezea? Tulitafuta uhuru wa nini, tutashika hatamu lini? Serikali na Baraza la Mawaziri, naomba mtusaidie kutuambia maana ninyi ndiyo mnasimamia mikataba, ninyi ndiyo mnasimamia shughuli zote za kila siku. Naomba mtusaidie kutueleza, mnatupeleka wapi ninyi Mawaziri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutagharamia vipi maendeleo ya nchi yetu ili matakwa ya Katiba ya kujenga ujamaa na kujitegemea yatekelezwe? Mwegemeo wa uchangiaji wa shughuli za uchumi wetu na pato la ndani ya nchi au pato la taifa unategemea kilimo. Lakini kilimo kimekua kwa asilimia ngapi? Mwaka 2007 - 2000 kimekua kutoka 4.2 hadi 4.6%. Sasa hizi, sijui ni parapanda, mimi nashindwa kuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunazungumzia masuala ya vitambulisho; mimi naomba ku-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wakala wa Kutengeneza Vitambulisho, iondoke Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa sababu ni malumbano tu. Lakini hasara tunayopata kutokuwa na vitambulisho ni kubwa sana. Vitambulisho vinasaidia sana makusanyo ya mapato, kwa mfano tungekuwa na vitambulisho na naomba nitoe takwimu za walipa kodi Tanzania wapo kiasi gani. Mwaka 2004 mwezi Juni walikuwa 259,799; mwaka 2005, 318,000, mwaka 2006, 287,000, mwaka 2007, 334,000; mwaka 2008, 398,000, tuko *population* ya zaidi ya milioni 40, tunawalipa kodi ambao wangeweza kuchangia hapa kwenye *formal sector*, Tanzania tukapata *a lot of money*. Naomba kutoa mfano mmoja kwa sababu muda hautoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tungekuwa na walipa kodi wanaolipa na wanaostahili kulipa kodi ni milioni 18 katika milioni 40. Je, kama hawa Watanzania wangekuwa wanalipa shilingi 3,000/- tungekuwa tunakusanya bilioni 324 kwa mwaka. Lakini kwa sababu hakuna vitambulisho hatuwezi kukusanya na huo uhujumu uchumi. Tusibebane, uongozi wa kubebana umepitwa na wakati, panapotokea mtikisiko wa kwamba mtu hataki maslahi ya nchi, anataka atambulike, abebeke yeye, ni vyema akatupisha, *the struggle must continue*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niyaseme haya kwa sababu, siasa ya kushika hatamu za uongozi, iko mikononi mwetu. Naomba Serikali itekeleze ahadi ya kuwapa maisha bora wafugaji. Hivi, kwa nini masuala ya mifugo yapo nusu nusu, TAMISEMI, mara Maendeleo ya Mifugo na je, kwa nini hatutaki kutumia rasilimali zetu? Naomba kuwauliza Baraza la Mawaziri, ni kwa nini Tanzania tuna mikataba mibaya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini tutapeleka kesi Umoja wa Mataifa, kuwashtaki wanaotudhulumu kupitia mikataba mibovu, kama ambavyo Mahakama ya Dunia inavyowashtaki viongozi walionyonya Tanzania na kuwa na utawala mbovu na demokrasia kuhatarishwa. Je, unyonyaji huu hauhatarishi demokrasia na utawala bora katika nchi tunazonyonywa madini yetu? Baraza la Mawaziri, hivi ni nani anayesababisha mikataba mibovu? Waheshimiwa Mawaziri na Baraza la Mawaziri, tuwaambieni Watanzania, kila mara kuna kuwa na mikata mibovu, ya madini, Bandarini, *TICTS*, Air Tanzania na vyote vinapitia kwenye Baraza la Mawaziri, je, uzalendo wenu, utapimwa vipi na tutahakikishiwa vipi kwamba ninyi ni wenzetu katika kujenga ujamaa na kujitegemea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya maziwa Tanzania hakuna. Tanzania tumekuwa soko la maziwa, yanakuja yanatupwatupwa hapa, kila nchi inaleta maziwa. Mifugo yetu na kulinda kwetu rasilimali zetu, zitakuzwa vipi kama ninyi wenyewe hamtengenezi wigo wa kulinda rasilimali za Tanzania? Viwanda vitawezaje kukua? Je, Tanzania, mna mpango gani na viwanda vya pamba ili bei ya kununulia pamba ikue. Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Baraza la Mawaziri, mna mpango gani kwa viwanda vya nguo ili bei isiwe inayumba? Mna mpango gani wa rasilimali mifugo kwa sababu wafugaji wamechoka kuwa na ng’ombe nyingi? Wanataka ng’ombe mbadala ya matrekta ili wafugaji, wakulima waweze kuendeleza kilimo katika nchi hii. Je, kama mnategemea wawekezaji kutoka nje, ni imani yangu Watanzania watakuwa manamba, tumechoka, tunaomba mtekeleze Azimio la Arusha, Ilani ya Uchaguzi wa CCM na mtekeleze matarajio ya Chama cha Mapinduzi kwa wananchi. Nchi ya Tanzania itajengwa na Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya mkulima wa pamba inazidi kuyumba, sasa naiomba Serikali ijiandae kuhakikisha kwamba pembejeo zinapunguzwa bei, kwa sababu bei ya kuuzwa kwa pamba siku hizi, iko chini sana. Kwa hiyo, hawatamudu na kama hawatamudu kununua pembejeo, basi ubora wa pamba utateremka, mapato kwa taifa yatayumba, sasa sijui tutakuwa tunaomba tena Umoja wa Mataifa utusaidie?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhuru wa Tanzania uko mikononi mwetu na utalindwa na Watanzania wenyewe. Kusimamia rasilimali na pesa vijijini; Watendaji wa Kata hawana mafunzo wala *book-keeping* na hawana hata vitabu. Je, hawa watu watawezaje kuhamasisha hata mafunzo ya *fund raising* wakati wa misimu ya kuuza, hawajui kuhamasisha umma ili uweze kuchangia mapato kwa ustawi na maendeleo katika vijiji. Ninaomba Ofisi ya Waziri Mkuu waandae utaratibu maalum wa kuelimisha na kuwapa mafunzo ili tuweze kuhakikisha wanakuwa na uwezo wa kuhamasisha umma kuliko kutumika ubabe wa dhamana za madaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutengeneza vitambulisho, naomba kurudia ni hoja nzito ambayo ni muhimu ikapewa uzito wote na tukahakikisha kwamba tunaweza kufanikisha kujitegemea. Mimi nitamuomba Waziri Mkuu, nitampa *research* iliyotengenezwa ya kuhalalisha …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, kengele ya pili.

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naahirisha kuunga mkono hoja, nikisubiri majibu. *(Makofi)*

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu mdogo kwenye hii bajeti iliyosomwa mbele yetu. Nitakuwa naenda taratibu sana maana msemaji aliyepita kidogo ametupa mchango moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, niipongeze Serikali, niwapongeze Watendaji wa Wizara kwa kutuletea hii bajeti. Bajeti ni ya wananchi hata kama wengine hawataki hivyo lakini hali ndivyo ilivyo na kwa maana hiyo ninasema kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, mimi ninaiunga mkono 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuiunga mkono bajeti hii labda niseme kwamba mimi ni mjumbe ambaye ni Makamu Mwenyekiti kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali, kwa hiyo yale ambayo nitakuwa ninayazungumza mara nyingi yatakuwa ni yale ambayo kwa namna moja au nyingine yalikuwa yanajitokeza katika vikao vyetu vya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwanzo ambalo nitaanza kuliongelea ni suala la utegemezi wa bajeti. Bajeti yetu imekuwa tegemezi na imekuwa hivi kwa kipindi kirefu sana kwamba hizi fedha ambazo tunazizungumzia humu kwa kiasi kikubwa sana huwa tunazungumzia na michango ya wahisani. Lakini hali halisi ambayo tumekuwa tukiiona kwenye Kamati ni kwamba kwa upande wa wahisani vilevile kumekuwa na ahadi nyingi kuliko utekelezaji. Kwa hivyo, ninaishauri Serikali na tumekuwa tukiishauri hivyo hata katika vikao vya Kamati ambavyo tumekuwa tukiongea na Watendaji Wakuu wa Wizara mbalimbali kwamba sasa basi na ufike wakati Serikali ianze kujichomoa taratibu sana kwenye utegemezi. Kidogo kidogo tuanze kujitegemea, tuanze kupanga bajeti kwa kile kidogo ambacho sisi tunacho na tuache kutegemea wahisani kwa sababu utegemezi kwa wahisani unafanya isomwe bajeti na ionekane kwamba ni kubwa sana lakini kwa kiasi kikubwa kile ambacho kinasomwa humo ambacho kinatokana na wahisani hakifiki kama vile inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa linalojitokeza hapa ni kwamba Mhisani anapokukosesha zile fedha au unaposhindwa kuzipata kwa wakati sababu zinazotoka kwanza watakwambia kwamba ooh, unajua ninyi mwaka wenu wa bajeti na mwaka wetu

haviendi sambamba. Lakini wakati mwingine wanapokosa sababu ya aina hiyo wanakuja na sababu za ahadi ambazo zinatolewa na Watendaji pamoja na hao wengine ambao wanakwenda ku-*negotiate* hiyo misaada ambayo tunaitegemea. Lakini kwa ujumla wake ni kwamba tuanze taratibu sana kuondokana na utegemezi kwa sababu wapo wenzetu ambao kwa kiasi kikubwa sana wanajitegemea wenyewe kwa fedha zao za ndani na wanakwenda. Hicho hicho kidogo tulichonacho tukipangie matumizi halafu hizi ahadi tuzipokee; wakiahidi kutusaidia ni sawa na tuwasikilize na tuzipokee lakini tusiziingize kwenye bajeti tusizioneshe kwa sababu hatuna uhakika nazo. Kwa maana hiyo ningeitaka Serikali iseme kwa uhalisia kabisa kama ambavyo tunaona kwenye vitabu vya *CAG*, ni asilimia ngapi ya kile ambacho tunaahidiwa na wafadhili tunakipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiliacha hilo nizungumze hili ambalo limeugonga ulimwengu mzima, huu mtikisiko wa kiuchumi. Mtikisiko wa kiuchumi umeigonga dunia nzima na sisi Tanzania ni sehemu ya dunia, sie sio kisiwa na sisi kwa namna moja au nyingine tumeguswa na mtikisiko wa kiuchumi lakini linalosikitisha ni kwamba rasilimali tulizonazo katika nchi hii hata hapo kabla ya huo mtikisiko wenyewe wa kiuchumi zingestahiki sana sisi tuweze kujiendesha wenyewe bila hata kuwategemea hao wafadhili kama nilivyotangulia kusema wakati nilipokuwa nalizungumza lile suala la mwanzo. Sekta ya madini tuhakikishe kwamba sekta hii kwa kiasi kikubwa sana inashiriki kuchangia katika uchumi wetu, kwa sababu sasa hivi hata hao wenye madini wanaanza kisingizio hichohicho kwamba uchumi umewagonga lakini hapo kisingizio kilipokuwa hakipo tulikuwa hatupati kitu kutokana na madini kama ambavyo tungestahili kupata kama zinavyopata nchi nyingine. Kuna nchi zinaendeshwa na madini tu, sisi tuna maeneo mengi sana na madini kama dhahabu kwa kiasi kikubwa sana hayajaathirika na mtikisiko huu lakini hata wao watakupa sababu hiyo hiyo kwamba tumetikiswa. Kwa hiyo, Serikali ijaribu kuangalia kwa karibu zaidi chanzo hiki cha madini ili kiweze kuendesha uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la mafuta, wenzangu wengi sana wamelizungumzia labda na mimi nilichangie kidogo tu. Mafuta yamekuwa yakipanda na kushuka bei zake lakini huku kwetu kumekuwa na tofauti kidogo, mafuta yakipanda tunapanda nayo lakini yakishuka tunashuka kidogo sana ingawa mafuta yanashuka sana. Kuna wakati yalikwenda yalifika mpaka zaidi ya dola 100 kwa pipa, ikashuka mpaka 40 lakini *fluctuation* ile sisi hatukwenda nayo vile; sisi tulipanda halafu baadaye tukashuka tena kidogo. Sasa hili suala liangaliwe kwa sababu mafuta yanagusa karibu kila sekta ya uchumi na kiasi kikubwa sana pia yanagusa huu mtikisiko kwa hiyo Serikali idhibiti kidogo suala hili la mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo ninapenda kuichangia ni sehemu ya ukusanyaji wa mapato. Mimi niwapongeze *TRA* kwa sababu wanachokikusanya huo ndio uwezo wao lakini wanatakiwa waangalie maeneo mapya ya makusanyo ya kodi. Lakini sehemu mojawapo ambayo ninapenda kuwashauri ni sehemu ya upunguzaji wa kodi yenyewe kwa bidhaa mbalimbali. Si kwamba kila ukipandisha kodi ndio unakusanya zaidi, unapopandisha kuna watu wengine unawasumbua katika zile biashara zao wanaamua kuachana nazo tu wanaenda kwenye maeneo mengine ambayo watakuwa wanapata unafuu. Sasa ule ujanja wa kupandisha kodi kwa mategemeo

kwamba utakusanya zaidi hausaidii lakini pengine ungeshusha kodi kwa baadhi ya vitu ungepata zaidi kwa sababu waletaji huko nje wangekuwa wengi na ungekuwa na makusanyo zaidi na hii sifa ambayo unaipata hivi sasa ungeipata zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kama nilivyosema sio kisiwa. Kutokana na huu mtikisiko wa kiuchumi, nchi nyingi sana duniani zenye viwanda wameathirika sana katika biashara za bidhaa zao mbalimbali na hata hao wafanyabiashara wetu wanakwenda kununua hivyo vitu huko nje wanakuta bei zile ambazo zinatokana na huo mtikisiko kwa maana kwamba bei zimepungua lakini bidhaa zile zinapobebwa zikiletwa huku nchini kodi zetu sisi Tanzania hazijawa na macho ya kuona kwamba dunia imetikisika kiuchumi; sasa *TRA* wangekuwa wanaliangalia suala hili pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano wa suala la magari; magari yameshuka bei huko yanapouzwa Japan na kwingineko, bei ziko chini lakini *TRA* ukija nalo gari wana kijitabu chao sijui ni cha mwaka gani maana yake mtikisiko umeanza kutokea mwaka jana, wana kitabu wao wanakuambia kwa gari hili la mwaka fulani bei halisi ni hii kwa hiyo utalipa kodi kwa mujibu wa hiyo orodha waliyonayo; si kweli kwa sababu sisi si kisiwa na watu wanaokwenda kununua vitu hivyo nje wanapokujanavyo wanakuja na hizo bei walizonunulia za kweli. Kwa hiyo, wawatoze watu kodi kwa bei za kweli walizonunulia huko nje na sio kwa bei wanazowapangia wao *TRA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili litasaidia kwa sababu mtikisiko wasidhani kwamba imetikisika nchi tu lakini ni wananchi wanaoumia zaidi na mwananchi anaumia kwa sababu hiyo fedha yake anayoitumia kwenda kununua hicho kitu nje, akirudi matokeo yake ndio anakuja kukumbana na vitu vya namna hii. Kwa hiyo, *TRA* hili waliangalie kwa karibu sana, bei zimepungua kwa hiyo na wao wawatoze watu kodi kwa bei za kweli walizonunulia bidhaa. Hii pia itasaidia kwa sababu watapata zaidi na Watanzania walio wengi pia wanataka kufaidika na huu mtikisiko kwa unafuu ambao upo ili waweze kumiliki hivi vitu. Kitu kama gari sio anasa sasa hivi, ilikuwa ni anasa miaka ya 70 lakini sasa ivi si anasa tena ni kitu cha lazima, Mtanzania wa kawaida awe nacho ili aweze kujikimu maisha yake pamoja na kile ambacho kinamtegemea katika familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni hili suala ambalo tumekuwa tukilipigia kelele la *pre-shipment inspection.* Suala hili kuna kitengo nafikiri ni cha Wizara ya Bisahara kiko nje wanafanya ukaguzi unaoitwa ukaguzi wa magari lakini kwa kweli kinachofanyika sio ukaguzi, wanauza stika sijui dola 300, ukiwa nje unanunua gari unabandikiwa stika unalileta nchini; ukikosa kuinunua hiyo stika huko nje hiyo adhabu unayopata hapa unalipa shilingi laki nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali, tunataka ku-*account* hizi fedha ambazo zinatokana na mauzo ya hizo stika huko nje za haya magari yote ambayo yanakuja humu ndani. *TRA* tuliwauliza kwa kipindi cha miaka mitatu watuambie ni kiasi gani cha magari kimekuwa kinaingia nchini? Tukaifanya sisi tukazidisha mara bei ya hizo stika tukaona kumbe nchi inakosa pato kubwa sana kwa

sababu fedha zile hatuzioni na hakuna mahali ambapo zinakuwa *accounted,* tulipata karibu bilioni 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kwa nini hiki kitengo kisiletwe kikawekwa hapo bandarini ili fedha hizi tunazozitoa sie Watanzania zibakie hapahapa na zitusaidie kuweka sawa hizi barabara zetu na miundombinu mingine ambayo imekuwa inapata matatizo? Suala hili liangalieni kwa karibu sana kwa sababu tunaendelea kupoteza fedha za kigeni tunazipeleka nje halafu hakuna marejesho tunayoyaona. Kwa hiyo, hili waliangalie ili kama ni Sheria ambayo tumeitunga Bunge, basi Sheria za hapa kila kukicha tunaleta *miscellaneous amendments,* tuleteni *amendment* tu-*amend* hili suala ili tuendelee kufaidika nalo hapa nchini na tusiendelee kuwafaidisha watu wachache ambao wako nje Hongkong, Uingereza na Japan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama nilivyokuambia awali nitachangia kisayansi, nitachangia mambo machache sana na ninazidi kuwapongeza Serikali na nilisema kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kwamtipura hii bajeti ninaiunga mkono lakini Serikali iangalie hayo maeneo ili iweze kuboresha pato la wananchi na iweze kuboresha makusanyo na hatimaye tuweze kuwa na miundombinu ambayo inatokana na pato letu halisi na ili tupunguze utegemezi kwa kiasi kikubwa, tuanze kujizoesha kupunguza utegemezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano upo kwetu sisi wenyewe, utegemezi ndani ya familia zetu, huishi kwa kumtegemea jirani kwamba wewe uwe unapika ugali tu na yeye alete mboga. Anapika ugali lakini maarifa ya mboga unayafanya wewe mwenyewe. Kwa hiyo, tuanze kuelekea huko kama nchi tujitegemee. Mtu akikuahidi kukuletea mboga, iwe ni samaki anakuongezea lakini kwa kiasi kikubwa uweze kujitegemea kwa mlo wako. Kwa hiyo, nchi ianze kupunguza kutegemea nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, napenda kumalizia tena kwa kuunga mkono na napenda kutoa shukrani, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niungane na wenzangu katika kuchangia hoja hii ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nakuja kuzungumza hapa nilijiuliza maswali kadhaa na swali moja ambalo nilijiuliza ni methali ya zamani na swali la zamani sana waliulizwa watu kwamba, *"what do you see?"* na mimi jana usiku nikawa nafikiria ukija kwenye hili Bunge useme nini? Ni kitu gani nakiona? Lakini swali la pili nikalipata, "wewe unatoka wapi"? Yaani mimi Lazaro Nyalandu. Mimi natoka Singida, Jimbo la Singida Kaskazini. Mkoa wa Singida una wananchi sasa kuzidi milioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi uliopita kwa mara ya kwanza kabisa tulienda kushuhudia na kwa furaha kabisa ujenzi wa barabara ya lami inayoanzia Singida inaelekea Khatesh, inatoka Khatesh inaenda Babati, inatoka Babati inaenda Minjingu na Arusha. Katika lile swali langu la kwanza, *what do you see?* Mimi niliona *progress* na wananchi wa Singida wamefurahi sana kwamba kwa mara ya kwanza tunaona barabara ya lami inayounganisha Mkoa wa Singida na Mkoa wa Arusha. Hiyo ni *production route* kubwa sana kwa wananchi wa Singida Kaskazini lakini wananchi wote wa Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikajiuliza swali lingine, ninaona nini kufikia Disemba mwaka huu? Barabara inayotoka Dodoma kwenda Manyoni kwenda Singida ina uwezekano mkubwa sana itakuwa imekamilika. Maana yake ni hii, mimi kama Mbunge wa Singida, katika miaka yote ya Ubunge wangu tumeomba, tumeisihi Serikali, tafadhalini sana tuunganishwe na Mikoa mingine. Mtu atatoka Dar-es-Salaam kwenda Mwanza kwa kupitia Dodoma na Singida kwa barabara ya lami. Nchi hii inafanya *progress* ambazo ni vigumu sana kuzielezea ila ni rahisi mimi kuja hapa na kuelezea yale ambayo hayajafanyika; ni rahisi sana kama Mbunge. Kuna mtu mmoja alisema *there is more in loving good than hating what is evil.* Ninaweza nikachagua mkono wangu wa kushoto nikatoa hotuba inayoelezea kila kisichofanyika Singida Kaskazini lakini nikasahau 90% ya mema yote yaliyofanyika katika miaka mitatu iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imekuwa ni nchi ya kwanza katika nchi za Afrika ya Mashariki na Afrika ya Kati kwa pamoja kwa kufanikiwa kujenga Chuo Kikuu kikubwa. Narudia, katika nchi hizi zote *Makerere University* imekuwa na wanafunzi zaidi ya elfu hamsini, imekuwa ni kitivo cha elimu katika Afrika ya Mashariki lakini kwa mara ya kwanza katika miaka minne tu Tanzania imefanikiwa kujenga Chuo Kikuu ambacho kitafikia *capacity* ya wanafunzi elfu arobaini. Nikajiuliza unaona nini, naona *progress* na ni *progress* ya kufurahisha, siongei hapa kumfurahisha mtu yeyote, ninapenda Watanzania waone upande wa pili wa mema yanayofanyika. Halafu kila siku nilipokuwa naenda *Sunday School* nilifundishwa jambo linasema shukuruni kwa kila jambo lakini unashukuru zaidi kwa jambo zuri linalokuwa linatendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki mbili zilizopita nilienda kijiji kimoja kinaitwa Kijota kuangalia kisima cha maji kilichokuwa kimeshindikana, kilichimbwa mita 200 hawakupata maji. Siku mbili baadaye nikasikia *BBC Swahili Service* wakitangaza jinsi ambavyo Singida ni vigumu sana kupata maji; wanachimba mita 200 hadi 250 hawakupata maji lakini baadaye walifanikiwa kupata maji, habari iliyokuwa imeenda ni kwamba walichimba mita 200 hawakupata maji, habari nzuri ikatokea baadaye na ile sikuisikia. Serikali hii imefanya kila jitihada, mimi kama Mbunge wa Singida, tumepata maji kiwango kikubwa tumetengeneza malambo, tumechimba visima, Serikali imewachukua wananchi katika hatua waliyokuwanayo na wananchi wangu wengi wa Ilongero, Kijota na sehemu nyingi wananisikia tumefikia hatua ambayo ningeweza kusema Tanzania *is making Singida proud. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza na baadhi ya wanafunzi wa vyuo vikuu na kesho nina nafasi ya kutoa hotuba kwa *Youth of the United Nations* wakifanyia

mkutano wao pale Dar-es-Salaam. Wengi wa hawa vijana na katika itifaki ya vyuo vikuu nchi tano nilizoziangalia ukiangalia Kenya, Uganda, Tanzania, Burundi, Rwanda na Kongo, Kongo haipo kabisa maana haiwezi ikakaribia tuliko; mpango wa kuwakopesha wanafunzi vyuo vikuu umewezesha kwa mara ya kwanza kutoa wanafunzi wengi kuliko *job market.* Tuna wanafunzi wengi wanaohitimu chini ya huu mpango, nchi hii *is making progress, this Nation is going forward.*

Mimi ninapenda kila mtu unapoitazama Tanzania, unatazama upande wa kwanza wa shilingi na wa pili wa shilingi. *Progress* ambayo tunaifanya katika elimu ya shule za msingi, Singida kule katika Jimbo langu kila kijiji, wakati mwingine vijiji vingine vinatengeneza shule mbili shule za msingi *literate rate* ya Tanzania inakuwa zaidi ya ule mpango wa *millennium goal.* Kwa ufupi ni kwamba tuna watu wengi wanaojua kusoma na kuandika kuliko nchi nyingi duniani, ninazungumza kama Mbunge wa Singida, tuna watu wengi wanaojua kusoma na kuandika. Nchi hii ina *make progress.* Nchi hii inapiga hatua ambazo mimi kama Mbunge *back bencher* nikizingalia, ninafurahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes*, kuna matatizo mengi ambayo tunapambana nayo. Lakini zile ni changamoto ambazo ninapenda tuungane pamoja kama nchi, wapinzani, Wabunge wa CCM tuisogeze nchi hii hatua mbele. Nchi hii haijengwi na mtu mmoja, nchi hii haijengwi na Baraza la Mawaziri peke yao, nchi hii haijengwi na Wabunge peke yao, sio Madiwani peke yao, kila Mtanzania ana nafasi na wajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge la Tanzania limefanya *progress*, hivi karibuni nilipita Australia na watu wanauliza wanasema nchi hii ya Tanzania *is the most beautiful*, ni nchi ambayo *a lot of people* wangetamani kuja kufanya biashara hapa. Tunayo nchi nzuri ambayo wenyewe na wengine wanashiriki kuibomoa. Nchi hii imebarikiwa, Chama cha Wananchi *CUF, CHADEMA* na vyama vingine vya kisiasa vikiongozwa na *CCM* vimefanya vizuri katika kuhakikisha kwamba *freedom of expression* ipo. Hili linatuletea heshima sisi kama wananchi wa Tanzania. Ukienda Darfur hakuna demokrasia, ukienda Somalia hakuna demokrasia, naweza nikataja nchi nyingi, *Central African Republic*, lakini Tanzania unaweza ukawa Mbunge kutoka Singida Kaskazini ukaweza kusimama katika Bunge na kuliambia jambo, y*ou are making this Nation proud. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipita Jimboni wiki tatu zilizopita nikakutana na mama mmoja aliyekuwa amesimama katika shamba lake la uwele na ulezi. Hili shamba lilikuwa limestawi na ni kijiji cha Kijota. Nikasimama, nilikuwa natembea na Waandishi wa Habari wengi tu, nikaenda kumuona nikamwambia mama hongera umestawisha mazao yako. Huyu mama nikamwambia ongea na Waandishi wa Habari waambie jinsi ulivyobarikiwa. Huyu mama akasema hapana, lakini najua tu nitakuwa na njaa. *This attracted our attention,* nikasema mama mazao yamestawi kiasi hiki halafu unasema utakuwa na njaa! Akasema ndio mume wangu hadi kufikia sasa hivi saa nne amelewa. Jambo la kwanza tunapobarikiwa, tukubali kwamba tumebarikiwa, nchi hii haiwezekani tukaendelea kuomba chakula wakati vyakula tumebarikiwa, tunavyo, ardhi tunayo. Pale Singida Kaskazini watu wengi wana mazao ya kutosha. Nikawaambia katika mkutano wa hadhara, sitegemei mtu aje aiombe Serikali chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kusema, tuna wajibu kwa Watanzania wote wa kawaida, kwa Viongozi, kila mtu afahamu kwamba ana wajibu wa kuifanyia nchi hii kitu. *J. F. K.* alisema usijiulize nchi yako itakufanyia nini, usijiulize Baraza la Mawaziri litakufanyia nini, Wabunge watakufanyia nini; jiulize wewe mwenyewe uwe Mbunge, uwe mwananchi, uwe mkulima, utaifanyia nini nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya msemo unaonifurahisha sana hapa duniani ni ule uliosema, *let the weak say I am strong and the poor say I am rich,* kwa sababu kimsingi hakuna mtu maskini katika nchi hii kwa sababu utajiri uliainishwa kwa kitu kinachoitwa *landlord,* Watanzania wote wanao uwezo wa kumiliki ardhi na wote ni ma-*landlord* wadogo wadogo na wakubwa wakubwa. Tuchukue nafasi hii kuiambia dunia nchi ya Tanzania *not only is making progress* lakini nchi ya Tanzania ina *capability* ya kuishangaza dunia kwa kiasi ambacho tunaenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba wanafunzi walioko katika vyuo vikuu na sekondari nchini Tanzania wafahamu kwamba kila mtu ana wajibu ambao amepewa na Mungu wa kuhakikisha kwamba nchi hii itasogea hatua moja kwa sababu yake. Mariah Carey, muimbaji maarufu alisema *there is a hero that lays in you.* Kila mtu aliyekaa hapa *there is a hero; there is something within you,* kinachokaa ndani yako na kinachoweza kukusukuma uisogeze nchi hii hatua moja mbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *GDP* ya Tanzania imezidi sasa hivi ni bilioni 24, Kenya wametuzidi lakini tunawazidi Uganda, tunawazidi Rwanda, tunawazidi Burundi, kuna nchi nyingi sana tunazozizidi. Lakini ninaomba hesabu kamili ya mali za Tanzania itolewe, mimi nina uhakika dunia itashangaa Tanzania tuko hatua gani. Ninaomba, sasa hivi tunasema tunataka tuwe *mini tiger,* hakuna sababu ya Tanzania kuwa *mini tiger* tuwe *tiger* mwenyewe; tunao watu wengi wanaosoma, tunao Viongozi ambao wamebobea na wamekuwa hapa muda mrefu tunaweza kutumia muda mwingi sana kulaumiana tukaacha kutumika huu muda kuijenga nchi, kuisogeza hii nchi mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwaambia katika Bunge lililopita na niseme hili nimalizie; nchi hii ina masaa 24 ya kufanya kazi. Amerika wanafanya kazi masaa 24, Rwanda, Kenya, Uganda, Burundi, Tanzania tu ndio mahali ambapo inapofika usiku watu wote wanalala, Wabunge wanalala, Mawaziri wanalala, wakulima wanalala, madereva wa malori wanalala, wa matrekta wanalala, wote wanalala; kila mtu anaenda kulala, wengine wanalala saa mbili usiku. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika*
*kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nyalandu, muda wako umeisha.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninaomba nchi hii ifanye kazi masaa 24 na ilindwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Lazaro Nyalandu. Niseme tu kwa wale wasiomfahamu Lazaro Nyalandu, ni Mwenyekiti wa Wabunge Vijana ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mimi kama Mbunge kijana ndani ya Bunge hili basi nakupongeza Mwenyekiti wangu kwa mchango wako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba nimwite Dr. Mzeru Nibuka na kama nilivyosema msemaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Mnyaa. Dr. Mzeru, tafadhali.

**MHE. DR. OMAR M. NIBUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti hii ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mungu wa rehema ambaye amenipa nguvu za kuweza kusimama hapa pamoja na Wabunge wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kwanza kumpongeza Kaka yangu Waziri wa Fedha na Uchumi, pamoja na Manaibu wake wote wawili, Katibu Mkuu na Watendaji wengine wote kwa jinsi walivyotuletea hii bajeti ambayo imelenga sana mazingira ya nchi yetu pamoja na hali halisi hasa kwa kipindi hiki cha msukosuko ya uchumi duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mjumbe katika Kamati ya Fedha na Uchumi, kwanza ninapenda niwapongeze sana hii timu ya Waziri wa Fedha kwa jinsi walivyokuwa wasikivu kwanza walipoleta *proposal* yao ya bajeti kwetu kwenye Kamati ya Fedha. Nakumbuka tulikutana nao mara mbili, mara ya kwanza, walileta tukawaambia mrudi mkatuletee tena na kwa kweli baada ya kufika hapa nimeona kuna mabadiliko makubwa sana yamefanyika ukilinganisha na mara ya kwanza walipotuletea bajeti yao. Kwa hiyo, nawashukuru sana kusema kweli na hizo ndizo busara za mtu mwenye kutaka kufanya kazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba nijikite kwenye suala la Kilimo Kwanza lakini, wakati najikita kwenye suala la kilimo, kwanza kabisa napenda nimpongeza sana Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuamua kwa makusudi kwamba, Kilimo kimepewa umuhimu wa kwanza na hivi juzi tu aliitisha Mkutano mkubwa pale kwenye Hoteli ya Kunduchi, Mjini Dar es Salaam ambao uliwakutanisha wadau wakubwa wapatao 400 ndani humo kulikuwa na Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Ma-DC, Wabunge, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na kadhalika, kusema kweli alifanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu ni mtu ambaye anajua sana au anaonekana kuguswa sana na maendeleo ya Watanzania wote. Hata wakati wa mazungumzo yake utaona kwamba kwa kweli inamgusa kuhahakikisha kwamba, wananchi hawa wa Tanzania wanakuwa na maisha bora na ndiyo maana akaanza na kusema Kilimo Kwanza, akijua kwamba, Kilimo ndiyo mkombozi kwa Watanzania hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu wakati akifafanua katika mkutano ule, kusema kweli nilikuwa namuangalia kwa makini sana, ilifikia mahali mpaka nikawa naona kama machozi yananilengalenga nikifikiria kwamba, yeye mwenzetu ana muono wa ndani sana ambao pengine sie tunaomsaidia hatujauona. Utampata wapi Rais yule ambaye anazunguka karibu dunia nzima kuhakikisha kwamba, Watanzania wanapata maslahi? Kila mara anaporudi faida tunaiona na kwenye Mkutano ule alituambia kwamba, zipo nchi kwa mfano Japan, China, Marekani n.k ambao wametukubalia kutuunga mkono katika suala la Kilimo, kwa hiyo kilichobaki ni sisi sasa watendaji tuongeze nguvu tufanye kazi zetu kwa bidii ili tuhakikishe kwamba, Kilimo kinatuvusha hapa tulipo, kwa kweli nampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi wote mtakuwa mashahidi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati wa kuomba kura za uchaguzi mwaka 2005 alizunguka kwenye majimbo yote. Lakini hivi karibuni ameamua kuzunguka kwenye Majimbo yote tena ili kuwashukuru wananchi ambao walimuweka madarakani. Lakini utakuta wakati akija kwenye Mikoa, wakati wa mazungumzo inaweza ikafikia mpaka saa nane usiku, nyinyi Wajumbe mnasikia usingizi wa kuanza kulala lakini yeye yuko macho kabisa, unaweza ukahisi labda pengine kuna dawa anazitumia ili asilale, kumbe siyo kweli ni kwamba, anawajibika, anajituma kwa Watanzania, kwa kweli Mungu amjalie, ampe afya njema ili kusudi aweze kutusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa na chakula cha kutosha pamoja na cha kuuza nchi za nje, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliamuaa Mkoa wa Morogoro kuwa Ghala la Taifa la Chakula. Toka ameamua hivyo sasa huu ni mwaka wa tatu, lakini aliamua hivi kwa kujua kwamba, Morogoro anaifahamu vizuri, ni Mkoa ambao kwanza una ardhi yenye rutuba ya kutosha, una mvua ya wastani, ina hali ya hewa nzuri, lakini ni njia panda ambapo kila mtu kufika Morogoro ni rahisi mno, lakini pia ni rahisi kupeleka pembejeo za kilimo pamoja na mbolea kwenye mashamba, lakini pia hata baada ya kuvuna, kuchukua mazao hayo kuyaleta mijini au pengine kuyapeleka kwenye bandari ni rahisi mno. Lakini kama hilo halitoshi kuna mito zaidi ya 148 ambayo haikauki kwa mwaka mzima, kwa hiyo Mkoa kama huu ni Mkoa wa pekee ambao Mwenyezi Mungu ameujalia na ndio maana ameamua auchague kuwa Ghala la Taifa la chakula, akijua kwamba, kama tukiweka nguvu zetu katika mkoa wa Morogoro kwa kweli tutapata chakula cha kutosha na ziada ya kuuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ni mkubwa sana, sio mradi ambao unaachiwa Mkoa peke yake, huu mradi ni mkubwa, sasa utakuta sisi kama Mkoa au viongozi wa Mkoa kwa maana ya Mkuu wa Mkoa na viongozi wenzake, peke yetu hatuwezi, tunatakiwa hapa tupate nguvu za kitaifa, huu mradi sio wa Morogoro ni mradi wa Taifa, isipokuwa Morogoro tu ndipo mahali ambapo unafanyika huu mradi. Kwa hiyo, sijajua mpaka sasa hivi Wizara ya Kilimo, imejipangaje katika kuhakikisha kwamba, inausaidia Mkoa wa Morogoro kuweza kufanikisha mradi mkubwa kama huu wa ghala la Taifa la chakula. Nikisema hivyo maana yake mgao wa fedha, vifaa vya kutendea kazi, wataalam n.k, maanake toka tumeanza kwenye mradi huu tuna miaka sasa mitatu, sioni kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachoomba ni kwamba hawa watendaji wetu ambao tumewapa majukumu ya kuhakikisha wanatuongoza katika sekta hii ya kilimo, wasiangalie masuala ya ubinafsi, kama alivyosema jana kaka yangu Selelii hapa kwamba, watu wanajawa na ubinafsi ukitaja kitu ambacho kiko Tabora anahisi kinawasaidia watu wa Tabora, sio kweli, hii yote ni nchi yetu moja. Tunajenga nchi yetu, tunapozungumza reli, reli inaisaidia nchi yetu, tunapozungumza bandari, bandari inaisadia nchi yetu. Ruvuma hakuna reli, lakini tunapozungumzia reli nafikiri Wabunge wa Ruvuma, Mbeya wapi na wenyewe wanaunga mkono wakijua reli hii itatuvusha katika matatizo yetu ya kinchi, sasa nataka kuzungumza kwamba, huu mradi wa Ghala la Taifa la Chakula kule Morogoro tunaita FAMOGATA, huu ni mradi wa kitaifa kwa hiyo naomba Waziri wa Kilimo, Naibu wake na Wataalamu wote wajue mradi huu si wa Morogoro, ni mradi wa Taifa. Kwa hiyo naomba sana wahakikishe kwamba, wanajikita katika kuhakikisha kwamba mradi huu unafanikiwa, ili Watanzania waweze kuvuka pale walipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia Ghala la Taifa la Chakula, sisi wananchi wa Manispaa ya Morogoro, tunazo kero zetu kubwa na zaidi ni mbili. Sasa hivi Morogoro idadi ya watu imeongezeka sana, tuna msongamano mkubwa, lakini kama unavyojua Morogoro ni njia panda ambapo watu wengi na sidhani kama hapa kuna Mbunge anayesema kwamba, hajawahi kufika kwenye Manispaa ya Morogoro, sijui, kwa sababu ni njia panda, ni mahali ambapo ukitoka Mbeya ni lazima upitie Morogoro, ukitoka Songea lazima upite Morogoro na wapi na wapi.

Kwa hiyo nalotaka kuzungumzia ni kwamba, pale Morogoro tunalo tatizo la msongamano wa magari pamoja na watu, kiunganishi chetu ni daraja moja tu, linaitwa daraja la Shani ambalo linatuunganisha watu wa Magharibi na watu wa Mashariki, lakini daraja hili sasa hivi ni bovu, limekatika, limeweka ufa kutokana na mafuriko ya hapo zamani ambapo yalikuwa yamekita katika daraja lile, sasa sisi watu wa Manispaa ya Morogoro tumeona tujenge daraja mbadala ili kulisaidia daraja hili kupunguza msongamano ili liweze kuishi kwa muda mrefu. Kwa hiyo, tunashukuru kwamba, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipokuja Morogoro tulimweleza shida yetu ya daraja, lakini kwa bahati nzuri aliwaambia wananchi wakati wa kuhutubia kwamba, atasaidia hela hizi za daraja, kwa hiyo nimeona nikumbushe tu kwa Waziri wa Fedha, asije akasahau ahadi hii ya Mheshimiwa Rais, kwamba angalau na sisi tupate daraja mbadala kwa sababu tukikosa daraja tutakuwa hatuna kiunganishi kingine tena cha kuhakikisha kwamba, wananchi wanapata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo sisi wananchi wa Manispaa ya Morogoro, katika huduma ya afya tunategemea Hospitali moja tu ya Mkoa wa Morogoro. Hospitali hii sasa hivi imezidiwa, hospitali hii ina Wodi 12 tu na kila wodi ina vitanda sio chini ya 20, kwa hiyo, ukifanya hesabu ni kama vitanda 240 lakini wagonjwa wanaolazwa pale ni kati ya 400 na 800 kwa siku. Sasa utakuta wengine wanalala chini, wengine wapi na kwa kipindi hiki katika kuhakikisha kwamba ile hospitali inaboreshwa kuna ukarabati mkubwa unaofanyika pale hospitalini, kwa hiyo wagonjwa wengi wamesambazwa katika vituo vya afya ambavyo uwezo wake wa kuhudumia wagonjwa sio mkubwa, lakini kwa dharura ile ya kutekeleza ukarabati mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wagonjwa wale tumewasambaza hasa wazazi ambao wanajifungua au wengine wanasubiri kujifungua tumewapeleka kwenye kituo cha afya kimoja kinaitwa Kituo cha Afya cha Mafiga, lakini hapatoshi kwa hiyo sisi katika mwono wetu tulishapanga kwamba, tuwe na Hospitali ya Wilaya ndani ya Manispaa ya Morogoro na tumechagua Kituo cha Afya cha Sabasaba kiwe Hospitali ya Wilaya ili kiweze kuondoa au kupunguza kero za wananchi katika huduma ya afya na tumeomba pesa kwa ajili ya kituo hiki kuweza kuboreshwa. Hata hivyo, Mheshimiwa Rais alipokuja Morogoro alituambia kwamba, atatusaidia fedha za kujenga hospitali, kwa hiyo, namkubusha Kaka yangu Waziri wa Fedha na Uchumi, aone kwamba, miradi hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, asije akasahau kutusaidia kuhakikisha kwamba tunapata hospitali ya kuwasaidia wananchi wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho baada ya kuzungumzia hayo, ndani ya Manispaa ya Morogoro pia zipo sehemu ambazo hazina umeme pamoja na kuwa umeme unatoka Morogoro, eneo la Kidatu na gridi ya Taifa ya umeme inapita katikati ya Manispaa ya Morogoro, Kata mojawapo ni Kata ya Mzinga ambapo umeme wa Gridi ya Taifa unapita pale, lakini nashukuru mwaka jana niliwahi kumuomba Waziri wa Nishati na Madini tukaenda wote mpaka katika eneo lile akaona na akaongea na wananchi kuhakikisha kwamba, angeweza kutuletea *Transfomer* kwa ajili ya kupoza umeme ili wananchi wale waweze kuutumia kwa sababu umeme unaopita pale ni mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimkubushe ndugu yangu, Mdogo wangu, Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja, asisahau ahadi yake ile aliyowaambia wananchi wa Morogoro kwamba, atatuletea *Transformer* na kama mnavyojua *transoformer* ni kitu kidogo ambacho naamini anaweza ili wananchi hawa waweze kupata umeme kwa sababu wasipopata umeme ni sawasawa na mtu ambaye umemuwekea chakula mezani, halafu unamwambia usile kwa sababu ukila labda kitakudhuru na ndivyo ilivyo kwamba umeme unapita pale lakini hawawezi kuutumia kwa sababu umeme ule ni mkubwa. Kwa hiyo, naomba sana Waziri wa Nishati ahadi yake aweze kuitimiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Manispaa yetu, wananchi wangu wamekuwa wakinilalamikia kuhusu suala la upandishwaji holela wa kodi za nyumba hizi za Msajili. Meneja wa Msajili wa Nyumba amekuwa akiwaandikia barua wapangaji hawa kwamba, ifikapo tarehe moja mwezi wa Saba, atakuwa ameongeza kodi na kodi hiyo itaanza mara moja, sasa mimi nilishtuka nikaona pengine labda ni maagizo ya Wizara, lakini kwa bahati nzuri nilipokuja hapa Bungeni nilimuona Waziri wa Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika*
*kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. DR. OMAR M. NIBUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mzeru, nakushukuru sana. Kuna mtu hapa alikuwa ananiuliza kama umesimama, nikamwambia ndiyo ameisimama na anaendelea kuchangia. Kwa hiyo, nakushukuru sana kwa mchango wako Dk. Mzeru na wananchi wa pale Morogoro kwa kweli wamekusikia vizuri kabisa ukiwawakilisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na msemaji wetu wa mwisho, ninaomba mtambue kuwa Mheshimiwa Magdalena Sakaya, toka kipindi cha saa Nne baada ya maswali amekalia Kiti akimwakilisha Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni. Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana na ninaona yuko *busy* kabisa pale anatekeleza majukumu yake sawasawa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namuita msemaji wetu wa mwisho kwa kipindi hiki cha asubuhi na yeye ni Mheshimiwa Mohamed Mnyaa. Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, naomba uchukue nafasi yako sasa.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi kunipatia nafasi. Kwanza, nipongeze hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed pamoja na ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi na michango yetu yote tutakayotoa Wabunge wote humu Bungeni, ikiwa ushauri uliomo katika hotuba mbili zile, nafikiri Wizara ya Fedha inaweza ikapata mengi na tukaweza kufanikiwa, hasa ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni ambapo hakupata nafasi ya kuisoma yote kutokana na muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda na mimi nianze kwa masikitiko kidogo juu ya Wizara hii na kwa kuwa, bado tuko katika kuchangia bajeti hii ya Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi. Jana ilipokuwa inajibu swali Namba 37 lililoulizwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, swali lililohusu umri wa miaka 48 wa uhuru, bado Watanzania walio wengi ni maskini na baadaye akauliza swali kwa nini rasilimali za Watanzania zinawanufaisha majirani? Lakini Serikali ilivyojibu ni kwamba, haina takwimu kwamba, kuna rasilimali za Watanzania zinawanufaisha majirani. Ni kitendo ambacho mimi nasikia ni cha aibu na cha kushangaza na inasikitisha kwamba, Serikali haina takwimu na haijui rasilimali za Watanzania zinazowanufaisha majirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu hilo la Mheshimiwa Waziri, alimtaka muuliza swali amsaidie. Nakuomba, kwa niaba ya muuliza swali, mimi nimsaidie kidogo lakini akazitafute kwa ukamilifu. Hivi leo hatujui kweli aina za magogo yanayoondoka Mikoa ya Iringa, Mbeya, Mufindi huko pamoja na viwanda vilivyobinafsishwa, hivi misitu ni nani waliochukua? Magogo yanatoka kule yanasafirishwa kwenda nchi za jirani na wao misitu yao wamezuia, inavunwa misitu yetu hata *TANESCO* wanaona wanunue magogo Afrika Kusini kutokana na magogo yalivyo ghali hapa, lakini wao hawavuni misitu yao, hiyo si rasilimali ya Watanzania? Iweje leo Tanzania haina takwimu ya magogo haya yanayotoka Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wanaotoka Mkoa wa Mara, hivi leo hawajui kwamba, kuna ng'ombe wanaotoka Mkoa wa Mara wanauzwa nchi za jirani wala hawataki kununua nyama Tanzania, wananua ng'ombe? Leo Tanzania tuseme hatujui idadi ya ng'ombe wanaouzwa nchi za jirani? Hizo si rasilimali za Tanzania na wanafanya hivyo kwa madhumuni ya kupata ngozi na vifaa vingine? Leo Wizara ya Fedha inaposema hawajui na hawana takwimu, ni aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo halitoshi, hivyo viwanda vya mafuta hapa nchini ambavyo vina malighafi ni hiyo Alizeti inayozalishwa hapa nchini. Kwa sababu ya tatizo la *COMESA* hivi leo Wizara ya Fedha na Uchumi haijui kwamba, mafuta hayo yanapitia nchi jirani kwa sababu ya matatizo ya *COMESA* na yanauzwa? Hiyo Alizeti ni raslimali ya nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo matatizo, mimi *personally* namheshimu sana Waziri wa Fedha, nawaheshimu sana Manaibu Waziri wa Fedha tena ni Swahibu zangu wakubwa lakini wakati mwingine *call a spade a spade* na hii kuoneana haya ndiyo inayotufikisha mbali, kitendo hiki mimi nathubutu kusema wajiuzulu kama hawana takwimu hizi, haiwezekani ni kitendo cha aibu.*(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ulikuwa ni utangulizi. Katika ukurasa wa 41 na 42 wa hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, alizungumzia suala la Wizara ya Nishati na Madini ambayo kwa mwaka wa fedha uliopita ilipangiwa bilioni 378.8 lakini kwa mwaka huu imepangiwa bilioni 285.5 kwa maana kuna upungufu wa asilimia 24.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoudhi pamoja na Kilimo Kwanza na Wizara tulizozipa kipaumbele, lakini tuna hakika Wizara zote hizo mafanikio yake kwanza kwa kupatikana umeme na isitoshe sababu zilizotolewa na Mheshimiwa Waziri, za kupunguzwa na hakuna malipo tena tumemaliza Mikataba ya Dowans, Agreco na Alston. Ni kweli, hizo kampuni Tatu hizo, ambazo zilikuwa na mikataba ya kifisadi ya kuifilisi nchi na kuwapa mzigo wananchi zilikuwa zinapokea *capacity charge* ya bilioni 104 kwa mwaka na pesa hapa iliyopungua ni bilioni 99 na kitu, kufikia angalau bajeti ya mwaka jana, kwa hiyo leo wakati wanatoa sababu hizo, mtu anaweza akajiuliza, hivyo pesa hizo zimepunguzwa hapo tulipokuwa na mikataba hii fedha hiyo ilikuwa inapatikana, leo mikataba haipo fedha haipatikani, kulikoni na kwa sababu gani? Wakati huo Serikali ilikuwa inazipata wapi na leo kwa nini wasizipate?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *Power System Master Plan* ya *TANESCO* na *Financial Recovery Programme*, *TANESCO* inahitaji fedha nyingi sana, zaidi ya bilioni 300 lakini leo, Wizara hii ambayo *TANESCO* iko katika Wizara ya Nishati na Madini, imepunguziwa hela. Ikiwa utakwenda kwenye hiki kitabu cha *Volume Two* uende ukaangalie *programme Ten* ya Wizara zote ambayo utafiti mdogo nimefanya huu hapa, utaona pesa iliyotengwa kwa usafiri wa ndani na usafiri wa nje ya nchi, ni pesa nyingi sana na imefikia idadi kubwa sana, imefikia zaidi ya bilioni 34.6 katika Wizara zote. Lakini kutenga fedha ya kuisaidia Wizara ya Nishati na Madini hasa katika kuisaidia *TANESCO* hazipatikani, ikiwa tuliweza kufunga mikanda mwaka 1978 ambayo haikufunguka mpaka leo, kwa nini tushindwe kupunguza hizi safari tukaweza kuisaidia

Wizara nyingine? Ni mambo ambayo kidogo yanatia aibu na yanatia walakini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande huohuo, katika ukurasa wa 44 na ukiunganisha na hotuba ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 10, mwezi wa Sita, inaonekana kuna fedha itakayokopeshwa *ARTUMUS*, ni suala zuri na la msingi *ARTUMUS* kupata hela, lakini kwa nini Serikali inasahau? Katika bajeti niliyosoma hapa ya Kambi ya Upinzani mwaka 2007/2008, tuliikumbusha Serikali namna gani ya kuongeza mapato yake kwa haya makampuni yanayofanya utafiti wa mafuta na gesi na katika mikataba hii ya *PSA* (*Production Sharing Agreement*). Tunajua Serikali imepewa asilimia 5 mpaka 20 ya kununua hisa ya kujiongezea mapato, Serikali inunue hisa katika miradi ya gesi ya Songosongo na Mnazi Bay, sasa leo ni kwa nini Serikali hii hii kweli inajua *ARTUMUS* wana matatizo, ni kwa nini wawakopeshe wasinunue hisa? Wakati tunajua zinahitajika si chini ya bilioni 35 katika miradi ya Songosongo na Mnazi Bay wa *ARTUMUS*? Hivi leo kwa nini tukopeshe? Ni vitu ambavyo kidogo vinatia mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande huo huo, *STAMICO* ilipeleka maombi Wizara ya Fedha, kutaka kibali cha kukopa *NBC* kwa ajili ya kununua mitambo ya kuchoronga, mpaka leo tangia mwaka 2007 kibali hicho hawajapata. Wizara ya Fedha kulikoni, *STAMICO* wanajiendesha wenyewe kwa nini kisitolewe kibali? Lakini leo tuko tayari kuwafidia watu ambao wamekula hasara katika mtikisiko wa dunia, *STAMICO* kuwapa kibali tu cha kukopa NBC tunashindwa, kulikoni Wizara ya fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine na *time* inakuwa ni ndogo hapa katika ukurasa wa kwanza wa bajeti hii, Mheshimiwa Waziri, alizishukuru Taasisi za Serikali, akashukuru Taasisi nyingine zisizokuwa za Serikali, akawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kuchangia mpango wa bajeti, na mimi nakubali lakini nataka nitoe angalizo kwamba, *BOT* walikuja wakatoa semina kwa Wabunge na semina ile tulipopewa kwa wakati ule wote tunajua kwamba, tuliambiwa mtikisiko wa uchumi duniani hautatuathiri namna hii, athari ndogo sana, kwa ujumla tulikuwa hatuna tatizo. Kwa hivyo, michango yetu Wabunge katika bajeti ikaja katika kiangalizo hicho. Wakati huo katika taarifa za fedha walisema kwamba uchumi wetu unakua kwa asilimia 7.4 ukilinganisha na mwaka 2007 ulivyokuwa kwa asilimia 7.1, kwa maana hiyo kweli Waheshimiwa Wabunge, tulichangia lakini, *BOT* haohao au Wizara ya Fedha hiyohiyo, wataalamu haohao kuna ripoti nyingine ambayo ndiyo wamempa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Rais alipohutubia Wazee wa Dodoma na Wabunge juzi tarehe 10 Juni, mambo yamekuwa mengine, mtikisiko huu utatuathiri vibaya sana na bajeti yetu hii yote imeathirika kwa sababu ya mtikisiko wa dunia. Hivyo si ni Wachumi walewale waliotushauri sisi, leo kulikoni? Ikiwa uchumi unakua kwa asilimia 7.4 lakini baadaye tunakuja kuambiwa kwamba makusanyo safari hii katika bajeti ya mwaka uliopita yatapungua kwa silimia 10, kinachoshangaza hapa tujiulize kulikoni, uchumi unakua mapato yatapungua kwa asilimia 10, hivyo pana kitu gani Wachumi hawa wanavyotueleza, nini kinaendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda unasonga mbele, labda nilikuwa na angalizo moja la mwisho kwamba wale *STAMICO* pia kuna madai yao ya zile milioni

171 na mpaka sasa hivi Wizara ya Fedha inatathimini na muda unakua mrefu, mimi ninataka Waziri atakapokuja kujumuisha atueleze hiyo tathmini wataifanya kwa muda gani ili hawa watu na wao wapate haki yao na wakati Wizara yako inajua vizuri namna gani wakifanikiwa hili wataweza kutengeneza mizania yao (*balance sheet*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Mnyaa kwa mchango wake, ninakupongeza Mheshimiwa Mnyaa.

Kabla sijasitisha shughuli hizi, Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo moja kutoka Mkurugenzi wa Idara ya Shughuli za Bunge, ameniomba niwaarifu kwamba, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi wamewasilisha Ofisi ya Bunge, ukurasa Namba 296 ambao ulikosekana kwenye kitabu cha pili cha Makadirio ya Fedha za Serikali, (yaani *Volume Two* ya *Estimates of Public Expenditures*). Hivyo ukurasa huo wa 296 utagawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge hivi punde, tutaugawa kipindi cha jioni tutakapokuwa tumerudi hapa ndani. Kwa hiyo, meza yangu imepokea ukurasa huo wa 296 pamoja na tangazo hili kutoka kwenye Ofisi ya Katibu wa Bunge.

Labda tu nichukue nafasi hii nitangaze msemaji wetu wa kwanza tutakaporudi saa 11 jioni atakuwa Mheshimiwa Joyce Machimu. Kwa hiyo, ninamuomba Mheshimiwa Joyce Machimu ajiandae ili achukue nafasi hiyo ya kwanza kipindi cha jioni na wengine tutaendelea nao kwa mujibu wa orodha itakavyokuwa imepangwa.

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru sana kwa ushirikiano mzuri toka kipindi cha asubuhi cha maswali na majibu, basi sasa nachukua nafasi hii kusitisha shughuli hizi za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06:56 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Saa 11: 00 Jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano na kama mlivyotangaziwa pale asubuhi, tutaanza na Mheshimiwa Joyce Machimu na atafutiwa na Mheshimiwa Eustace Katagira na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi ajiandae.

Mheshimiwa Joyce Machimu Karibu!

**MHE. JOYCE N. MACHIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuzungumza machache kuhusu dira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, niipongeze Serikali ya CCM jinsi inavyojitahidi kujali maeneo yote ya kijamii na hii ni kwa vile inaye kiongozi mahiri na makini, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na washauri wake bila kumsahau Mama Salma Kikwete. Nasema abarikiwe sana ili aweze kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hatua iliyochukuliwa na Serikali kufidia upungufu uliojitokeza kutokana na msukosuko wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali nia yake ni nzuri kabisa na hasa kuwajali wawekezaji wetu wakiwemo pamoja na wanunuzi wa Pamba. Mimi naomba nizungumzie wanunuzi wa Pamba. Nia ya Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla ni nzuri ili wananchi wake waendelee kuuza mazao yao angalau hata kwa ile bei ambayo ipo kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha kusikitisha ni kwamba wanunuzi hawa pamoja na Serikali kuwajali kiasi hiki hivi ninavyoongea katika Halmashauri nyingi nchini zinazonunua mazao ya biashara ushuru wa mazao haujalipwa. Ninazungumzia hasa ushuru wa Pamba na hasa katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa, nijikite zaidi katika Mkoa wa Shinyanga. Kuna wanunuzi wengi ambao wamenunua Pamba lakini uzoefu unaonyesha kwamba wanunuzi hawa wanapotaka mikopo benki wanapewa ni pamoja na gharama zote za uendeshaji, lakini cha ajabu wanakuwa wazito na wanakuwa na kigugumizi kuzilipa Halmashauri ushuru wa Pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni mwa msimu wa mwaka jana, Halmashauri zilitoa kauli kwamba wanunuzi hawa wasipate leseni walipe angalau asilimia kidogo ya ushuru huu wa Pamba.  Lakini Serikali kupitia Waziri wake wa Kilimo ilitoa kauli na kusitisha Halmashauri hizi ziwaache wanunuzi wanunue Pamba bila masharti hatimaye watalipa ushuru. Cha ajabu ushuru haujalipwa na kama unavyojua Halmashauri zetu uwezo wake kimapato si mkubwa sana nikichukulia Halmashauri ninayoishi mimi yaani Halmashauri ya Bariadi kuna milioni karibu 700 hazijalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachotaka kusema kwa nia nzuri ile ile ya Serikali, naomba sasa Serikali iwashauri hawa wanunuzi walipe huu ushuru mara moja kwa vile wamepunguziwa mzigo kulipiwa hayo madeni moja kwa moja banki. Lakini naomba kama kuna uwezekano madeni hayo, sehemu hiyo ya ushuru wa Pamba zilipwe hizi Halmashauri ili ziweze kukidhi miradi yao ambayo sasa hivi bado imekwama kutokana na upungufu wa hizo hela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri hizi, wakulima wameuza Pamba kwa bei ya chini sana lakini wamevumilia, sasa kinachohitajika kwa msimu huu kabla haujaanza Serikali itamke pia kwamba wanunuzi hawa walipe ushuru kabla ya kupewa leseni za kununua Pamba ili wasiendelee kuzikwamisha hizi Halmashauri kupata huo ushuru, ziweze kununua madawati ya shule, ziweze kuendelea kujenga madarasa na wananchi wapate unafuu wa kuchangia shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni tatizo la wakulima na wafugaji. Niombe Serikali kupitia Tume ya Waziri Mkuu iliyoundwa iharakishe kutoa majibu ya ufumbuzi wa tatizo hili lakini wakati huohuo Serikali inapotafakari iangalie tokea enzi za ukoloni na hadi uhuru, hadi hivi tunavyoendelea maeneo yanayotumiwa na wakulima hayaongezeki lakini wananchi wameendelea kuzaana, wanaongezeka, mifugo nayo imeongezeka lakini ardhi iko palepale. Ushauri wangu, naiomba Serikali katika mipango yake kama inataka kweli kuondoa hii adha ya wakulima na wafugaji inayofikia kupoteza maisha ya watu baada ya ugomvi kutokea itoe kipaumbele kwa maeneo yaliyo wazi kuwagawia wafugaji na kuwawekea miundombinu kwa masharti maalumu waweze kuendesha maisha yao kama vile inavyofanya katika Wizara ya Maliasili inafikia mahali inapanua maeneo ya utalii. Kwa hiyo naishauri Serikali ione umuhimu wa kupanua pia maeneo ya wafugaji na wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huohuo Serikali pia izingatie hiyo takwimu kama nilivyosema hapo mwanzoni ili kuweza kuwapa haki yao ya msingi makundi haya mawili kama wazawa wa nchi hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ni elimu. Serikali inapokuwa katika huu mchakato wa bajeti yake iangalie upya Sheria, Kanuni na taratibu za utumishi. Ninasema hivyo kwa sababu katika Halmashauri zetu kumejitokeza tatizo, Walimu wengi sasa hivi hawafundishi, mara tu Serikali ilivyotoa fursa ya kuwaongezea kipato kwa kuwapa mikopo ilikuwa ni nia njema ya Serikali lakini baadhi ya Walimu wamekiuka maadili ya kazi zao, sasa Serikali ifike mahali ilione hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nitoe angalizo kwa Hazina Kuu, Utumishi, kuna kitu ambacho wamekifanya ambacho mimi naona hakina tija, wanawezaje kufunga mikataba ya mikopo na Walimu bila kumuhusisha mdhibiti wa Walimu hawa ambaye ndiye mwajiri ambaye ni Halmashauri? Matokeo yake *payroll* zinapokuja kila mwezi mishahara inakuja *nil*, wamekata huko huko Makao Makuu hata kama Halmashauri inapojiwekea malengo ya kumdhibiti huyu Mwalimu mtoro wa vipindi wanakuta kwenye mshahara wake hakuna kitu. Kwa nini wasingefuata utaratibu kama wa benki nyingine zinavyoweza kukopesha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hii kampuni ya *Bay Port* sielewi ni ya nani, inatuchanganya sana hasa katika Mkoa wetu ambao uko nyuma kielimu, wa Shinyanga imekuwa ni tatizo. Wamewakopesha, wanawakata hukuhuku Makao Makuu, mwajiri hana habari inakuwa ni vigumu huyu Mwalimu kumdhibiti, hana chochote kwenye akaunti yake. Lakini pia Mwalimu anakuwa anafika mahali anabanwa kimaisha, maisha ni magumu sana. Sasa kama Serikali hiyo hiyo imeruhusu hicho kitu na huyo *Bay Port* waliyemuona anafaa mimi nasema hafai, angepitia utaratibu wa kawaida, akafunga mkataba na Halmashauri angalau zikabakia asilimia kidogo kama tunavyopata mikopo katika benki nyingine, unaacha kwa tahadhari lakini sasa hivi Mwalimu huyu anakuwa hana chochote kinachobakia. Hebu niambie tutawafukuza Wakurugenzi wangapi? Tutawafukuza Maafisa Elimu wangapi kwa kushindwa kuwadhibiti hawa Walimu? Kwa hiyo, ninaomba Serikali katika mipango yake ijipange vizuri kila inapotaka kufanya kitu kuangalia kama kitu hicho kina tija katika huduma za maendeleo ya jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, ni kuhusu fedha zinazopelekwa katika Halmashauri. Naiomba Serikali inafahamu kabisa Halmashauri zetu hazina Wataalamu wa kutosha na fedha hizi ni nyingi sana, naomba ufuatiliaji kutoka Serikali Kuu usiachwe. Serikali Kuu isijitoe, ifuatilie na hasa kwa mfano uunganishaji wa Idara kwa mfano Idara ya Ujenzi na Maji, Mifugo na Kilimo, naomba Serikali hili izitenganishe ili hawa watu waweze kujitegemea na mafungu yao yalenge kasma husika na miradi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia harakaharaka. Naishukuru Serikali ya Awamu ya Tatu, kwa mpango wake, wa kuthubutu kusaini mkataba wa mradi wa maji wa Ziwa Victoria na naishukuru Serikali ya Awamu ya Nne kwa kukamilisha mradi huu. Kwa niaba ya wananchi wa Shinyanga na hasa Wanawake ambao mara nyingi ndiyo ambao wamekuwa wanapata shida ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho. Yale mabilioni ya JK mwanzoni yalitoka hayakukaa vizuri, sasa naiomba Serikali ijipange vizuri iyalete tena na yawalenge walengwa ili tuweze kufikia ile azma ya maisha bora kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wanawake wa Shinyanga, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Waheshimiwa Wabunge, nawapenda sana na ninawashukuru kwa kunisikiliza nasema ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joyce Machimu. Sasa namwita Mheshimiwa Eustace O. Katagira atafutiwa na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi na Mheshimiwa Ernest G. Mabina ajiandae.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kuniruhusu na mimi niweze kuchangia hoja hii ya bajeti.

Niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake kwa jinsi walivyoandaa bajeti nzuri na jinsi walivyoiwasilisha hapa Bungeni. Lakini pia niwashukuru siyo kwa kuandaa bajeti peke yake bali niwapongeze na kuwashukuru kwa jinsi walivyoendesha shughuli zote za Wizara nyeti yaani Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa ukaguzi wa ndani. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amependekeza muundo mpya wa ukaguzi wa ndani, muundo huu naona utakuwa wa manufaa makubwa sana. Naelewa kuna aina mbili za ukaguzi yaani za *auditing*, aina moja ambayo tumeizoea ni ya *external auditing* na aina ya pili ni *internal auditing*. *External auditing* sisi katika fani ya *Auditing* huwa tunaiita jina la utani la kusema ni *Post-mortem Auditing* maana yake ni kwamba pesa zinatumika anayefanya mabaya anayafanya kwa mwaka mzima makaratasi yanaandaliwa lakini baada ya kumaliza mwaka wa fedha na baadaye kusubiri mpaka vitabu viandikwe ndipo huyu *External Auditor* anakuja kukagua na kuangalia yapi yalitokea. Kwa kweli, katika utaratibu huu ni kwamba mambo yote ni historia aliyefanya maovu ameshafanya mwaka mzima na yaliyopotea yameshapotea. Lakini si kwamba *external auditing* haina maana,

ina maana yake na ina faida zake lakini hii *internal auditing* ikitumika vizuri inaweza ikazuia maovu kabla hayajaendelea kwa sababu huyu *Internal Auditor* anakuwa katika Shirika lilelile, ana mambo yote siku kwa siku na kwa hiyo ni suala ambalo linaweza likazuia matumizi mabaya ya pesa na upotevu wa mali ya shirika au Idara usiendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kule kuna tatizo moja, chukulia mfano kama Halmashauri, unakuta yule *Internal Auditor* wa pale amepewa kazi na ameajiriwa na anawajibika na anategemea maendeleo yake kwa wale wakubwa wa pale kwa mfano *DED* na Afisa Utumishi na wengine, inakuwa ni vigumu huyu Mkaguzi wa Ndani kuweza kuwadhibiti, kuwashughulikia na ku-*report* mambo yao yote ambayo yanatendeka pale. Sasa katika muundo mpya huu utamfanya huyu Mkaguzi wa Ndani aweze kuwajibika kwa *Supreme Internal Auditor* wa Kitaifa kwa hiyo anakuwa na mamlaka na uhuru wa kuweza kushughulikia masuala yote katika ile Idara bila kuwa na woga kwamba *promotion* yake itabaki nyuma tu na kwamba masurufu yake hatapewa kwa sababu yeye atakuwa anawajibika kwa yule mkubwa wake ambaye ni wa kitaifa. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hilo alilolileta na ninasema liendelee na litumike vizuri ili liweze kuzuia upotevu wa mali za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kwanza. Hii ni kauli mbiu ambayo tumeanza nayo sasa, sina haja ya kulisemea hili sana, kwa sababu kila Mbunge aliyesimama aliliongelea kwa hiyo nadhani halina sababu. Lakini nisisitize tu kwamba, ili tuweze kufanikiwa katika suala hili la kilimo, ili hii kauli mbiu na mikakati tunayoiweka, iweze kuzaa matunda, lazima tuwe na Watendaji, Serikali kwa upande wake itimize yale ambayo inatakiwa kuyafanya na wananchi tutimize yale ambayo tunatakiwa kuyafanya katika msukumo huu wa kilimo kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namaanisha kwamba, kwa mfano kama wako wanaotaka kulima, kulima *on a large scale* wakapata ardhi sasa ni kazi ya Serikali ku-*expedite* ili sasa wapimiwe ardhi yao, wapate hati harakaharaka, ili hii hati pia iwasaidie katika kutumika kama dhamana ili waweze kupata mikopo ya kujipatia mitaji. Lakini pia Serikali ihimize benki zetu ili ziweze kuangalia shughuli za kilimo kwa jicho linalostahili. Mimi naelewa ukija kufanya biashara katika nchi ya watu, lazima uangalie pia *aspirations* zao, usikae kando ukataka kuchuma lakini yale wanayoyapanga na wanayoyafanya ukasema hayakuhusu, benki zilizo hapa ni benki zilizo katika nchi yetu, zinatumia *deposits* zetu. Kwa hiyo, ni muhimu na Serikali iwasukume, iwahimize ili waweze kujumuika na sisi katika kutekeleza yale ambayo tunayapanga na yale ambayo tunapanga yalete maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nipongeza baadhi ya benki kwa mfano Benki ya *CRDB*, imekuwa mstari wa mbele kusaidia kutoa mikopo katika nyanja ya kilimo, nyanja ya ununuzi wa mazao. Nasema waendelee namna hiyo lakini na benki nyingine ziunge mkono ili tusukume mbele maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza pia katika hili kwamba ukiangalia katika *report* ambazo zinatolewa kila robo mwaka na benki hizi, pale chini huwa wanaweka *foot note* moja, jumla ya wafanyakazi. Ninapenda katika kufuatilia hili

tuwaombe benki hizi wakitoa *report* zao za kila mwaka, pale chini watuwekee *foot note* ya kuonyesha kwamba mikopo *percent* gani inakwenda katika fani ya kilimo na mikopo kiasi gani inakwenda katika nyanja nyingine, ili tuweze kufahamu kwamba benki hii iko nasi na benki hii haiko na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa maagizo ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Kyerwa, tatizo la mnyauko wa migomba na kahawa. Kumetokea ugonjwa wa hatari sana katika Wilaya ya Karagwe na pia katika Mkoa mzima wa Kagera. Migomba mikubwa kabisa iliyo-*mature* inaanza kunyauka na kufa harakaharaka. Serikali katika ngazi ya Wilaya imeshafanya jitihada za kutosha, lakini hili tatizo ni sugu sana na ninaomba na nimeagizwa na nimeombwa na wapiga kura wa Wilaya ya Karagwe hususani Jimbo la Kyerwa kwamba niiombe Serikali sasa iweke mkono wake, iweke msukumo wake kusaidia Serikali ngazi ya Wilaya ili suala hili lidhibitiwe haraka na vizuri kabisa, kama halitadhibitiwa, tunakokwenda mbele na si mbali sana, kutakuwa na njaa katika Wilaya ya Karagwe, kutakuwa na umaskini kwa sababu mikahawa itaharibika. Kwa hiyo, tunaomba kabisa Serikali katika ngazi ya Taifa iingilie kati na isaidie katika kudhibiti ugonjwa huu wa mnyauko wa migomba na mikahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme vijijini katika Wilaya ya Karagwe. Serikali imeahidi mara nyingi hata kwa maandishi kwamba itasambaza umeme katika vijiji vya Wilaya ya Karagwe na kuja kuliweka kofia kabisa suala hili, Mheshimiwa Rais, kwa upendo mkubwa alitembelea na kuzunguka katika Wilaya ya Karagwe na kila mahali alipokwenda na nina hakika alikuwa amekuwa *briefed* na Wizara husika, yaani Wizara ya Nishati na Madini, kila alipokwenda, aliwaeleza wananchi na kuahidi kwamba umeme unasambazwa katika vijiji vya Wilaya ya Karagwe. Alikwenda Rwambaizi katika kituo ambako ni kwa mwenzangu Mheshimiwa Blandes akaahidi namna hiyo kwamba umeme unakuja vijijini. Akaenda Murongo, akarudia ahadi yake kwa nia nzuri kabisa, akaenda Kaisho, Isingiro, Nkwenda na Wilayani akawaahidi wananchi kwa upendo mkubwa kwamba umeme unasambazwa vijijini. Naomba sana na wananchi wameniomba sana, nilieleza suala hili kwamba wanasubiri ahadi ya Mheshimiwa Rais itekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie wimbo wangu wa kila mara ninaposimama, huwa ninaongelea kugawanya Wilaya ya Karagwe katika Wilaya mbili. Wilaya ya Karagwe nirudie kusema na nimeagizwa na wapiga kura wangu wa Wilaya ya Jimbo la Kyerwa na Wilaya ya Karagwe nzima, kwamba Wilaya ya Karagwe ni Wilaya kubwa sana na katika hali hii tutabaki nyuma kimaendeleo. Katika Mkoa mzima wa Kagera hakuna Wilaya inayolingana na Wilaya ya Karagwe na unaweza ukaunganisha Wilaya mbili, chukua Wilaya ya Chato na Wilaya ya Misenyi, unganisha hujafikia Wilaya ya Karagwe labda nusu yake. Unganisha Wilaya ya Bukoba Vijijini na Wilaya ya Misenyi, huwezi kufikia ukubwa wa Wilaya ya Karagwe. Tafadhali sana narudia tena, tunaomba Wilaya hii igawanywe ili maendeleo yaweze kusukumwa mbele haraka kwa sababu sasa hivi ukija kwenda kwa Mkuu wa Wilaya kutoka sehemu moja ya Karagwe ni kilomita 150 au120 huduma ziko mbali, usalama uko mbali, *OCD* yuko mbali, Afisa Elimu yuko mbali. Kwa hiyo, narudia ombi la wananchi wa Wilaya ya Karagwe hususani Jimbo la

Kyerwa maombi yao kwamba Wilaya ya Karagwe itengwe tuwe na Wilaya ya Kyerwa ambayo bado itakuwa ni Wilaya kubwa sana na Wilaya ya Karagwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nazidi kukushukuru kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kyerwa na Wilaya ya Karagwe kwa ujumla kwa kuniruhusu nisimame niwasilishe maombi yao na maono yao. Lakini pia niseme kwamba naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Katagira, ahsante kwa kuchangia kisayansi kwa sababu ume-*serve* muda mwingi tu. Sasa namwita Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi atafutiwa na Mheshimiwa Ernest G. Mabina na Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura ajiandae. Mheshimiwa Mporogomyi haonekani na sasa namwita Mheshimiwa Ernest G. Mabina.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hotuba ya Wizara ya Fedha kwa jioni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kutoa shukurani zangu za dhati kwa wananchi wa Tanzania na Waheshimiwa Wabunge wote, Ofisi ya Bunge kwa kuniwezesha kusimamia hapa nikiwa peke yangu nafikiri mlikuwa mnajua kabisa kwamba tulikuwa na mwenzangu hapa lakini Ofisi hii ilinisaidia sana kuweza kushughulikia mazishi ya Mheshimiwa Faustine K. Rwilomba, niwashukuru sana wananchi wote wa Tanzania kwa niaba ya wana-Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwa sababu kulikuwa na mchakato mkubwa katika Wilaya ya Geita, sina budi kuwashukuru Watanzania wote waliotuombea na kukiombea Chama Cha Mapinduzi kikapata Ushindi wa kishindo hasa kwa kuturejeshea mwana-CCM mwenzetu Mheshimiwa Lolensia J. M. Bukwimba ambaye yuko hapa mpaka sasa hivi. Niwashukuru sana wananchi wa Geita na hasa Geita Mjini ambao ilikuwa ni chachu kubwa waliokwenda katika Jimbo la Busanda na kuweza kuleta ushindi mkubwa kama huo, niwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naingia katika suala moja ambalo linatusumbua sana Geita, Geita ni mji mkubwa, kuna watu wengi, kunahitajika kuangaliwa kwa jicho la huruma hasa kwa Mawaziri na Serikali ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa ninavyozungumza Geita haina huduma ya maji safi, maji yake yapo lakini wanatumia visima vifupi, visima ambavyo havitoshelezi mahitaji ya wana Geita. Geita ina watu wengi sana, Jimbo la Geita tu lina watu zaidi ya 500,000, Majimbo yote matatu tuna zaidi ya watu 1,000,000, jifikirie hatuna huduma ya maji. Ukiangalia kuna mradi mkubwa ambao umefunguliwa juzi na Rais unapeleka maji Shinyanga, ni sawasawa na mfugaji, anafuga ng'ombe, anakamua maziwa, watoto wanahitaji kunywa maziwa nyumbani lakini anayapeleka kwa jirani, ni kama sisi kwa Ziwa Victoria, miji yote ambayo iko karibu na Ziwa Victoria haina maji,

ukianzia Geita yenyewe, Misungwi, Magu, Bunda hata kwa ndugu yangu kule Tarime hakuna lakini watu tunasema kwamba watu wa Kanda ya Ziwa mmeshanufaika, mmeshapata maji. Ndugu zanguni, Geita hatuna maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii afanye juu chini kwa sababu tumeshaahidiwa na watu wengi sana kila tukija tunaambiwa tutakapata maji. Ninaimani kabisa Waziri aliyepo sasa hivi kwa umahiri wake na kwa kuwa ni Mwanageita kwa sababu Geita huwa tunasema tuna Wabunge watano, lakini wawili wanatoka Rungwe Mashariki na Rungwe Magharibi, Rungwe Mashariki ndiyo Waziri wa Maji, tunaomba Mwanageita mwenzetu utuletee maji. Bila maji Geita hatutaweza kuielewa Serikali hii, tunaomba sana tupate maji ili tuweze kuendeleza shughuli zetu za ujenzi wa Taifa. *(Makofi)*

Mwaka jana, Mheshimiwa Musalika alichangia hapa akasema tunakunywa maji yaliyo na Zebaki na ni kweli kwa sababu shughuli nyingi za wachimbaji katika Wilaya ya Geita wanatumia Zebaki. Kwa hiyo, maji mengi unakuta yameathiriwa na Zebaki. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, tunakuomba kwa huruma kabisa uliyonayo, uwapatie maji salama Wananchi wa Geita, ambayo yanaweza kuwasaidia katika maisha yao. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme ni tatizo kubwa hivi sasa na ili kuweza kuleta maendeleo tunahitaji umeme. Umeme uliopo Geita hauna nguvu kabisa, tunahitaji umeme wa *Grid* ya Taifa ambao mlisema utaanzia Kakola kuja Geita mpaka Biharamulo kwenda mpaka Karagwe; huu mradi umefikia wapi? Mradi huu ukija utatusaidia sana. Kwanza, unaweza kupunguza gharama za mafuta yanayotumika kwenye Mgodi wa Geita. Umeme ule ukifika hapo, nina uhakika kabisa kwamba, Mgodi wa Geita utatumia umeme ule ule na Wananchi wa Geita watafaidika katika viwanda vikubwa vikubwa kwa kutumia umeme ule. Hadi hivi sasa hatujui umeme uko wapi, tunamwomba Waziri mwenye dhamana ya umeme, aliangalie suala hili ili tuletewe umeme Wana-Geita tuweze kufanya kazi katika hali ya ufanisi.

Vilevile tumeahidiwa Umeme wa MCC, ambao utaanza Kasamwa, utapitia Brela, utaenda Nyang'hwale mpaka Kaluma kwa Mheshimiwa Musalika; mradi huu tunauomba uje haraka. Kuna mradi ambao unaanzia Kakola unakuja Bukoli, Nyarugusu, Katoro kwenda Lwamngasa, huu umeme tunauhitaji. Kuna umeme ambao wamesema utaanzia Geita kwenda Nkome; tunahitaji miradi hii itekelezwe haraka iwezekanavyo ili Wana-Geita waweze kufaidika na suala la umeme. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalotaka kulizungumzia ni la Wakulima wa Pamba. Tumekuwa na matatizo sana kwa wakulima wa pamba, tumewahamasisha kulima pamba, lakini inapoiva au wanapoanza kuvuna, ndiyo tunatangaziwa bei. Ijulikane kwamba, kazi kubwa ya mkulima inaanzia wakati wa kupanda au kulima na wakati wa kupalilia, gharama zile zote wanunuzi au Serikali haizijui. Mpaka sasa Serikali haijatangaza bei, mwaka jana bei ilifikia shilingi 400 mpaka 500, lakini kwa sababu Serikali imesema kwamba, Zao la Pamba hivi sasa halinunuliki, nina imani bei ya pamba inaweza kuteremka. Naiomba Serikali kama ilivyowafidia wafanyabiashara na kama ilivyofidia mabenki, basi na Wakulima wa Pamba wafidiwe bei ile ile ili

wasiathirike na kuamua kuacha kulima Zao la Pamba. Leo hii Zao la Pamba halina bei, lakini kesho linaweza likapata bei likatuokoa katika Pato letu la Taifa. Kwa hiyo, tusidharau Zao la Pamba au tusiwakatishe tamaa wakulima wakashindwa kuendelea kulima pamba kwa sababu bei imekuwa kidogo. Serikali iingilie kati iwasaidie hawa wakulima ili kuleta tija katika eneo letu la Kanda ya Ziwa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tumelizungumza hapa na Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumza ni suala la Bandari yetu ya Dar es Salaam. Bandari hii imekuwa na matatizo sana, tatizo lake kubwa ni hii TICTS; sasa sielewi TICTS maana yake nini? Ninadhani TICTS ni wakala ambao wamewekwa kuweza kupakua makontena na kuyaweka pale ili yaweze kuondoshwa na kwenda sehemu zinazohitajika.

Tatizo lililokuja TICTS sasa hivi, unakuta wanaweka makontena pale wanaacha tu, kwa hiyo, yanakaa kwa muda mrefu wakiwa na lengo lao, yakae muda mrefu ili waje wapate *charge* kubwa kwa kum-*charge* yule ambaye ameleta pale. Haya ni makosa makubwa na ndiyo maana Serikali iliamua kwa makusudi ikasema lazima tuanzishe bandari kavu ili kurahisisha kuyaondoa haya makontena yanayoteremshwa na TICTS yaende moja kwa moja kwenye bandari kavu. TICTS imekuwa na ukiritimba wa hali, imepuuza Kauli ya Waziri Mkuu, imepuuza Kauli ya Rais! Mimi najiuliza huyu TICTS ni nani, ana kiburi kutoka wapi? Hata Waziri Mkuu alisema kwamba, kama kuna uwezekano lazima hii ifutwe. Sasa ninaweza nikachukua hata madaraka ya Mheshimiwa Spika, labda niwahoji Wabunge wanaosema tuifute TICTS waseme ndiyo. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Ndiyooo! (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mabina usiwahoji Wabunge, hiyo ni kazi ya Kiti, endelea kuchangia tu.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunapata machungu kwa masuala kama haya, tunajiuliza tunashindwa tunaanzie wapi. *(Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyoona hata Wabunge wengine wanakubali, kwa hiyo, ujue ni kitu ambacho hakifai. Sasa kama tuliweka mikataba, ndiyo iliyotusababisha sisi wengine tunaathirika na mikataba mibovu. TICTS kuingilia mpaka sasa hivi wanakuwa na ukiritimba wa hali ya juu, tunaiomba Serikali kama kuna uwezekano basi awekewe mshindani mwingine badala ya kukaa peke yake washindane. Bandari kavu hizi zifanye kazi, kwa sababu sasa hivi hazina makontena zimekaa tu. Hawa TICTS wanafanya kazi gani, wanapenda kuweka makontena yao pale ili watoze *storage charge*, baada ya siku 20 sijui dola ngapi hizo; ni pesa za bure wakati kuna bandari kavu ziko wazi; kwa nini wasipeleke kwenye bandari kavu? *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana suala la TICTS tusisubiri wakati wa Wizara ya Miundombinu, tuendelee tu hapa hapa aondoke huyu TICTS. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wamekuwa wakimbizi katika nchi yao. Katika kila hotuba ambayo ninaisikiliza, wanazungumzwa wakulima, wafanyabishara, lakini mfugaji hatajwi popote; tunampeleka wapi huyu? Nina uhakika kabisa, sisi maeneo ya Geita wafugaji ndiyo wachangiaji wazuri kwenye suala la kilimo, hata sehemu nyingine wafugaji ndiyo wakarimu. Wageni wakija, lazima utakimbia kwa mfugaji, lakini leo masuala mengine yanapokuja mfugaji anawekwa pembeni. *(Makofi*)

Ninaomba kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, Geita tuna mapori na misitu, ambayo haina hata wanyama imebaki miti tu, basi wafugaji wa Wilaya ya Geita waruhusiwe wakachungie mle. Kama wakulima watabaki katika sehemu zao, basi wale wafugaji waende kwenye misitu ile ili ng'ombe waweze kupata malisho ya kutosha.

Nje ya pale, unakuta kunakuwa na ugomvi kati ya mkulima na mfugaji, lakini ninaiomba Serikali kila inapoweza kuangalia katika bajeti yake, iliangalie suala kubwa la mfugaji ili aweze kuongeza tija katika maisha yake. Tunaachwa tu hivi hivi, ndiyo maana unakuta mtu unamcheka lakini usimcheke kwa sababu unapomcheka hawezi kuendelea na unazidi kumkandamiza. Naomba sana Serikali iangalie suala la mfugaji kwani ndiye kiongozi. Tuliomo humu wengi ni watoto wa wafugaji, tangu tukiwa tumboni tumeanza kupata lishe ya wafugaji. Kwa hiyo, unapotoka pale unakuta ni mtu mwenye afya. Jaribu kuangalia watoto wa wafugaji; waangalie akina Mheshimiwa Lekule Laizer na Mheshimiwa Msindai. *(Makofi/kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mabina ahsante lakini kanuni hazituruhusu kuahirisha shughuli za Bunge kwa hiyo kazi ya kuhoji haikuwa ya kwako. Sasa namwita Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, atafuatiwa na Mheshimiwa Alhaji Dkt. Juma Ngasongwa na Mheshimiwa Archt. Fuya Kimbita ajiandae.

**MHE. MTUTURA ABDALLAH MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana ingawa taarifa hii ya kuchangia imekuja ghafla mno, kwa sababu sikutarajia kuchangia hivi sasa, lakini hata hivyo, kwa kuwa nilikuwa nimekwishajiandaa hakuna kitakachoharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nawashukuru na kuwapongeza sana Waziri, Naibu wake na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha, kwa kutuletea bajeti hii nzuri, ambayo inatuletea matumaini ya siku za usoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, vilevile nitoe shukrani kwa Serikali kwa kutukumbuka Wananchi wa Tunduru safari hii. Tulikuwa tumeomba fedha kwa ajili ya kujenga Daraja la Kalulu, tunashukuru tumepata fedha hizo. Vilevile tunashukuru kwa kupata fedha kwa ajili ya kufungua barabara itokayo Lukumbule kwenda Kijiji cha Tulingane. Kwa hiyo ni matumaini ya Wananchi wa Tunduru kwamba, fedha hizi zitawafikia haraka iwezekanavyo ili wananchi hawa ambao walikuwa kisiwani waweze kukomboka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajikita zaidi katika masuala ya Tunduru, labda nianze kuchangia bajeti yetu. Nitakuwa silitendei haki taifa langu, kama sitazungumzia utendaji ulioshuka wa Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Dar es Salaam kama ingeweza kutumika vizuri, ninaamini ingeweza kuchangia Pato la Taifa si chini ya asilimia 40, lakini nasikitika hata nusu ya hiyo haipatikani. Bandari kulikoni; wakati kila Mbunge hapa aliyechangia anathibitisha kwamba, kama bandari ingeweza kutumiwa vizuri kama wanavyotumia nchi za wenzetu kwa mfano Kenya, Msumbiji na Afrika ya Kusini, Pato la Taifa lingekuwa kubwa sana kutokana na mchango wa bandari zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitasita kugusia upungufu wa ufanisi katika Bandari ya Mtwara wala sitasita kusema kwamba, TICTS inachangia si chini ya asilimia 70 ingawa kuna sababu nyingi zimetolewa kwamba, miundombinu ni mibovu lakini tunasema ule msongamano unaoletwa pale na yale makasha, TICTS ina mchango mkubwa na leo nitatoa ushahidi hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya serikali kubaini kwamba, kuna msongamano mkubwa wa makasha pale bandarini kiasi kwamba, TICTS wanalazimika kubebesha yale makasha mpaka kufikia sita na vyombo ambavyo vinatumika katika kubebesha yale makasha ni hafifu, ilishawishi baadhi ya wawekezaji wa ndani kuanzisha *dry ports* zinazoitwa ICD, wananchi wengi wakakopa kwenye mabenki, wakanunua vipande vya ardhi na sote tunafahamu ardhi ilivyo ghali Dar es Salaam; walinunua vipande vile vya ardhi wakiwa na matumaini kwamba, vitaweza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa niliyonayo hapa inaonesha ni namna gani zile *dry ports* hazitumiki, licha ya kwamba, kuna msongamano mkubwa sana katika Bandari ya Dar es Salaam. Taarifa hii ni ya tarehe 2, Juni 2009, inaonesha makasha yaliyokuwepo bandarini siku hiyo ni 8210, wakati huo huo hizi ICDs za watu binafsi kwa mfano ya *TRH* ina *capacity* ya makasha 2500, *MOFET* wana *capacity* ya makasha 1000, *AMI* wana *capacity* ya makasha 750, *MCC* wana *capacity* ya makasha 750 na *DICD capacity* yao ni makasha 4000; jumla ni makasha 5400. Sasa *ICDs* hizi kama zingeweza kutumika vizuri, zingeweza kuleta unafuu katika bandari na eneo lile ambalo linahifadhiwa makasha 8200 lingeweza kuhifadhi makasha 3000, lakini *TICTS* akiambiwa atumie zile *ICD*s hataki. Kwa taarifa ambazo tumezipata hivi karibuni, ameingia mkataba na kampuni moja tu *TRH*. Zile *ICDs* nyingine anasema watatafuta namna wanayoielewa wao, kutafuta wapi pa kuhifadhia makasha. Sasa tunajiuliza, hivi jeuri hii *TICTS* anaitoa wapi wakati serikali imehimiza watu wanunue ardhi, waanzishe *ICDs* ili kupunguza msongamno wa makasha pale bandarini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa cha kushangaza zaidi, huyu *TICTS* ameongezewa gharama za kuhifadhi yale makasha *(storage charges)*, mara mbili zaidi. Matumani ya TPA kuongeza ile gharama ni ku-*motivate* watu wachukue yale makasha haraka, matokeo yake yeye anayadhibiti pale na mtu anaweza akawa amelipia kuchukua makasha yake,

lakini hayachukui siku ambayo ametarajia eti tu kwa sababu hana vifaa vya kutosha kuweza kuchambua lile kasha kama liko chini. Vifaa vyake havitoshi na hata hivyo makubaliano yaliwepo kwamba, endapo mfanyabiashara amelipia kasha lake na anahitaji kulichukua siku hiyo hiyo lakini *TICTS* wakashindwa, basi inabidi *TICTS* amlipe yule mfanyabiashara; *TICTS* amekataa kwa sababu anasema hana vifaa vya kutosha na pia hana nafasi ya kutosha; sasa kama huna nafasi ya kutosha kwa nini usitumie zile *ICDs* za wafanyabiashara wengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo, kama *TICTS* ataachiwa kuendesha shughuli hizi kama anavyotaka yeye, nchi yetu tunaipeleka mahali pasipotakiwa. Sitasita kusema kwamba, siku za nyuma tulishuhudia hapa watu wamekamatwa wakiwa na vipande vya sabuni, wakaitwa wahujumu wa uchumi, wakahifadhiwa kule walikohifadhiwa, wamekaa rumande miaka chungu nzima, leo *TICTS* anahujumu uchumi wa mabilioni kwa nchi yetu, lakini haonekani kama ni mhujumu wa uchumi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida watoto wanapopeleka kilio kwa baba na vilio hivi vikiwa vingi, baba ana kawaida ya kutoelewa kilio kipi kina umuhimu. Sisi Wabunge, tunapeleka kilio hiki kwa Serikali, tunajua vilio ni vingi lakini tunaomba kilio hiki cha *TICTS* kionekane kwamba ni muhimu kuliko vilio vingine vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inapata athari gani kwa kuendelea kumvumilia huyu *TICTS*? Kwanza, kuporomoka kwa Pato la Taifa. Vilevile meli nyingi zinakimbia nchi yetu. Sasa hivi mizigo mingi ya Zambia inapitia Msumbiji na Afrika Kusini. Congo nao wanajiandaa kupitishia mali zao Zambia ziende Msumbiji au Afrika Kusini. Vilevile hali hii inapandisha gharama za maisha, kwa sababu gharama za uchukuzi zinapanda, kwa hiyo anayeathirika pale ni mnyonge, mlaji wa mwisho. Vyakula na madawa yanapanda gharama, kwa sababu makasha yanakaa muda mrefu bandarini bila kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo, tunaiomba sana Serikali iliangalie hili kwa upeo mkubwa, kwa sababu tupo katika vita ya kupamba na umaskini; sasa kama vita hii wachache watakuwa wanatukwaza, Watanzania hatuwezi kuvumilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu alithibitisha Bungeni kwamba, *TICTS* wameshindwa. *TPA* ambaye ni mwajiri naye amethibitisha na aliwahi kuandika barua ya kusudio la kusitisha mkataba, lakini bado naona kuna kusuasua; sielewi kusuasua huku kunatokea wapi? Tunasema *kill one to save many*, *TICTS* ang'olewe hata kama kuna gharama za kufidia, siamini kama tutalazimika kulipa gharama kwa sababu yeye mwenyewe ameshindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, kwa hiyo, najua vigezo vilivyowekwa na yeye ameshindwa wapi; tutumie nafasi hiyo kuhakikisha kwamba, *TICTS* ananyang'anywa ule mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi sasa Tunduru. Tunduru tuna vivutio vingi vya utalii, naomba nichukue fursa hii kwa sababu sielewi muda umebaki kiasi gani, nimualike

Waziri wa Maliasili na Utalii aje Tunduru ili tumtembeze kwenye vivutio mbalimbali vya utalii, ambavyo ni vya aina yake Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tunduru kuna jiwe moja kubwa ambalo halijawahi kuonekana Afrika Mashariki na ya Kati. Jiwe hili kama ndugu zetu hawa wanaorekodi nyimbo watafanikiwa kufika pale, watanufaika sana kwa sababu watauza sana nyimbo. Sasa hivi tumekuwa tukiona picha nyingi sana, mawe yaliyobebana, sisi tunayo mengi zaidi, kwa hiyo, tunaomba Waziri siku moja atembelee Tunduru ili tumwoneshe vivutio vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono azma ya Serikali kwa tamko lake la Kilimo Kwanza na sisi Tunduru tumejipanga, hatujasubiri hiyo Kampeni ya Kilimo Kwanza; tumeshaanza na hivi sasa tumeshashika masoko ya mchele kule Kusini. Kwa hiyo, tunachosubiri ni uwezeshaji tu wa Serikali tuweze kuzalisha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tunduru tuna mchele fulani ambao watu wa maeneo mengine wameubatiza jina wanasema Nitalima Wangu kutokana na ubora wake. Tunaiomba serikali iuangalie kwa makini sana na ituwezeshe; haya matrekta ambayo yataagizwa na Serikali basi kabla hayajaenda sehemu nyingine yapelekwe Tunduru ili Tunduru iwe *centre* ya uzalishaji wa mchele Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mtutura, pamoja na kushtukiziwa tu, lakini naona muda haukutoshi unahitaji muda wa ziada. Sasa namwita Mheshimiwa Alhaji Dkt. Juma Ngasongwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Fuya Kimbita na Mheshimiwa Blandes ajiandae.

**MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie katika Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka kuchangia kama mambo matano hivi, lakini itategemea muda. La kwanza, nilipenda nichangie suala la mpango. Namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwanza, tunatoka kumoja Morogoro, nampongeza kwa kazi nzuri na ngumu ya kuandaa bajeti. Bajeti inaandaliwa katika mazingira magumu ya msukosuko na mtikisiko wa uchumi duniani, ambao hata sisi Tanzania umetuathiri. Pili, nampongeza zaidi kwa kuwa amefikia kiwango kile cha tirioni 9.5; sio kazi ndogo. Hongereni sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Uchumi na Wataalam wote, ambao wameshiriki kazi hii ambayo ni ngumu lakini wamejitahidi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuzungumzia mambo ya mpango kwanza na vipaumbele vile viko katika ukurasa wa 40 mpaka wa 41 katika Kitabu cha Bajeti, maana Waziri ametoa vitabu viwili; cha Hali ya Uchumi na Bajeti, mimi nitazungumzia cha Bajeti. Kwanza, nizungumzie kidogo tu juu ya umuhimu wa kupanga; kwa nini

tunapanga? Tunapanga kwa sababu tuna mahitaji mengi na rasilimali za kutosheleza mahitaji yote ni ndogo sana; kwa hiyo, lazima upange kwa tafsiri kwamba, lazima utakuwa na vipaumbele vichache ili viweze kupata rasilimali ambayo itawezesha kuchochea uchumi au kuwezesha uchumi kukua. Mwalimu Nyerere, alitufundisha vizuri alisema kupanga ni kuchagua na kuchagua maana yake uende mbele sio uzunguke zunguke tu katika *vicious circle* au urudi nyuma. Tafsiri hii ya kupanga ni muhimu kwa sababu ya hicho nilichokisema hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie vipaumbele; vipaumbele vilivyopo katika ukurasa ule ni sita, ingawa Waziri hakutusaidia sana kwa kutuwekea *percentage* ya *allocation* alizozifanya kwa kutengea pesa. Mtu yeyote anaweza kufanya hesabu na mimi nimefanya hesabu kidogo kulinganisha tu hivi vipaumbele sita viko vipi. Cha kwanza kile ambacho ni cha elimu, shilingi trilioni 1.7 ni sawa sawa na asilimia 18.3; Miundombinu shilingi trilioni moja sawasawa na asilimia 11.5, Afya shilingi bilioni 963 sawasawa na asilimia 10; Kilimo ingawa ni Kilimo Kwanza lakini ni namba nne ina shilingi bilioni 666.9 ambayo ni sawasawa na asilimia saba; Maji ambayo imetengewa shilingi bilioni 347.3 ni sawa sawa na asilimia 3.7, wakati Nishati na Madini shilingi bilioni 285 imetengewa kwa asilimia tatu.

Sasa nikipiga hesabu zote hizi napata asilimia 53.6, sipati asilimia 64 kama ilivyo kwenye Kitabu cha Bajeti katika ukurasa ule wa 41, lakini ile *figure* ya trilioni 5.1 naipata na ukiipigia hesabu inakuja asilimia 53.6 haiji 64 ya triloni 9.5 shilingi. Labda hii inaweza kuwa ni *typing error.* Ninachosema, muhimu katika vipaumbele hivi hapa ni vitatu ndiyo maana hivi vyote kuna asilimia 10 kwenda juu, ndio vipaumbele vyenyewe. Hivi vingine vya asilimia saba kwa Kilimo na Maji asilimia 3.7 na Nishati asilimia 3.0, kuviita vipaumbele nashangaa kidogo. Hii ndiyo hoja ninayotaka kuitilia mkazo kwamba, ningekuwa napanga ningesema elimu ndiyo ingepata namba moja; kwa nini? Watu wote waliofanya maendeleo duniani hasa Nchi za Asia, *The Tiger Economies*, kitu cha kwanza walichotilia mkazo ni elimu, kwa sababu suala la afya ukiwa na watu waliosoma watajua mambo mazuri ya kufanya ili kuepukana na magonjwa. Kwa hiyo, elimu ni namba moja ili kuwawezesha watu kujua namna ya kupambana na mazingira na pili unahitaji ujuzi ili ufanye maendeleo. Katika hali ya sasa, bila ya kuwa na ujuzi huwezi kufanya maendeleo yanayostahili. Kwa hiyo, hili la elimu kuwa kipaumbele cha kwanza, nasema ni la muhimu sana na ninaliunga mkono.

La pili, ambalo ningeliunga mkono na kulitilia mkazo ni miundombinu; kwa nini? Leo asubuhi Mheshimiwa Kigoda, amezungumzia juu ya *economic history,* ambayo imeonesha zile nchi zilizopiga maendeleo zilifanya masharti mawili makubwa. La kwanza ni kuwa na Serikali ya nchi nzima *(National State);* lazima uwe na Serikali inayosimamia mambo ya nchi nzima. Pili, lazima uwe na Soko la Kitaifa; kwa nini? Soko la Kitaifa linakuwezesha kuunda mazingira ya uzalishaji, lakini pia na uuzaji wa bidhaa. Bila hiyo, ndiyo maana sisi tunakuwa na njaa Shinyanga, lakini tuna mahindi kibao Rukwa ambayo hayawezi kwenda Shinyanga. Utapelekaje huna barabara wala reli?

Kwa hiyo, tukitaka kujenga uchumi wa sasa lazima suala la miundombinu liwe ni nambari moja; lazima utengeneze barabara, utengeneze reli. Lazima tutengeneze reli kwa sababu ni njia rahisi zaidi kusafirisha bidhaa kuliko barabara. Nchi nyingine wanatengeneza mabomba ya mafuta kuogopa kusafirisha mafuta kwa malori; kwanza, yanaharibu barabara lakini pia ni gharama nyingine za kijamii kama ajali na kadhalika.

Kwa hiyo, nasema hili la pili la miundombinu ni kubwa na liwekewe fedha za kutosha zaidi. Ndiyo maana hapa naweza kusema kwamba, mimi siogopi kwenda kukopa. Kwanza, Mheshimiwa Rais amesema humu, ngoja niwasomeeni maneno mazuri sana kwenye hotuba yake ya tarehe 12 Juni, 2009, ukurasa wa nne; alikuwa anazichambua Serikali hizi za wakubwa zilivyojiingiza katika kusaidia haya makampuni yaliyopata matatizo. Rais anasema hivi: "Hali hii imelazimisha Serikali za nchi hizo kuingilia kati na kutumia fedha za Serikali kuokoa makampuni binafsi kinyume kabisa na falsafa ya uchumi huria na soko huria."

Mimi ningesema, uchumi wa soko na vile vile Serikali za nchi hizo zimelazimika kukopa fedha nyingi kwa ajili ya miradi mingi mikubwa ili kuchochea shughuli za kiuchumi za nchi hizo. Sasa hii ndio *essence* ya Rais, anasema kwanza uyaokoe makampuni makubwa kwa sababu ndiyo yanayotoa ajira na unahitaji ajira ili watu wapate kipato waweze kuishi vizuri. Pili, lazima ujenge misingi ya kuchochea uchumi na kitu cha kwanza cha kuchochea uchumi katika nchi yetu ni miundombinu na pili ni kilimo. Kilimo kwanza katika *level* mbili huwezi kuwa na kwanza ya chakula na pili ya mambo mengine ya mapato ya wakulima na taifa. Kuna wakati fulani nilijibu swali hapa la nyongeza la Mheshimiwa Mhagama, ambalo lilikuwa linahusu mfumko wa bei. Nikasema bwana mfumko wa bei matatizo zaidi ni chakula. Jamaa hapa wakabishabisha kidogo, wakasema hapana, lakini baada ya miezi mitatu, mine, hivi tukakuta chakula ni tatizo. Kwa hiyo, mfumko wa bei wa chakula ni muhimu sana kuuzuia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili nilitaka nilieleze hivi na sina muda zaidi, lakini nilitaka kulisemea la kilimo. Nimefarijika sana kuhusu vipaumbele vile vya mikoa sita; Kigoma, Mbeya, Rukwa, Iringa, Ruvuma na Morogoro. Mimi nasema hata katika hizi lazima upange vipaumbele. Rais ameshatoa maelekezo kwamba, Mkoa wa Morogoro uwe na mradi wa kuzalisha chakula, ndiyo hiyo ghala ya nchi. Pale kuna mambo mawili makubwa; kwanza kilimo cha umwagiliaji, lakini pili ni zana za kisasa na hili lipo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, mambo mawili haya ni muhimu sana; la ujenzi wa kisasa na uwezeshaji wananchi kiuchumi. Kwa hiyo, nasema *focus* inatakiwa iwe nzuri. Ahsante, naona wenzangu wananikumbusha, bado dakika tano ngoja niendelee.

Tatu, nitaliruka hili la *stimulus package,* maana tayari nimeshalisemea kwa kifupi, nataka nizungumzie bajeti ya maendeleo. Mimi siogopi misaada; lazima tuipate kwa sababu katika dunia tumejifunza watu wengi wamepata misaada, kwa mfano, Ujerumani ilipata ile *Marshal Plan* ndiyo ikafanya iendelee haraka. Ireland pia imepata msaada kutoka *European Union* ndiyo maana wakaendelea haraka. Hoja hapa; unatumia fedha za msaada namna gani? Mimi nashauri fedha za misaada zitumike kwa kuchochea uchumi na uchumi wetu hapa namba moja ni kilimo na nambari mbili lazima tutilie

mkazo viwanda, mimi nasikitika sana kuona baadhi ya viwanda vinafungwa. Wengine wamefanya *package* ya kuvifufua viwanda ili kuongeza ajira, lakini pili kwa ajili ya *value addition* lazima ufanye jambo hili. Kwa hiyo, hili nataka kulisema kwa ufupi namna hiyo, maana hatuna muda tena.

Nne, nataka kuzungumzia suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi, naona tunalegalega kidogo na hatutakiwi kulegalega kwa sababu hili ni namba mbili katika Ilani ya chama chetu. Ilani hii ukiitazama yapo mambo mawili tu; kujenga uchumi wa kisasa na uwezeshaji kiuchumi wananchi. Sasa ni hii fedha tunayoiita maarufu mabilioni ya JK sawa, lakini ile sio yenyewe, yenyewe ni kuanzisha Mfuko wa Uwezeshaji wa Taifa au wengine wanauita *Mwananchi Economic Empowerment Fund* na wengine wanauita *National Economic Empowerment Fund,* pale ndipo tunatakiwa tupawekee fedha za kutosha ili kusaidia ujenzi wa mitaji kwa ajili ya Watanzania hasa Watanzania kama Juma Ngasongwa hivi, Martha Mlata, Lucy Mayenga, hawa hawawezi kupata mitaji mingine haiwezekani. Benki hizi zinakopesha watu wachache tu, tena wengi zaidi watakuwa wanafanana na sisemi, maana nikisema …

**WABUNGE FULANI:** Sema!

**MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA:** Sisi hatuwezi. Kwa hiyo, mfuko ule lazima tuuanzishe na una msingi na maagizo ya Rais ya kujenga *the middle class*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano iko Malaysia wamefanya hivyo, India wamefanya hivyo, South Korea wamefanya hivyo, Wachina wanafanya hivyo na South Africa wanafanya ingawa kule wanaitwa *Black Economic Empowerment Fund*. Hili jambo lazima tulifanye na tusilionee haya, kwa sababu litawezesha wananchi wengi kupata mitaji na tutapunguza EPA, maana watu walikosa fedha za halali wakaingia kwenye EPA, sasa kama hivyo mtafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni pensheni. Mimi nakubali kabisa kwamba, mmefanya vizuri kuingeza lakini nimekwenda pale Sukari House kuna mpiga kura wangu mmoja ameniambia mzee sasa nina miezi sita hapa sipati pensheni yangu. Nilipokwenda pale panatisha, kuna wazee pale na magongo, akina mama na wanaume, lakini hawapati pensheni zao wanasumbuliwa sana. Pale pako ovyo kabisa na mimi naogopa kwa sababu nakaribia kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tungependa tuendelee kukusikia lakini muda umemalizika na mchango wako ulikuwa mzuri tu, sasa namwita Mhandisi Majengo pekee tuliyonaye humu, Architect Fuya Kimbita.

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia nafasi jioni hii. Nakushukuru kwa kutambua Architect pekee ndani ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia tena wakati huu kujadili bajeti muhimu kwa ajili ya Wananchi wetu wa Tanzania. Kwa masikitiko, nianze kuwapa pole ndugu zangu, Wananchi wenzangu wa Wilaya ya Hai, kwa hali ya hewa iliyobadilika baada ya kilimo kushamiri vizuri, lakini hapo hapo katikati mvua zimekatika. Tunazidi kumwomba Mwenyezi Mungu, kwani anajua mengi zaidi, lakini kusema ukweli hali inatishia. Kwa hiyo, nawapa pole wale wananchi, tuendelee kumwomba Mungu atujalie tupate mvua kama tutaokoa chochote na kuweza kufanya chochote kitakachowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumshukuru Mheshimiwa Rais na kumpongeza sana, kwa sababu hotuba yake tuliyokwenda kuisikiliza pale Kilimani, ilifungua mwanga wa bajeti kwa maneno mengine, kama tungekuwa shuleni tungesema tulianza kupata Desa la Bajeti. Kwa hiyo, tulianza kupata picha bajeti yetu tunatarajia iweje baada ya hotuba nzuri ya Mheshimiwa Rais; hivyo, nina kila sababu ya kumpongeza pamoja na kuzungumzia yote hayo aliyoweza kuyaweka kama *stimulus package*. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu wake na Watendaji wote pale Wizarani, kwa kutuandalia haya waliyoweza kutuletea, kwa sababu kwa upande mwingine nao wangeweza kufanya mengi na makubwa zaidi lakini uwezo ndio hapo ulipokwama. Kwa hiyo, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumwomba Mheshimiwa Waziri, labda atakuja kunisaidia kunipa tafsiri kutokana na huu mtikisiko wa uchumi hapa duniani unaoendelea hivi sasa. Nchi kubwa na tajiri zimeanza ku-*inject* fedha katika Mabenki yao na Makampuni yao; je, kiuchumi ndio tunasema kwamba ule uchumi sasa utakuwa unamilikiwa na Serikali kwa sababu zile fedha wanazotoa ni mkopo kwa yale Makampuni tofauti na ile Sera yao ya Kibepari? Mheshimiwa Waziri, atatusaidia Serikali zinavyo-*inject* fedha katika hayo Makampuni na Mashirika mbalimbali hiyo tafsiri maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetangulia kusema kwamba, hali ya hewa kule Hai Mkoani Kilimanjaro sio nzuri, kwa hiyo, niendelee kumwomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu nimeshazungumza na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kabla na alishapeleka wataalamu wake kufanya tathmini, atakapoomba fedha kidogo kutupatia msaada wa chakula asisite, kwa sababu ndiyo hali halisi ilivyo. Kwa hiyo, nazidi kusisitiza kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba, tutahitaji msaada. Nimwombe Mheshimiwa Waziri pia wakati anahitimisha, atueleze tunapata kigugumizi gani hadi leo hii, huduma nyingi hapa nchini bado zinatolewa kwa fedha za kigeni (Dola); je, hii haisababishi kutikisa uchumi wetu; kwa nini Serikali haijawa *very firm on this issue*? Unafika kwenye baadhi ya maduka, mwenye duka anakuuliza utalipa kwa Dola au unalipa kwa shilingi! Sawa sawa na wale wengine wanaokuuliza je tukuandikie risiti au tusikuandikie!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri, atueleze hii katika uchumi ina athari kiasi gani kwamba fedha yetu hapa nchini haithaminiwi vya kutosha? Mfano tosha ni nchi jirani kama ya Kenya, *strictly* huwezi kutumia Dola kwenye maduka yao na hata ukilipa kwa Dola, utarudishiwa *change* kwenye fedha yao ya Kenya. Hali kadhalika South Africa, utalipa kwa *Rands* na *change* yako itakuwa ni kwa

*Rands,* ukiwa na fedha za nje unaambiwa nenda duka la kubadilishia fedha hawapokei fedha za kigeni na nchi nyingine ni hivyo hivyo lakini hapa Tanzania kuna uhuru uliopita kiasi. Kwa hiyo, nitamwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kama ile sheria imeshindwa kufanya kazi na athari za kutumia Dola badala ya kuitumia shilingi yetu ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha na kuendeleza yale mazuri yote yaliyofanywa na yanayoendelea kufanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni lazima kuimarisha ukaguzi wa kiufundi *(Technical Audit*). Lazima kufuatilia kwa karibu Matumizi ya Serikali *(Expenditure Tracking),* pamoja na kuthaminisha miradi yetu kujua kama thamani ya miradi tunayoelezwa kwenye vitabu ipo. Vilevile ni ukweli usiopingika, kuna miradi mingi sana imefanyika; mingine imefanyika vizuri kwa *quality* inayoridhisha lakini mingine ipo chini ya viwango vinavyotarajiwa (*sub-standard)*. Ili tuweze kuwa na matumizi mazuri ya fedha ya mlipakodi wa Tanzania, kwa sababu hata ile ya nje tutakayokuwa tunakopeshwa tunakopa kwa jina la Serikali yetu ya Tanzania; kwa hiyo, niombe tuwe tunafanya haya mambo yote ili tuweze kupata thamani halisi ya ile miradi na miradi ambayo ina viwango vinavyoridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii dhana au kaulimbiu yetu Kilimo Kwanza, baadhi ya ndugu zetu labda hawajaelewa vizuri, wamekuwa na wasiwasi mbona tulikuwa na mambo mengi; DADPs, ASDP vitu vingi tu wanasema kwamba labda ile tumeiacha hatujaiacha. Mipango yote ya kilimo, mipango yote ya Serikali, mipango yote ya kumwendeleza mwananchi, natumaini iko pale pale ila ni kaulimbiu ya kumhamasisha Mtanzania kwamba Kilimo Kwanza. Kwa wale waliosoma *Chemistry* ni kama *Catalyst,* haibadilishi ila inaharakisha. Kwa hiyo ni kaulimbiu ya kuweza kumwamsha zaidi Mtanzania na kumhimiza na kumsisitiza kwamba kilimo ni kipaumbele na ndicho kitakachotusogeza mbele kuepukana na umaskini. Kwa hiyo, niwatoe wasiwasi wale ambao wanadhani kwamba ile mipango mingine yoyote iliyopo inawekwa kando na tunakuja na huo mkakati mpya wa kilimo kwanza, hapana. Naamini kwamba, mipango yote; DADPs, ASDP na mingine, bado inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizidi kusisitiza tu; ili tuweze kumkomboa huyu Mtanzania elimu ya ujasiriamali ni kitu muhimu sana. Katika elimu ya ujasiriamali si suala la fedha tu, kuna kumpatia huyu Mtanzania elimu kama ni kilimo cha kuku wa kienyeji, kilimo cha ufugaji kwa maana yake, lakini ajue anafuga vipi hata huyo kuku wa kienyeji awe na tija kwake. Ng’ombe wake wa maziwa, kilimo kama wanalima kilimo cha mazao, analimaje hicho kilimo ili kiwe na tija kwake. Naomba nisisitize elimu ya ujasiriamali kwa wananchi wetu ni muhimu sana na nimeligundua hili baada ya kuwatembelea wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Arusha kuna kampuni moja NGO RECODA, wana mambo mengi ya ujasiriamali; nimewaomba tumeweza kupeleka baadhi ya wananchi kutoka katika kila kijiji katika Wilaya yetu ya Hai. Baada ya kufika kule ni kwamba, wameshuhudia na ile elimu wamekiri kwamba inawasaidia. Hivi sasa tuko kwenye maandalizi, tuweze kwenda kutoa elimu zaidi kwa wananchi wote kule Wilayani Hai kwa kushirikiana na Halmashauri yetu ya Wilaya ya Hai, NGO ya Wananchi wa Hai inayojulikana kama Hai Maendeleo Kata (HAMAKA), pamoja na hawa watu wa

RECODA. Ufumbuzi wa matatizo tuliyonayo ni wananchi wetu waweze kupatiwa elimu ya ujasiriamali. Wananchi wetu wanafanya kazi kama kawaida; mtu anaamka asubuhi anaingia shambani, anatumika kwa muda mwingi sana lakini pasipokuwa na ile elimu atakuwa anapoteza muda yule mwananchi. Kwa hiyo, tuwasaidie wananchi wetu katika kuwapatia elimu ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda si mrefu, natumaini Watanzania watashuhudia hatua ya maendeleo ambayo Tanzania tutakuwa tumeifikia na niwaombe wananchi wasisikilize porojo au kelele nyingi ambazo zinapigwa huko pembeni kwamba, Serikali ya Chama cha Mapinduzi haijafanya. Serikali ya Chama cha Mapinduzi, imefanya mambo mengi sana. Niungane na Mheshimiwa Nyalandu, alituelezea vizuri tusikae upande wa kulaumu tu, tuangalie upande mwingine nini ambacho kimeshafanyika. Tangu tumepata uhuru hadi leo tumefikia wapi? Ni kwamba Serikali imefanya vizuri sana na inaendelea kufanya vizuri ni kiasi tu cha muda mfupi ujao wananchi waweze kushuhudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sera za mapato ambayo tumeyasoma katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri, pamoja na vipengele vingine vyote, kile cha udhibiti wa bidhaa za mafuta ya petroli pamoja na *flow meter* ni muhimu mno. Kitakachokuambia hizi *flow metres* huwa zinaharibiwa kwa makusudi, angalia utitiri wa vituo vya mafuta vilivyojaa kuanzia Dar es Salaam kuja Chalinze. Ukitembea ukiangalia pembeni ni kama vile unapigishwa kwata, kushoto kulia, kushoto kulia ni vituo tupu. Kusingekuwepo na hujuma au dalili mbaya ya kukwepa mambo, hivi vituo visingeota kama uyoga. Kibaya zaidi, watu wengi sana wamepata hasara kutokana na uchanganyaji wa mafuta wanaita Chua au Chakachua, yale ambayo yanatakiwa kwenda nchi nyingine yanarudishwa hapa ndani, kwa hiyo, inatuvurugia uchumi wetu. Namshukuru Mheshimiwa Waziri amelitaja hilo. Niombe sana kile kigugumizi cha kuiwezesha TPDC kuagiza mafuta kwa wingi kiishe. TPDC yetu tuiwezeshe iweze kuagiza mafuta na tuweze kudhibiti soko la mafuta. Bei itadhibitiwa lakini pia na *quality* ya mafuta itakuwa nzuri na tutapata mafuta bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia Kodi ya Majengo, ambayo Mheshimiwa Waziri ameizungumzia kwenye kitabu chake cha bajeti. Naomba hizi kodi zinapotozwa na wale wananchi wanaolipia wapate huduma kama za barabara na vitu vinginevyo. Ukija kwenye suala la kipengele cha mapato kutoka Serikali za Mitaa, angalizo tu ni kwamba, tusije kurudisha ile kodi ya kichwa. Vilevile Waziri amezungumzia mapato ya Serikali za Mitaa na vyanzo vya mapato au mirabaha kutokana na maliasili zilizomo katika eneo la Halmashauri husika. Nikumbushie tu, katika Halmashauri tano zinazozunguka Mlima Kilimanjaro, bado hatupati lile gawio. Tuliahidiwa kwamba, tutaanza kulipata na ni wakati muafaka kutokana na hii bajeti ilivyo, ndiyo maliasili tuliyonayo. Kwa hiyo, tupate gawio kutokana na mapato ya Mlima Kilimanjaro, kama wenzetu wanavyopata kutokana na madini. Hii misaada na mikopo, nisingeamini sana misaada ni bora tungefunga mkanda kidogo tukope tufanye kazi kwa ujasiri zaidi na kwa bidii zaidi.

Uwezeshaji Watanzania kiuchumi ni muhimu sana, suala la *black empowerment* kama wenzetu wanavyoita kule Botswana; tuangalie ni kazi gani Mtanzania anafanya na yule ambaye sio Mtanzania. Tusiwe na kigugumizi wala tusiogope kwamba watu watatusemaje, haya ni mambo yetu ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umwagiliaji kwenye kilimo ni muhimu sana kuboresha kilimo chetu cha mazao. Muda usije ukaniishia, niendelee kuishukuru Serikali kwa ile mipango mizuri iliyonayo katika mambo ya miundombinu na niombe kabisa kwamba, barabara ya lami inapojengwa lazima ina muda wake wa ukarabati, usipoikarabati ile barabara itakuwa ni hasara zaidi. Kwa hiyo, tuendelee kuzikarabati barabara tulizonazo na tuendelee kujenga nyingine mpya. Mengine yote yamezungumzwa, lakini lile suala la misamaha ya kodi kufutwa kwenye Makampuni ya Madini ni muhimu mno. Haya Makampuni yameshapata starehe ya kutosha, tusipate kigugumizi wala tusiseme ni Makampuni mapya yatakayokuja kuingia mikataba, haya yaliyopo ule msamaha ufutwe, lakini Taasisi zetu za Dini na NGO zisamehewe. Baadhi ya NGO kweli hawafanyi vizuri, Taasisi zetu za Dini zile nyingine ambazo hazifanyi vizuri, Serikali ina macho na mkono mrefu lakini naomba zile ambazo zinafanya vizuri, ziendelee kupunguziwa kodi na Serikali iingie ubia nao na ndiyo maana tunaweza kupata elimu na afya kupitia Taasisi za Dini. Naomba sana, Mheshimiwa Waziri afafanue hili jambo ili lilete amani. Viongozi wengi wa Dini wametupigia simu wakilalamikia hili jambo, shule ziko nyingi sana na hospitali zilizojengwa na Taasisi za Dini ni nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja licha ya muda mfupi. Ahsante sana. *(Makofi*)

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Manaibu wake wote wawili; Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji wote. Nawapongeza sana na kwa leo nasema mbarikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo nitapenda nijikite sana kwenye kaulimbiu ya Kilimo Kwanza. Katika kuizungumzia, nitazungumza mambo mbalimbali mojawapo kilimo kwanza kinategemea sana miundombinu, kwa maana ya barabara na mambo mengine. Kwa mara ya kwanza, nasimama hapa Bungeni kutoa shukrani za pekee kwa Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kutimiza ahadi waliyoahidiwa Wananchi wa Jimbo la Karagwe, Barabara ya Kyaka mpaka Bugene. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii iliahidiwa na Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais ni msema kweli, anayoahidi anayatimiza, barabara yangu hii ya Kyaka hadi Bugene kwa mara ya kwanza imetengewa shilingi bilioni 3.6 si haba. Wananchi wa Karagwe wamefurahi sana, nimewapigia simu na wengine wataendelea kunipigia simu, wanaishukuru sana Serikali. Cha msingi, baada ya bajeti hii kupita, ninaomba Serikali ipeleke watendaji kwenye *site* haraka sana. Nisingependa kuona barabara hii inadorora na inasuasua, tunajua mambo ya mwaka 2010 yanakaribia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kuna jambo moja limenivutia sana, limenifurahisha, nalo ni kuhusiana na kupunguza ushuru wa mazao ya ununuzi kutoka asilimia tano kwenda asilimia tatu, kiwango cha ukomo. Kabla ya hapo, kiwango cha ukomo wa ushuru wa mazao kilikuwa asilimia kuanzia moja mpaka tano, lakini hapa wameshusha kuanzia moja mpaka tatu. Mimi nasema nimefurahi sana, kwa sababu hii itawaongezea wakulima na hasa wakulima wangu wa kahawa, bei nzuri ya kahawa yao, kwa sababu kadiri ushuru unavyopungua, basi na mnunuzi anayenunua kule shambani anaongeza bei inakuwa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kilikuwa ni kilio changu cha siku nyingi ninaposimama hapa Bungeni. Pamoja na shukrani hizi, nilitaka kusema kwamba, kama kweli tunasema Kilimo Kwanza na Kilimo Kwanza kimjali mkulima; mimi ningesema hii asilimia tatu iondoke na ushuru huo uondoke moja kwa moja. Kabla ya hapo, kuna wengine walikuwa wanatoza ushuru wa asilimia tatu kwa sababu ilikuwa ni kuanzia asilimia moja mpaka tano; kwa hiyo, ningependekeza ushuru wa mazao uondoke moja kwa moja na mapato haya yaende kwa mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalizo pekee ni kwamba, Serikali ihakikishe inafidia mapato ya Halmashauri ambayo yatapotea kwenye Halmashauri zao. Nasema hivyo kwa sababu Halmashauri yangu ya Wilaya ya Karagwe, mwaka jana tulipata ushuru huu karibu shilingi bilioni moja, kwa hiyo utakapopotea nadhani Serikali itaturudishia. Katika Kilimo Kwanza, nikipongeze Chama cha Ushirika cha Karagwe KDCU, chenyewe kimetangulia haraka sana kuwapa Wananchi wa Karagwe miche ya kahawa bure. Serikali ilenge kuwawezesha wananchi kuwapa bure miche ya mazao. Vile vile soko la kahawa duniani na hapa nchini linanipa utata. Katika hili, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha anisikilize kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Jimbo la Karagwe na Wilaya ya Karagwe kwa ujumla ni wakulima wazuri sana wa kahawa. Inapofika wakati wa kuvuna kahawa zao na kwenda kuuza, Soko la Tanzania linakuwa chini sana, lakini Soko la Uganda linakuwa juu mara mbili ya Soko la Tanzania na Wananchi wa Karagwe wanapenda kuuza kahawa yao kwa bei ambayo inalipa na si bei ambayo inawalalia. Sasa wanapoamua kuuza kahawa yao Uganda, Serikali inawawekea udhibiti wa hali ya juu sana mpaka maaskari wanakwenda kuwavizia kule mpakani.

Mimi najiuliza; kwa nini bei hii ambayo inapatikana Uganda isiletwe hapa Tanzania ikawa sawa Wananchi wangu wa Karagwe wakauza kahawa sawa na bei inayopatikana Uganda kuliko kuanza kukimbizana na Polisi wasiuze kahawa yao Uganda? Tatizo hili la soko, naomba Serikali ilifanyie kazi na haipendezi kusikia wananchi wanakamatwa kwa fedha zao binafsi.

Katika Kaulimbiu ya Kilimo Kwanza; Mheshimiwa Rais nilimsikiliza kwa makini sana wakati anaazungumza majuzi na kuna kitu kimoja cha msingi alikizungumza. Alisema; Kilimo Kwanza lazima iendane na *component* ya mawasiliano. Katika mawasiliano bajeti ya mwaka jana tulipitisha hapa Bungeni shilingi bilioni 17 za kitanzania, fedha hizi tulizilenga kujenga Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Mkongo

huu baada ya kutengewa fedha, kwa masikitiko makubwa fedha hizo hazikutolewa katika mwaka wa fedha 2008/2009, badala yake zilitolewa shilingi bilioni sita peke yake, maana yake ni kwamba, mkongo hatuuhitaji na hatutaujenga.

Mkongo huu katika awamu ya kwanza una awamu mbili; awamu ya kwanza unategemea kugharimu shilingi bilioni 30. Sasa katika bajeti hii ni shilingi bilioni nne tu zimetengwa kwa ajili ya Mkongo huu wa Taifa na Mheshimiwa Rais amesema hiki ni kipaumbele. Amesema mengine yanaweza yakasubiri lakini mkongo kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Waziri wa Fedha atueleze, je, Mkongo huu haujengwi tena na makubaliano tumejipangia kwamba ifikapo mwaka 2010 tayari uwe umejengwa? Mkongo huu ukikamilika, utakuwa na manufaa mengi sana. La kwanza, utapunguza gharama za simu za mkononi kwa wananchi wetu wa vijijini; kwa sababu utafika mpaka ngazi za vijijini. Pili, mkongo huu utakuwa na faida; kwanza, utaingiza mapato kwa Serikali yetu, utaenda nchi ya Rwanda, Burundi na DRC; na pia mkongo huu utatuwezesha kupunguza gharama za kuajiri hata walimu. Mwalimu mmoja wa *physics* ana uwezo wa kufundisha wanafunzi wa nchi nzima akiwa Dar es Salaam ama sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na mkongo huu, Daktari mmoja kutoka Uingereza anaweza akawaongoza Madaktari walioko Karagwe wakafanya operesheni ya mgonjwa. Mkongo huu una uwezo wa kuboresha mawasiliano ya kibiashara na mambo mengi. Kwa hiyo, naomba Serikali ijitahidi, itafute fedha mkongo huu ukamilike ifikapo 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nitazungumzia Kilimo Kwanza; katika Kilimo Kwanza kuna *component* moja muhimu sana ya miundombinu ambayo inahusisha viwanja vya ndege, reli, bandari, meli na kadhalika. Wenzangu wamezungumzia kuhusiana na viwanja vya ndege, Mheshimiwa Kagasheki, Mbunge wa Bukoba Mjini, naomba nimsemee kidogo; ule Uwanja wa Ndege wa Bukoba Mjini tumeona umetengewa fedha na wanasema kwamba ni Bukoba Mjini na Mpanda. Sasa mimi sijui Bukoba Mjini na Mpanda hicho ni kiwanja gani cha ndege? Mimi nakifahamu Kiwanja cha Ndege cha Bukoba peke yake na Kiwanja cha Mpanda peke yake.

Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapokuwa ana-*wind up*, atueleze wazi fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya Kiwanja cha Ndege cha Bukoba Mjini? Vilevile naomba fedha hizo zikitengwa, zijenge kiwanja cha ndege haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimo Kwanza ni pamoja na usafiri wa majini. Mwaka jana nilisimama hapa kuzungumzia madhara yaliyoipata MV Bukoba, nikazungumzia matatizo yanayoipata MV Victoria. Wakati napitia makabrasha haya, nimeona MV Victoria ilistahili kufanyiwa matengenezo yanayogharimu shilingi bilioni 1.4. Kwa masikitiko makubwa sana, MV Victoria haikutengewa hata shilingi moja. Sasa pamoja na kusema Kilimo Kwanza, lakini nasema MV Victoria Kwanza katika bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua madhara ya meli kuzama; juzi hapa tumeona matatizo kule Zanzibar na sehemu nyingine. Kuna MV Lihemba ya mwaka 1913 tangu itengenezwe imezeeka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie umeme vijijini na nilitaka kutoa tahadhari mapema sana; umeme vijijini tumepata ahadi za kutosha za Mheshimiwa Rais, mara ya mwisho anatoka Karagwe aliahidi umeme kabla ya 2010 utakuwa umekamilika. Mheshimiwa Ngeleja, nimezungumza naye kiasi cha kutosha, amenipa ahadi nyingi sasa nimechoka na niseme inatosha. Nasema hivi; katika Bajeti ya Nishati na Madini kama umeme Vijijini Karagwe hautakuwepo, umeme wa Misenyi kwa Mheshimiwa Kamara, umeme kwa Mheshimiwa Katagira hautakuwepo, napenda kuahidi kwamba, nitawashawishi Wabunge wenzangu wote, bajeti hiyo isipite kwa mara ya kwanza. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Ngeleja aende kutafuta pesa mahali popote, tunataka ahadi ya Mheshimiwa Rais itimizwe. Mheshimiwa Rais akishasema Waziri anasubiri nini kutekeleza? Naomba niweke msisitizo katika hilo. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mabina amesema hapa kwamba, sisi tunatoka Ziwa Victoria, zamani Mkoa wa Kagera ulikuwa unaitwa West Lake, tumezungukwa na Ziwa lile lakini la ajabu ni Mkoa pengine pekee ambao hauna miundombinu ya maji. Tunaposema kilimo kwanza tutamwagilia vipi, twende tukachote maji Ziwa Victoria tupeleke mashambani? Ule Mradi wa Mwanza - Shinyanga - Kahama ninaupongeza sana. Serikali itenge fedha kupeleka mradi mkubwa sana wa maji Mkoa wa Kagera. Kilimo Kwanza hakitafanikiwa hata kidogo kama hatutakuwa na Benki ya Wakulima. Benki ya Wakulima ni muhimu sana ili wananchi waweze kukopa kwa wingi, mtaji mkubwa wenye riba nafuu na pia wa muda mrefu. Bila kufanya hivyo, hatutaweza kuwasaidia wakulima wetu. Amezungumza Mheshimiwa Katagira kuhusu kuitenganisha Wilaya ya Karagwe, ninarudia tena kuunga mkono, tunaomba Wilaya ya Karagwe itenganishwe kwa sababu ni kubwa na maendeleo yanachelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumzia msamaha wa petroli katika makampuni ya madini ifikapo tarehe 1 Julai, 2009. Kuna neno hapa petroli imetumika kusamehe makampuni ya madini, lakini makampuni ya madini yaliyo mengi hayatumii petroli yanatumia dizeli peke yake kwenye mitambo na kwenye magari. Sasa nitaomba ufafanuzi vizuri kama petroli inahusisha na dizeli au vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mseminari, nimesoma seminari na nayashukuru sana Masharika ya Dini pengine kama si hayo nisingekuwa hapa. Mimi niiombe Serikali, hatutaki ugomvi na watu wetu wa dini, wawe Wakristo au Waislam, ninaomba suala hili busara ya Serikali itumike vizuri sana kuweka suala hili la kuondoa misamaha ya kodi katika Mashirika ya Dini. Nchi yetu haina dini, lakini sote hapa tuna dini zetu; iwe ya asili, iwe ukristo au uislam na tunajua michango mikubwa sana ya Mashirika ya Dini. Kuendelea kuwachokoza wale wazee wetu wa dini ni kutenda dhambi kubwa sana mbele ya Mwenyezi Mungu. Naomba Mheshimiwa Mkulo, aweke vizuri taarifa hii Wabunge tuipate ili tunapokwenda kule Majimboni kwetu, tuweze kueleza vizuri. Maaskofu wangu wanalalamika sana, hata na Masheikh wamelalamika sana kwa sababu ya hizi taarifa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, nataka nizungumzie msamaha wa vifaa vya maziwa. Nimefurahishwa sana msamaha huo, lakini pia nimefurahi sana kuweka ushuru wa maziwa kutoka nje ya nchi, ile asilimia 60, kwa sababu itazuia maziwa yasitoke nje na kuingia hapa nchini. Isipokuwa swali; tunapozuia maziwa yasitoke nje; je, sisi tunavyo viwanda vya kusindika maziwa au tumejipanga vipi maana tusije tukaishia kuwapa watoto wetu utampiamlo? Je, tunayo mifugo bora ya kuzalisha maziwa; tuna mbegu bora? Najua tuna kituo cha kuzalisha mbegu za mifugo pale Arusha, lakini kwa masikitiko makubwa kituo kile kimetelekezwa. Bajeti yake humu siioni na kama kinapewa bajeti ni ndogo sana; hakina magari, watendaji hawawezi kufika hata kwa wafugaji. Kwa hiyo, katika hili ninapongeza lakini ninatoa tahadhari pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi*)

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja muhimu inayohusu bajeti ya mwaka 2009/2010. Awali ya yote, niishukuru sana Serikali kupitia Wizara ya Fedha, ikiwa ni pamoja na Waziri, Manaibu wake, pamoja na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuweza kutuletea bajeti hii ili tuweze kuichangia. Naamini kama wasingeiandaa, tusingekuwa hapa tukiichangia. *(Makofi*)

Kipekee kabisa, nimpongeze na kumshukuru sana Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, kwa hotuba yake nzuri. Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa kazi nzuri waliyoifanya na kwa kweli ninawashauri Wabunge wote, tuweze kuipitia hotuba hii ya Mwenyekiti kwa sababu ina mwelekeo mzuri sana na uchambuzi wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa nianze kujikita katika maeneo makubwa matatu; lile la elimu, kilimo na miundombinu. Nianze kwa kuangalia sura ya bajeti kama ambavyo imewasilishwa. Ukiangalia ukurasa wa 65, utaona kwamba kwa mwaka huu tunaanza bajeti yetu kwa nakisi; yaani tunaanza kwa nakisi ya shilingi trilioni 1.1 na hii tunaambiwa kwamba Serikali itakopa ndani. Hilo mimi naona ni tatizo kwa sababu maana yake ni kwamba, tunatumia kuliko tunavyokusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hilo, niende kwenye suala zima la kuondoa misamaha ya kodi kwenye Mashirika ya Dini. Najua hili limezungumzwa na watu wengi, lakini naomba nami nilizungumze hasa nikizingatia ni jinsi gani yameweza kusaidia wananchi wengi na hasa kielimu. Najua kuna wengi hapa Bungeni wamepitia shule mbalimbali za Mashirika ya Dini. Mheshimiwa Waziri, anasema kwamba vifaa vya kiroho vitaendelea kupata msamaha. Vifaa vya kiroho ni vipi kwa sababu siku zote huwezi kutenganisha roho na mwili?

Kwa hiyo, nategemea Mheshimiwa Waziri atatupa maelezo ya kina. Nimejaribu kuchunguza, nikaambiwa inaelekea kwamba, kuna watu wametumia msamaha huo kwa shughuli zao nyingine labda za kibiashara. Kinachonisikitisha ni kwamba, Serikali ndio

wasimamizi; kwa mfano, Mashirika ya Dini yapo katika Wilaya zetu zote na hiyo inajulikana.

Kwa maana hiyo, Wakuu wa Wilaya wanaelewa na vilevile watu wa TRA wanajua. Endapo tatizo hilo limejitokeza, basi wale wahusika wachukuliwe hatua lakini si kwa mashirika yote. Ikumbukwe wazi kwamba, hata kama ni Askofu au Sheikh hawana kinga. Kwa hiyo, kama Serikali ipo ambayo tunaamini ndiyo dola, wanaweza kuwachukulia hatua wale ambao wamekiuka taratibu, lakini kusema wanafuta kodi, watakuwa wanawaonea kwa sababu sote tunajua ni jinsi gani Mashirika haya yamesaidia. Kwa mfano, sasa hivi nina hakika kabisa kule vijijini magari ya Maaskofu, Mapadri ya Masheikh, yanatumika kama *ambulance*. Sasa ndugu zanguni, naomba lifafanuliwe hili kwa kina ili tusilete matatizo katika nchi hii. Sote tunajua ni jinsi gani tumefaidika na jinsi gani tunaheshimiana kati ya dini na Serikali na jinsi gani tumekuwa tunawatumia Viongozi wa Dini kwa ajili ya maadili, tukiwa katika makongamano tunawaomba watusaidie.

Inapofika hapa, kwa nini tunakwenda kinyume; niiulize Serikali au kwa sababu sasa hivi tumekuwa na maendeleo makubwa ya MMEM, MMES na sasa kuna mpango mzima wa MMAM ndiyo sababu tunataka kuwatelekeza? Mimi nadhani tuna haja ya kukaa Serikali na Viongozi wa Dini wa-*discuss* waone ni wapi wanaweza kurekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, labda niendelee kwenye suala zima la elimu. Katika vipaumbele mimi niipongeze Serikali kwa vipaumbele; nilitegemea elimu itakuwa kipaumbele namba moja na hivyo ndivyo imekuwa na tunaona hata kiasilimia kama ambavyo nimeweka imepata asilimia 18.3. Suala la elimu ni la msingi sana, tusipowekeza katika elimu maana yake sehemu nyingine au sekta nyingine zote zitakuwa zimekwama. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie nchi za Asia; huko nyuma Nchi za Asia maendeleo yalikuwa *almost* sawa na Nchi za Afrika, lakini wao waliamua kuwekeza katika elimu na tunaona sasa hivi mafanikio waliyoyapata wataalamu wengi mpaka Ulaya wanaotoka Asia. Hata tukiangalia Pato lao la Taifa lipo juu sana, kwa sababu waliamua kuwekeza kwenye elimu. Tunapozungumzia suala la elimu, tunazungumzia suala la kitaaluma na ndiyo sababu tunaona hata katika suala zima la afya na suala la miundombinu, wale wataalamu wote wanaofanya zile shughuli wamesoma. Kwa hiyo ni vyema kabisa tuendelee kuipa kipaumbele elimu, lakini tunapoipa kupaumbele tuangalie pia suala zima la ubora wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, tunatoa fedha nyingi sana kwa elimu, kwenye bajeti inaonekana ni trilioni 1.7, lakini ukimuuliza Waziri wa Elimu atakwambia ana bilioni 507, inaeleweka kwamba labda fedha nyingine zimeenda kwenye elimu katika Wizara nyingine. Kwa mfano, sasa hivi suala la D by D, elimu ya msingi na sekondari imepelekwa TAMISEMI. Suala la msingi la kujiuliza; je, tunaangalia ubora au wingi? Jambo la kusikitisha sana, pamoja na kuipa elimu kipaumbele toka mwaka jana, lakini bado shule zetu hasa za msingi na sekondari, zina matatizo makubwa sana ya walimu na ni jambo la kawaida kusikia kwamba shule ina mwalimu mmoja au wawili wanandoa. Hivyo, panapokuwa na tatizo kwa sababu binadamu sio chuma anaweza

kuugua, mwalimu anakwenda kuchukua mshahara, kwa hiyo ina maana shule ile inakuwa likizo. Siyo hilo tu, vitendea kazi, kuna *capitation fee* ya shilingi 10,000 kwa kila mwanafunzi wa *primary*, lakini sijaona ni jinsi gani inajitokeza katika bajeti. Kwa hiyo, ina maana watoto wetu hawataweza kupata vitendea kazi kutokana na suala zima la *capitation fee.* Lingine lililonivutia katika suala la elimu inasemekena katika bajeti wamesema kwamba, watahakikisha wanajenga nyumba za walimu hasa katika maeneo tunayoyaita *remote area.* Mimi ninaiomba sana Serikali itekeleze hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za pembezoni hazina nyumba na ndiyo sababu unakuta walimu wengi hawaendi kuripoti kule, matokeo yake watoto wale hawapati elimu iliyo bora. Kwa hiyo, ninaomba Serikali itekeleze kama ambavyo wametueleza.

Nakuja kwenye suala zima la elimu ya juu. Suala la elimu ya juu ni la msingi sana. Pamoja na kuzungumzia suala la elimu ya msingi na ya sekondari, lakini lazima tujue kwamba, wataalamu waliobobea hawawezi kupatikana kutoka shule ya sekondari. Lazima hao watokane na elimu ya juu, ikiwa ni pamoja na kuwa ama na Masters au PhD. Kinachosikitisha ni kwamba, ukiangalia suala zima la mikopo ya elimu ya juu, kwa kweli ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda wa miaka miwili mfululizo, Bodi ya Mikopo imekuwa ikipewa takriban shilingi bilioni 117 wakati kwa mwaka huu sote tunajua ni jinsi gani ongezeko la wanafunzi linavyoendelea kuongezeka katika vyuo vya elimu ya juu, hii ikiwa ni kwa sababu ya mpango mzima wa MMEM na MMES; Kwamba, tunaendelea kupata wanafunzi kutoka sekondari ambao kutokana na ule mpango wa MMES wanaendelea kuwa wengi na kwa maana hiyo, ita-*reflect* pia kwenye elimu ya juu. Mwaka juzi wanafunzi wa elimu ya juu walikuwa takriban 60,000, sasa hivi tunavyoongea ni zaidi ya wanafunzi laki moja. Fedha za mkopo zimekuwa zikipatikana zile zile na sote tunajua kwamba, pato la Mtanzania linaendelea kushuka, kwa maana hiyo bado wazazi hawana uwezo wa kuwalipia watoto wao. Kwa hiyo, utakuta wale wanafunzi wanaohitaji mkopo ni wengi sana lakini fedha ni zile zile.

Kwa hiyo, niseme kwamba, kwa mfano, mwaka huu bado wamepata shilingi bilioni 80 na sote tunajua ni jinsi gani matatizo ya mikopo yamekuwa yakileta madhara makubwa kwa taifa hili. Kwa mfano, wanafunzi wanapogoma ni lazima walimu na wafanyakazi katika vyuo husika waendelee kulipwa na lazima gharama za umeme ziendelee kulipwa. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali kwa mara nyingine tena, wahakikishe kwamba, pungufu ya bilioni 80 ambayo ipo katika bajeti ya mwaka huu, ipatikane. Pamoja na juhudi za Kamati na Waziri, bado fedha hizi hazijapatikana lakini naamini kwamba, kwa Serikali kuji-*commit* kuwa itazitafuta, izitafute ili wanafunzi wa elimu ya juu waweze kusoma kwa amani na utulivu. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna suala zima la miundombinu mibovu katika vyuo vya elimu ya juu. Mwaka jana peke yake, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilihitaji shilingi bilioni 100 kwa ajili ya ukarabati, lakini ni wazi kwamba, shilingi bilioni 100 ndio karibu nusu ya fedha za Wizara, kwa hiyo, ni jambo ambalo haliwezekaniki. Ukipita katika vyuo vya elimu ya juu vile vya zamani tukiacha cha

Dodoma ambacho ni kipya, hali ni mbaya mno, kwa mfano, badala ya wanafunzi kulala wawili kwenye chumba wanalala kumi. Hii ni hatari kubwa sana si tu kisaikolojia lakini kiafya ni mbaya. Hatujui katika vitanda viwili hivyo wanafunzi kumi wanawezaje kulala na sote tunajua maadili ya vijana wetu yamekuwaje. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali itupie jicho masuala mazima ya miundombinu ya vyuo vya elimu ya juu. Hata katika Hotuba ya Waziri anasema, wataendelea kuboresha miundombinu ya vyuo vya elimu ya juu. Ukiangalia katika bajeti hai-*reflect* hata kidogo. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara izingatie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala zima la bandari. Pamoja na kwamba, yameongelewa mengi sana kuhusu bandari na lawama zikienda TICTS lakini mimi bado nasema tuna matatizo makubwa sana na bandari yetu. Tanzania ni nchi ambayo imejaliwa kuwa katika *strategic position geographically*. Nchi nyingine zinatuonea wivu, tumezungukwa na nchi sita ambazo hazina bandari na kwa vyovyote vile, bandari hii ingeweza kabisa kuinua uchumi wetu kwa hali ya juu mno. Labda niseme tu kwamba, nchi kama Singapore, mwaka 2007 wameweza kusafirisha na kupokea makontena milioni 30 ya futi 20. Dar es Salaam kwa mwaka huo ni laki tatu tu mara 100. Hii ni aibu.

Hili ni tatizo kubwa sana na tujiulize sababu. Pamoja na kwamba, tunapata mizigo mingi sana, tunaambiwa DRC peke yake ina mzigo wa tani milioni tano. Tumeweza kuchukua tani milioni 1.9 tu, bado nchi nyingine tano ambazo sijazitaja. Kwa mantiki hiyo, tunaweza kupata tani milioni 10 kutoka katika nchi hizi zinazotuzunguka lakini bado hatuwezi. Wamezungumzia kuhusu TICTS, lakini mimi nasema pamoja na hilo tatizo kubwa ambalo naliona ni miundombinu yetu mibovu. Mimi naamini hata sasa hivi tukileta makampuni mengine matatu kama TICTS, bado suala la kuyatoa makontena kwenda nchi kavu litakuwa pale pale. Ukiangalia reli zetu bado ni mbovu sana na nimejaribu kuangalia kwenye kitabu cha maendeleo, reli hizo hazijawekewa bajeti. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tukiangalia barabara zetu bado ni mbovu. Kwa hiyo, ninasema kwamba ni lazima tuboreshe bandari yetu. Sambamba na hilo, nakumbuka kuna kipindi kama sikosei ni mwaka huu; Rais alipotembelea bandari alisema ana majina kumi ya wafanyakazi ambao wana-*collude* na wafanyabishara wakubwa ili walipe ushuru unaotosheleza kidogo. Hivi taratibu za utumishi zinakuwaje, kama kuna watu wa namna hiyo wanaokwepa kodi nchini kwa nini wasifukuzwe kazi mara moja na kupelekwa Mahakamani? Ndiyo maana tunasema TRA inashindwa, lakini kuna mambo ambayo Serikali inabidi iyafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja. *(Makofi*)

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii nichangie kidogo Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu Bajeti ya Mwaka 2009/2010. Kwanza, nampongeza sana yeye na timu yake, Naibu Mawaziri na Watendaji wote wa Wizara hiyo. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, nataka kuzungumzia hali halisi ya Bajeti yenyewe kwa ujumla Bajeti ni nzuri na inatia matumaini. Naanza kusema kwamba, naunga mkono bajeti hii. Uzuri wa bajeti hii utakuwa na maana zaidi ikiwa itatekelezwa ipasavyo na watekelezaji wa bajeti hii ni kila Mtanzania ambaye ana uchungu wa nchi kwa maslahi ya nchi hii na watu wake. Tatizo moja tulilonalo Watanzania ni kwamba, sisi ni watu wazuri wa kupanga mipango lakini tuna tatizo la utekelezaji. Katika kitu ambacho kinaturudisha nyuma kila mwaka ni kwamba, utekelezaji wa mipango yetu hauna ufanisi. Sasa uzuri wa vitabu au maneno haunogi kama hauna vitendo. Mimi nashauri na nawasihi Watanzania wenzangu, popote pale tulipo na kila mmoja kwa nafasi yake, tutimize wajibu wetu ili tuweze kupata haki yetu.

Haki bila wajibu haiwezekani, wengi wetu tuna desturi ya kulaumu sana Serikali haifanyi hivi, haifanyi vile, lakini sisi wenyewe hatujiulizi hivi tumeifanyia nini nchi hii au tunatakiwa tufanye nini ili hiki tunachokizungumza kifanikiwe. Sisi ni wazuri wa kulaumu sana, lakini ni wakosefu wa kutimiza wajibu wetu. Hili ndilo tatizo linalotushinda mpaka leo tunagombana kwamba, Serikali haifanyi kitu; wewe mwenyewe umefanya nini? Serikali ni nini? Serikali ni mimi, wewe na mwingine. Kwa hiyo, nawasihi ndugu zangu Watanzania, popote pale mnaponisikiliza, jamani tutimize wajibu wetu ili tupate haki zetu. Mimi nafikiri Serikali ina wajibu pia wa kuwaelimisha wananchi kila mmoja akajua haki na wajibu wake. Hii ni kazi kubwa, lakini kila siku tutapanga, tutaandika na hakutakuwa lolote kama hatutatimiza wajibu wetu. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawasihi ndugu zangu, hao tunaowaona wanaendelea kila mmoja anatimiza wajibu wake wa kulipa kodi na kufanya kazi, lakini sisi ni wazuri wa kusema tu vitendo hakuna. Mimi ninawasihi ndugu zangu, tujaribu kuwa waadilifu katika kufanya mambo yetu na kutimiza wajibu wetu kila mtu kwa nafasi yake alipo; kama mkulima alime vizuri na kama ni mwalimu afundishe vizuri na mwanafunzi amsikilize mwalimu vizuri *otherwise* tutakuwa tunaimba tu.

Mheshimiwa mwenyekiti, kuhusu hali ya uchumi; sote tunajua viongozi wetu, kama juzi Mheshimiwa Rais ametueleza vizuri sana, namna gani mtikisiko wa uchumi ulivyotukumba na hatua ambazo Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano inazichukua. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, atakapokuja kufanya majumuisho hapa, aniambie upande wa pili wa Muungano wana mikakati gani na wenzao kule kuhusiana na kunusuru hali hii ya uchumi wa mtu mmoja mmoja. Kule kwetu Visiwani, hii dhana ya Kilimo Kwanza ni ngumu kwa sababu hatuna ardhi ya kulima. Sisi kule ni Biashara Kwanza, lakini biashara yenyewe soko liko wapi, liko huku. Sasa kama hazijachukuliwa hatua za makusudi, kwa sababu kama mnavyojua, Zanzibar kwa kiasi kikubwa sana ilikuwa inategemea biashara ya utalii na utalii wenyewe pia umetetereka kutokana na matatizo haya ya uchumi wa dunia. Sasa kama itakuwa hakuna jinsi ya kuweza kupata angalau shilingi 1000 ya kununua kilo ya mchele, basi ujue Mzanzibari huyo ana tabu sana na hiyo ni kazi ambayo tunayo. Hakuna jinsi nyingine ya kuweza kupata maslahi kama hakutakuwa na harakati za kibiashara na huduma. Huduma zote haziishii pale, pale ni kama mlango tu zinaishia huku.

Mheshimiwa spika, sasa nafikiri katika kulegeza mambo haya ili kutusaidia na sisi kule ni kwamba, harakati za kibiashara na hasa soko hili la bara la bidhaa kutoka Zanzibar kuwe na *special case.* Sasa hivi tuache kidogo wenzetu wafanye biashara wajinasue, kwa sababu wakulima tayari wameshanasuliwa huko. Sasa mtatunasuaje kibiashara wakati soko liko huku? Kwa mfano; katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri alisema, naomba kunukuu katika ukurasa wa 53: "Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye huduma za upakiaji na upakuaji mizigo kwenye meli za hapa nchini kwa mizigo inayotoka nje ya nchi na ambayo huduma ya kupakua mizigo kutoka kwenye meli iliyotolewa mizigo kutoka nje ya nchi, ilishatozwa kodi hii. Hatua hii inalenga kuhamasisha wafanyabiashara kushusha mizigo katika bandari zetu nyingine za Tanga na Mtwara na hivyo kupunguza msongamano wa meli na mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam." Zanzibar haikutajwa. Bandari ya Zanzibar ni moja kati ya bandari ambazo zilikubaliwa katika Mkataba wa Afrika Mashariki. Hapa pananipa kazi kubwa, maana yake ni kwamba, Wazanzibari hawamo katika kuleta mizigo ambayo itateremshwa Zanzibar, ambayo pia ni bandari moja kati ya bandari zilizokubalika katika Mkataba wa Afrika. Naomba Waziri anieleze vizuri kwa nini hilo limekuwa hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule Zanzibar bila biashara hatuoni ndani. Kama tunavyojua, Kisiwa na sio cha Zanzibar tu, Visiwa vingi shughuli zao za kiuchumi zainakwenda katika harakati za *services* (huduma). Bila huduma hakuna jinsi, hatuna ardhi wala madini. Sasa kama ndugu zenu hamjatuachia hivyo na kwa taarifa yenu, Wazanzibari wote wanazitegemea mboga mboga na aina zote za nafaka kutoka Bara.

Kwa hiyo, hela yote inayopatikana kule matokeo yake itamnufaisha mkulima wa huku huku Bara; kwa nini? *Currency* yetu ni moja, Benki yetu ni moja, kwa nini isiwe hivyo mkatuachia na sisi kule kama mtu anataka kununua mchele, kununua maharage, anahitaji pesa na kama hakuna kazi ya kuzipata zile pesa, atazipata kutoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja kwenye suala la punguzo la thamani kwa vocha za simu. Hili ni wazo zuri kwamba, Serikali sasa itatoza ongezeko la thamani kwa vocha za simu wakati zinapokuwa zinaingia kabla ya kutumika. Nakubaliana na wazo hili ni zuri, lakini kuna kitu kimoja; sijui kama Serikali inalijua hili, kuna vocha hasa zile za shilingi 500, ambazo zinakuwa *printed* hapa hapa Tanzania na baadhi ya *dealers* wana mikataba maalumu na baadhi ya *telephone operators*. Vocha za mia tano, mia tano, zinakuwa na *some sort of papers* kama karatasi ya kawaida. Sijui kama hilo wanalielewa, kwa sababu zile nyingine zinakuwa *imported*, wanaweza wakazishika wakati zikiingia, zikitoka bandarini au *airport* wakaanza kuzitoza ushuru pale pale. Je, hizi zinazokuwa *printed* hapa wana taarifa hiyo au wata-*trace* namna gani? Kama wanayo itakuwa ni vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvuvi wa Bahari Kuu; Mheshimiwa Waziri na Wananchi wote wa Tanzania, waliona hivi karibuni bahari yetu ilivyokuwa na mali nyingi sana, ambayo inaweza ikatuokoa katika uchumi wa nchi yetu na wajanja wanavyotupiga *offside trick* wakachukua mali wakaenda zao. Juzi kwa bahati mbaya, wala si kwa bahati nzuri, maana mwizi akikamatwa ni bahati mbaya, tukawashika wale.

Sasa nafikiri hii ni kazi kubwa sana tuliyonayo mbele yetu, kuimarisha uvuvi ili tupate mapato ambayo yanastahili hasa kufuatana na mali aliyotujalia Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna tatizo moja ambalo linatokea la uvuvi haramu. Yale tuliyoyaona juzi juzi ya Mheshimiwa Magufuli kutembelea kwenye Mabwawa na Maziwa kuchoma nyavu, sasa kuna tatizo moja linalotokea hapa hapa Dar es Salaam la uvuvi haramu. Ukiwa unatoka bandarini Dar es Salaam kuelekea Zanzibar ni pale pale karibu na Visiwa vya Mbuja, sijui Mbuju zinakaa meli, kuna uvuvi wa mabomu pale, watu wanatupa mabomu na kuvua samaki kwa mabomu.

Hii ni hatari kubwa sana, matokeo yake wavuvi wale wanaharibu miamba kule chini ya bahari na baada ya muda si mrefu vile Visiwa vitakwenda havina kinga. Kuna Kisiwa kimoja kama mnakumbuka kule Tanga, kilikuwa kinaitwa Maziwe, kuna wavuvi haramu walikuwa wanavunja miamba ya chini, matokeo yake kile Kisiwa kimekwenda na maji. Kuna hatari pale ikiwa wavuvi wale hawajaangaliwa kwa makini au hawajakamatwa, watavunja miamba, vile Visiwa viwili au vitatu vitakwenda na maji yatakawa yatakuja zake buheri mpaka Msasani huku, wenye nyumba za Msasani baada ya siku mbili/tatu watapata *soil erosion*, habari imekwisha.

Wavuvi hao siyo kwamba hawaonekani, kwa sababu pale bandarini kuna mnara ambao unaona karibu sehemu zote za Pwani ya Tanzania. Wanawaona wanafanya yale na kuna *Police Marine* pale pale bandarini. Siyo mbali, ukipita tu ukienda Zanzibar kwa boti unakuta wanafanya kitu kama hicho. Ndicho kile tulichokisema, suala la uwajibikaji. Watu wenye shughuli zao na wenye kazi zao, hawawajibiki kutatua yale matatizo. Jambo lile watasema sijui ni la nani au sijui ni la Serikali; mimi sijui Serikali ni nani kama sio mimi, wewe na mwingine!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi ni yetu na kama tuna uchungu na nchi yetu, tuache kulaumiana, kila mmoja atimize wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ALHAJI MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ukweli ni kwamba, nilikuwa nategemea kuchangia kesho, nakushukuru sana kwa kunisogeza mbele na kunipa kuchangia leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kushukuru kwa hayo, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Manaibu Makatibu Wakuu wote watatu, Kiongozi wetu wa TRA na wote ambao wamehusika na kushiriki kikamilifu katika kutengeneza Bajeti hii mpaka imefika kwetu na sasa tunaiona kwamba ni yenye manufaa. Nawapongeza sana na nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia uniruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamahuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kikwete, kwa maelezo

mazuri aliyoyatoa kwenye mkutano aliohutubia Wazee na sisi Wabunge kule Kilimani. Baada ya kikao kile, Watanzania walio wengi na sisi wengine tulipata mwelekeo mzuri wa jinsi bajeti yetu itakavyokuwa. Amepunguza baadhi ya maswali ambayo tungemuuliza sana Mheshimiwa Waziri. Naomba tumshukuru sana kwa kutuongoza na Mwenyezi Mungu, aendelee kumpa afya ili aendelee kutuongoza vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuzungumzia suala la kilimo na uniruhusu niwapongeze Wakulima wa Wilaya ya Singida na Mkoa mzima wa Singida. Mwaka huu, Mwenyezi Mungu ametupa neema ya mvua, tofauti na majirani zetu Dodoma, Kondoa, Arusha, Manyara, Shinyanga na Tabora. Sisi katikati hapa tumepata mvua ya kutosha kwa rehema na mapenzi yake Mungu.

Kwa minajili hiyo, wananchi wetu wameitikia wito wa Serikali yao hasa Uongozi wa Mkoa na Uongozi wa Wilaya na sisi Wanasiasa katika kulima mazao yote ya biashara na ya chakula. Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana kwa kazi nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Watu wa Singida, kimsingi pale ambapo tuna mvua nzuri, sisi sio omba omba, tumekuwa tukijilisha. Kwa hiyo, wakati nawapongeza kwa kazi nzuri waliyoifanya, lakini niwaombe kama ambavyo tumekuwa tukiwaomba, kwa kuzingatia kwamba, majirani zetu wote wana matatizo ya chakula kwa sababu hawakupata mvua za kutosha, basi ni muhimu sana kutunza chakula. Niwaombe wale wanaonisikia na ambao hawanisikii waambiwe kwamba, kazi iliyopo sasa ni kutunza chakula kulingana na ukubwa wa familia ya kila mtu kwa sababu tunajua familia zenyewe. Majirani zetu watakuja, baadhi watakuja kwa nia safi, baadhi watakuja na nia nyingine ambayo siyo safi. Tunaweza tukajikuta ingawa tulikuwa tumeshiba, tukipata chakula cha kutosha, hatuna tatizo la njaa, lakini tukaipata njaa kwa sababu ya kutokutunza chakula na kuwaachia wenzetu wachukue chakula chote ambacho tumezalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile niiombe Serikali, ukiacha Singida katika hizi Big 4/5/6 wamepata chakula cha kutosha, naomba Serikali wanunue chakula cha hifadhi wakati huu ambapo bado bei ni nzuri. Kule Rukwa, Mbeya na Iringa bei bado ni nzuri, wanunue sasa wapeleke kwenye hifadhi, wasingojee mpaka bei zipande ndio nao wanunue, matokeo yake ni kwamba, hicho chakula kinachoonekana kama ni msaada kwa wananchi, baadae kinakuja kuwa ghali na mwananchi haoni kama anasaidiwa. Kwa mfano, Singida pale uje umuuzie mtu debe shilingi 7,000, shilingi 8,000 unamwambia huu ndio msaada wa chakula kutoka Serikalini, hawezi kukuelewa; atapata wapi shilingi 7,000 kwa debe, atapata wapi shilingi 8,000 kwa debe? Shilingi 3,000, shilingi 2,000, sana sana shilingi 4,000. Kwa hiyo, Serikali wanakuja kuuza ghali kwa sababu wanachelewa kununua chakula cha hifadhi. Sasa niwaombe sana kwamba, wanunue chakula cha ziada kutoka Singida, wanunue chakula cha ziada Rukwa, Mbeya, Iringa, Morogoro na Kigoma ili chakula cha hifadhi kije kiwe nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza swali hapa kuhusu Mpango wa ASDP nilipewa majibu, lakini kwa maelezo ya majibu niliyopewa na Mheshimiwa Waziri,

ukweli ni kwamba, Mpango huu bado haujulikani vizuri kwa wakulima walio wengi au kwa wananchi walio wengi. Alisema kwangu mimi vijiji 20, mimi nina vijiji 100, sasa vijiji 20 ina maana kwamba walio wengi hawana! Kwa hiyo, naomba Halmashauri zetu au Halmashauri yangu na nyinginezo, zibuni mkakati wa namna ya kuwaelimisha wananchi juu ya mpango mzuri wenye mahela mengi ya umwagiliaji na kadhalika. Wananchi waelewe faida zake ni hizi na kisha waweze kuibua miradi ambayo wanategemewa kufanyiwa. Kukaa hivi hivi tu, matokeo yake pesa zinatumika kwa mambo ya utawala na kadhalika badala ya kuwasaidia wale wananchi ambao wangehusika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ambao tunapata mvua mara moja ndio ambao hasa tunastahili kupewa nafasi kubwa katika masuala ya umwagiliaji. Wenzetu wanapata mvua mara mbili/tatu, sisi wa mara moja kwa kweli ndio hasa tungepewa msaada kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Kwa mfano, kule kwangu kuna Scheme inaitwa Mang'onyi ni ya siku nyingi; naishukuru Serikali kwamba, imekuwa ikitenga fedha kidogo kidogo, mpaka sasa inafika mahali. Ningeshauri kwamba, ile Scheme ya Mang'onyi ipewe fedha za kutosha ili mradi ule na watu sasa waanze kufaidika, tufunge *chapter* ile tuangalie mambo mengine. Sasa mradi mmoja umechukua miaka saba/sita!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Umwagiliaji, watenge fedha za kutosha Scheme hii iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma, Singida hatukuwa na zao la biashara; ni hivi karibuni tumefika mahali tukakuta alizeti ndio zao letu la biashara. Tumewahamasisha wananchi wameelewa, wamelima kwa wingi kwa muda wa miaka zaidi ya mitatu na wanafaidika sana na zao la alizeti. Vipo viwanda pale vidogo vidogo vinafanya kazi nzuri na wewe unajua hata Dodoma na sehemu nyingine, sasa hivi watu wanatafuta alizeti kwa sababu ni mafuta ambayo yako *recommended* kuwa ni mazuri kuliko mafuta mengine yoyote yale. Sasa kinachonipa tabu ni kwamba, Serikali inakuwa kigeugeu. Bunge hili hili lilifuta hapa habari ya kwamba, lazima tuweke kodi kwa ajili ya mafuta yanaoingizwa kutoka nchi za nje ili kuwapa nafasi wakulima wa ndani, waweze kulima mazao kama haya ya alizeti na wafaidike nayo. Leo tena tunabadili tunasema hapana, tufute ile asilimia 10 ili mafuta ya nje yaingine; hivi Serikali kwa nini mnajigonga gonga hivi?

Taarifa zilizopo ambazo siyo rasmi ni kwamba, wapo wafanyabiashara wanne hivi wanaoingiza hayo mafuta sijui ya akina Korie na nani, ndio waliokwenda kushawishi na kuhimiza. Sasa wewe unawasikiliza watu watatu/wanne, unaacha wananchi mamia na mamia ambao wanalima alizeti, wanaofaidika na mpango huu, unakuja kuwasikiliza wafanyabiashara watatu! Hii ni Serikali ya Wafanyabiashara au ni Serikali ya Wakulima na Wafanyakazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, mimi sikubaliani nalo hata siku moja. Tusiwe kigeugeu, leo kushoto, kesho kulia. Tumekuwa askari, *right turn, left turn,* Serikali nayo inakuwa inafanyiwa *left turn* na *right turn* kila siku. Tukiweka mambo ya

msimamo, yawe ya msimamo.  Nasema hili litatuumiza sisi. Jitihada kubwa ambayo imefanywa na Mkoa, imefanywa na Wilaya, kuwahamasisha wananchi walime alizeti itafifia tena kwa sababu soko halitakuwepo, alizeti haitanunuliwa, viwanda vitafungwa, vijana wanaopata kazi watakosa kazi na akina mama wanaopata ajira watakosa ajira. Sasa tutakuwa tunawaambia nini wananchi wetu wale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili liangaliwe na mimi ningeshauri Serikali iache kujigonga gonga, kesho *left*, keshokutwa *right*!  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Mradi wa Maji wa Benki ya Dunia. Tunashukuru, ulianza mwaka 2003.  Jimboni kwangu, vijiji vya kwanza vile vitano ambavyo wananchi wamechangia ule mradi, mpaka sasa ni vijiji vitatu tu ndivyo ambavyo vimepata maji, vijiji viwili wala havina habari ya maji.  Bado hivi vijiji vitano ambavyo tulianza mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni mradi gani huu ambao utawafanya watu wategemee maji miaka minane? Mwaka 2003 mpaka sasa ni karibu miaka saba/nane mtu anangojea maji; ni mradi wa aina gani huu?  Una jina kubwa "Benki ya Dunia", lakini haufanani na jina hilo.  Ukiuliza swali lolote hapa, wanasema uko Mradi wa Benki ya Dunia mtapata maji. Miaka saba mpaka minane mtu hajapata maji, unaendelea kuutegemea?  Hii wala siyo Singida tu, katika maeneo yote ambayo mradi huu upo.  Sisi tulikuwa wa kwanza kati ya zile Wilaya 12, ndiyo maana tumeathirika zaidi. Ninachokwambia ni kwamba, ni vijiji vitatu tu ambavyo vimepata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashauri Serikali ituangalie sisi wa vijijini, itupatie mradi mwingine kwa sababu huu hautusaidii na umetuchonganisha sisi na wananchi. Tumewachangisha wamechanga, lakini mpaka sasa hawapati maji yoyote. Ikiwezekana, tukimaliza *Secondary School*, tunaingia habari ya afya tunamaliza, sasa mpango ujao uwe ni wa visima vya maji kila kijiji na kila kitongoji, ndio liwe Azimio lingine linalokuja baada ya kumaliza habari ya zahanati na habari ya vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu; wenzangu wamesema sana kuhusu TICTS na TRL. Mimi nawajibika kuuliza; hivi kuna tatizo gani Serikalini; kwa nini Serikali inashindwa kufanya maamuzi? Serikali haifanyi maamuzi mpaka sasa tunagongana na magazeti, mara *statement* hii, mara *statement* ile, kwa sababu Serikali imeshindwa kufanya maamuzi ambayo yako wazi.  Bunge hili tumetakiwa kutoa ushauri; Kamati yangu imetoa ushauri na Wabunge hapa wametoa ushauri, yako mikononi mwa Serikali; hivi kuna kigugumizi gani cha Serikali kutokutoa maamuzi? Sifa ya Serikali nzuri, sifa ya utawala bora ni pamoja na kutoa maamuzi kwa wakati unaofaa.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la TRL toka tumeanza kulizungumza hapa ni lini?  Hawa ndugu zetu wana asilimia 51, sisi tuna asilimia 49, lakini wanashindwa kujiendesha, mishahara mpaka Serikali iwasaidie.  Pamoja na hivyo, kama kazi ni hiyo, basi tungeiachia TRC ya zamani, tuiwezeshe kama tunavyomwezesha huyu Mhindi sasa hivi, ingeendesha tu.  Kwa miaka 10, ilipokuwa *specified* ile TRC hawakupewa chochote;

walitegemea watafaulu namna gani? Huyu kila siku anapewa pesa, watu wakigoma anapewa pesa, kuna nini? Kuna siri gani juu ya hicho kitu? Sasa hizi fedha zinazotafutwa, shilingi bilioni 44 zimepatikana IFC, shilingi bilioni saba zimetoka na nyingine ziko njiani. Asipewe huyu mpaka tuhakikishe kwamba, *management* ya pale imekuwa pamoja na *management* ya kizalendo, maana ukiwapa Wahindi watupu, hela yote inakwenda India. Hakuna Mtanzania pale anayeweza kuona uchungu wa hela hizi.

Wasipewe pesa hizo kutoka Benki ya Dunia mpaka wakubali kwanza kubadilisha uongozi pale uwe uongozi wa pamoja wa Watanzania na Wahindi ndio wapewe. Vinginevyo, mimi nasema itakuwa ni vibaya na tufike mahali tusiende kwenye Uchaguzi Mkuu mwakani huku tunazungumzia habari ya TRL, tunazungumzia habari ya TICTS na habari nyingine. Ajenda hii imalizike, siyo ajaenda ya kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa habari ya TICTS wenzangu wamesema, sasa hivi kwa mfano, walitakiwa wajenge ICDs, wananchi wamejenga ICDs kwa pesa nyingi ili mizigo itoke kule. Watu wa TICTS hawataki kupeleka mizigo ICDs, matokeo yake sasa ni kwamba, zile ICDs ziko *empty.* Wamepoteza pesa zao, lakini ICDs ziko *empty*, hazifanyiwi chochote, hazina mizigo, TICTS inang'ang'ania haitaki kutoa, sana sana kamtafuta mtu mmoja anaitwa Tanzania Road Haulage ndiye amempa kwa mkataba wa kinyemela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais tulipokuwa kule Ikulu alisema, hakikisheni kwamba, mizigo inakwenda ICDs zote. Sasa kwa nini huyu TICTS amechukua majukumu ya kugawa mizigo iende TRH? Mimi naomba Serikali ilifanye kazi hili haraka, kwa sababu tutarudi kule kule kwenye meli 20 na vile vile kutakuwa na matatizo pale bandarini, kwa sababu ICDs sasa wanalalamika kwamba, hela ambazo wamepoteza zitakwenda wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya Stevedoring imezungumzwa na Mheshimiwa Waziri. Nashukuru kwamba, Mtwara umeondoa VAT, Tanga umeondoa VAT, lakini tatizo siyo hilo, tatizo ni kulipisha VAT kwa wenye meli. Mwenye meli ukimlipisha VAT, maana yake ni kwamba, unaifanya Bandari ya Dar es Salaam iwe ghali na kwamba, hawajakuja bali watakwenda Mombasa, watakwenda Beira na sehemu nyingine. Ukifanya utafiti hivi sasa, meli zimepungua, moja ya sababu ni hiyo, pamoja na udhaifu mwingine ambao uko bandarini.

Sasa tatizo hapa ni kwamba, *solution* bado haijapatikana. Umesaidia kupeleka kazi Mtwara, umesaidia kupeleka kazi Tanga, lakini *solution* bado haipo. Ilimradi VAT bado inatozwa kwa mizigo inayopakuliwa na kupakiwa, maana yake na mwenye meli ndiye anayelipa. Kwa hiyo, bandari yetu itaonekana ni ghali na kwa sababu Mombasa hawalipi, Beira hawalipi, bandari zote hazilipi ni sisi tu. Kwa nini tunafanya bandari yetu iwe tatizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali waliangalie hilo ili lisijirudie rudie. Baada ya kusema hayo, mimi nakushukuru sana. Matumaini yangu ni kwamba,

bajeti hii tutaipitisha ili ifanye kazi vizuri lakini wazingatie haya ambayo tumeyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti hii ya Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri sana na moja kwa moja naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii, kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwa kuwa chama cha viwango. Tangu uhuru hadi leo, Chama cha Mapinduzi kimetupatia Marais wa viwango. Hii ni mara yangu ya kwanza kuwa Bungeni hapa, lakini niseme kwamba, tuna Baraza la Mawaziri la viwango, tuna Spika wa viwango, Naibu Spika wa viwango, Wenyeviti wa viwango na Wabunge wa Bunge hili ni wa viwango na wale wanaowania viti hivi 2010 walie tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ni kigezo muhimu sana cha utekelezaji wa Ilani na Ahadi za Serikali kwa Wananchi, pamoja na Ahadi za Waheshimiwa Wabunge. uda ukiruhusu natarajia kuchangia maeneo sita yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni usimamizi wa fedha za Serikali. Ffedha nyingi zinakwenda Wilayani, lakini kwa uzoefu wangu kule Wilaya ya Lushoto, bado *capacity* au uwezo wa Halmashauri zetu kwa maana ya kuwa na wataalamu ni mdogo kuweza kusimamia vizuri fedha za Serikali. Kwa hiyo, niiombe Serikali iangalie eneo hili la *capacity building* kwa maana ya kutuongezea wataalamu. Hapo hapo nishauri kwamba, pamoja na nia nzuri ya Serikali kuwa na wakaguzi wa ndani wanaowajibika kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, aanzishe utaratibu wa Wakaguzi wa Ndani *(Resident Auditors)* katika kila Halmashauri ili fedha hizi za Serikali zisimamiwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nataka kuchangia ni upatikanaji wa mahitaji ya msingi, ibara ya 36 ya Hotuba ya Waziri. Ipo Mifuko ya Maendeleo, Mfuko wa Wanawake, Mfuko wa Vijana na TASAF. Kwa uzoefu wangu ni kwamba, Mifuko hii ama inafanya kazi kidogo au haifanyi kabisa. Naiishauri Wizara ya Fedha au Ofisi ya Waziri Mkuu, ipate taarifa ya utekelezaji wa Mifuko hii ya Vijana na Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nahisi tatizo ni kwamba, kule Wilayani hakuna wataalamu washauri. Hivi nani anawashauri vijana na wanawake kuhusu fursa ambazo zipo? Kama itawezekana, katika kila Halmashauri, awepo afisa wa kusimamia mifuko hii, apite kwenye maeneo ya makundi ya vijana na akina mama, awaelimishe na kuwasaidia namna ya ku-*access* mifuko hii; vinginevyo, mifuko hii itakuwa kwenye makabrasaha, lakini haifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa TASAF ni mzuri sana, lakini nahisi sehemu nyingi hatupati *value for money,* maana dhana iliyopo TASAF sehemu nyingine utakuta ni afisa mmoja tu, halafu anategemea Kamati za Vijiji kusimamia. Sasa Kamati ya Kijiji ukimkabidhi mkandarasi ukaiambia isimamie barabara, hawajui na hawawezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeona kule Wilayani kwetu Lushoto, Jimboni kwangu kuna Barabara za TASAF wamepewa wakandarasi. Nimekagua barabara zile, utekelezaji asilimia tano au kumi, mkandarasi amelipwa pesa zote halafu ameingia mtini, kwa maana hiyo sasa hatupati *value for money.* Kwa hiyo, naishauri Makao Makuu ya TASAF, hebu fanyeni *technical audit* na naomba muanze na Wilaya ya Lushoto ili mtuokoe, tupate *value for money.* Vilevile tushaurini namna nzuri ya kusimamia pesa hizi za TASAF.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala lingine la hali bora ya maisha kwa wananchi. Ibara ya 42 - 43 ya bajeti na naipongeza Serikali kusema chakula kwanza; yapo mahitaji ya elimu, afya, maji, barabara, umeme na ajira. Sisi kule Wilaya ya Lushoto tukizungumzia kilimo, kilimo ndio chakula, kilimo ndio ajira na ndio kipato; kwa hiyo, ndio maisha bora. Kilimo ndio ajira kwa watu wetu takriban asilimia tisini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo chetu kinategemea mvua na mvua mara ipatikane mara isipatikane; na inapopatikana inakuwa nyingi kiasi kwamba yote inakwenda baharini. Mimi naishauri Serikali na nitashukuru kama Waziri wa Maji na Waziri wa Kilimo watafafanua; hivi kule Wilayani Lushoto katika bajeti hii tutasaidiwa kujenga mabwawa mangapi au makinga maji yapi? Kule kwetu wananchi wakikosa mvua, wakikosa kilimo, maana yake ni kwamba, hawana chakula, hawana pesa. Mfano, Wananchi wa Tarafa ya Mlola wanalima maharage na mahindi; mwaka huu jua limekuwa kali maharage yote yamekufa na mahindi yote yamekufa, kwa hiyo, hawana chakula wala kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la kilimo cha umwagiliaji nikiri kwamba, ndio mkombozi wa maeneo mengi ya vijijini. Ninaomba Serikali ilitolee ufafanuzi kwa Mawaziri wanaohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu katika miaka hii mitatu, tumepiga hatua kubwa sana. Wilayani kwetu, kwa mfano, kuna sekondari zaidi ya sabini na asilimia mia moja na ishirini ya wanafunzi waliomaliza shule ya msingi na kufaulu wanapata nafasi ya sekondari, kwa maana kwamba, tunawafagia wote na nafasi zinabaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utaratibu wa Serikali wa kidato cha tano na sita ni shule za bweni. Mimi naishauri Serikali kwamba, wakati umefika tuwe na shule za *A Levels* za kutwa na hili linawezena. Sisi kule kwetu tumekaribia kila kijiji kuwa na sekondari. Utakuta Kata moja ina sekondari saba kama kule Shume. Hawa wanaweza kuwa na sekondari moja ya kutwa hivyo kupanua wigo wa wanafunzi wanaoendelea kidato cha tano na cha sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zahanati tumejenga maboma, tunakaribia kukamilisha maboma takriban kila kijiji. Hoja yangu hapa ni kwamba, je, Wizara ya Afya na TAMISEMI wanasaidia eneo lipi la nguvukazi za wanachi ili kukamilisha zahanati nyingi ambazo wananchi wamejenga kuboresha afya za wananchi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji ni kero. Barabara vivyo hivyo. Ukitaka kufika Lushoto, unapitia njia ya Mombo - Soni - Lushoto, Bumbuli - Mlalo na kwingine kupitia njia moja tu. Njia moja ni hatari. Tunashauri Barabara ya Dochi - Mombo iwe mbadala au barabara ya ziada chini ya TANROADS kuboresha usafiri kati ya Mombo na Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa Wananchi wa Tarafa nne za Kaskazini, barabara inayounganisha Mlalo - Mlola - Makanya - Mshiwi - Tanga ni fupi kwa wakazi wa maeneo hayo. Tumeishauri Serikali, barabara hii iwe ya TANROADS na tunataraji tamko la serikali katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye sera za mapato, *paragraph* ya 44 mpaka 47, suala la bandari limezungumzwa sana. Hivi hatuoni mgodi huu wa kuwa *entry point* ya nchi ambazo ni *land locked*? Hivi kwa nini hatuziboreshi Bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Zanzibar na nyinginezo tuweze kuu-*capture* huu mgodi? Haya matatizo madogo madogo ya utendaji katika Bandari ya Dar es Salaam, mbona yapo ndani ya uwezo wetu mpaka tuunde Tume ya Wabunge! Tunaishinikiza Serikali? Mimi Serikali hii naiamini sana, Serikali ya Mawaziri wa Viwango. Naomba sana suala hili lipatiwe ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye sera za matumizi, ibara ya 55 mpaka 65; pensheni ni kilio cha wengi kwamba, ziwe zinakwenda na wakati na bado ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye sheria za kodi. Lengo liwe kuhimiza uzalishaji, tulinde kilicho chetu. Baadhi ya mapendekezo ya sera za kodi, hayanipi matumaini ya kusimamia kile ambacho ni chetu. Mfano, ukurasa wa hamsini wa kitabu cha Hotuba ya Waziri *paragraph* ya 72(vi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Waziri anapendekeza kufuta msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye chai na kahawa inayozalishwa na kusindikwa hapa nchini. Eti hoja ni kuleta usawa na mazao mengine; hivi mazao yetu yanalingana kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila zao lina matatizo ya kipee na liangaliwe kipekee. Nitazungumzia suala la chai tena nitamke hapa kwamba, mimi ni Mjumbe wa Bodi ya Chai. Nchi yetu imezungukwa na wazalishaji wa chai, Kenya wanazalisha chai mara kumi, Rwanda usiseme, Burundi wanazalisha chai. Hivi sasa katika soko la chai la ndani, kumejitokeza chai chafu ambazo ni hatari kwa afya ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chai kutoka nchi jirani inaingizwa nchini kushindana na chai yetu. Bei elekezi ya mkulima kwa majani mabichi ya shilingi mia moja na kumi;

ni ndogo sana. Ukiweka VAT kwenye chai iliyosindikwa hapa maana yake ni kwamba, sasa unafungua milango chai ya Kenya ije, ya Rwanda ije, chai chafu ienezwe kwenye soko kuathiri afya ya watu wetu na pia kuharibu ajira za watu wetu. Tunahimiza kilimo cha chai kote nchini likiwemo Jimboni kwa Mheshimiwa Shellukindo, ambako chai ndio zao la biashara na ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya mkulima ni ndogo. Tunataka mkulima apanue uzalishaji. Hapa Tanzania *production* kwa heka kwa mkulima mdogo mdogo ni kati ya mia tano na mia nane. Nchi jirani kilo hadi elfu tatu. Mimi napendekeza kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, afute pendekezo hili ili chai yetu iweze kushindana na chai zinazotoka nchi jirani, chai chafu isiuzwe hapa nchini, kilimo cha chai kiongezeke na kipato cha mkulima wa chai kiwe cha kuvutia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme tena nampongeza Waziri wa Fedha na Wasaidizi wake kwa hotuba yake nzuri. Najua kazi ya Wizara ile ni ngumu. Nilibahatika kufanya kazi katika Wizara ile kwa miaka ishirini mfululizo. Mimi nasema wamefanya kazi nzuri sana, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema naunga mkono hoja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki haumtoshi mchangiaji anayefuata, kwa hiyo, kabla sijaahirisha nitatoa matangazo machache.

Kwanza, ningependa kuwataja wachangiaji wetu ambao watachangia kesho; wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, Mheshimiwa Dora Mushi na Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro.

Tangazo lingine ni kwamba, Waheshimiwa Wabunge wote waliojiorodhesha kwenda Kondoa kwenye mazishi ya Marehemu Mzazi wa Mheshimiwa Paschal Degera, gari litaondoka kesho saa mbili asubuhi hapa ofisini.

Kuna tangazo lingine vilevile kwa Wabunge wa CCM kwamba, kile kikao hakipo leo kitakuwepo kesho saa saba.

Kwa hiyo, mpaka hapo nasitisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.40 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,*
*Tarehe 17 Juni, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*